ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini.
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni.
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake.
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais.
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani.
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais.
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu.
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais.
10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.

12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais.
13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais.
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
17.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/\Jimbo la Jang'ombe.
18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni.
19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi.
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.

23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole.
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
26.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi.
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae.
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake.
32.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu.
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais

37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
58.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
65.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
66.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
70.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
71.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
74.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
75.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Saba – Tarehe 19 Disemba, 2013

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti, (Mahmoud Muhammed Mussa) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Hati Mezani Hoja ya Kuliomba Baraza la Wawakilishi la Zanzibar kutoa Azimio Dhidi ya Vitendo vya Udhalilishaji wa Watoto Zanzibar. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 38

Kuanzishwa Sehemu ya Mitambo ya Mazoezi Baraza la Wawakilishi (*GYM*)

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwa na ongezeko kubwa la maradhi yasio ya kuambukizwa (*Non – Comunicable Diseases*) hususani kwa wale watu wenye umri mkubwa na wale wasiofanya mazoezi ya viungo (*Physical Execise*) wakiwemo baadhi ya Waheshimiwa Wawakilishi. Na kwa kuwa inasemekana mazoezi ya kila siku ya viungo husaidia sana kupunguza maradhi hayo.

Je, ni lini Afisi ya Mhe. Spika wa Baraza la Wawakilishi itaanzisha sehemu yenye mitambo ya mazoezi (*GYM*) katika maeneo ya Baraza la Wawakilishi, ili Waheshimiwa Wajumbe waweze kufanya kwa kutumia vifaa hivyo vya mazoezi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba uniruhusu nitoe pole kwa mwenzetu Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi ambae amefiliwa na mama yake jana, nimtakie pole na nimuombee dua maiti huyo roho yake ilazwe mahala pema peponi, amin.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo kwa ruhusa yako kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi naomba uniruhusu nitoe maelezo mafupi na baadae nijibu swali lake Nam. 38.

Sote tunatambua umuhimu wa mazoezi kwa kila binaadamu, ili kuweka mwili wake imara na uwe na kinga kwa yale maradhi ambayo mara nyingi huwapata watu wenye umri mkubwa na ambao hawana utamaduni wa kufanya mazoezi, Ofisi ya Baraza la Wawakilishi inatambua umuhimu huo wa mazoezi.

Hivyo, ni moja ya sababu za msingi za kuanzisha *team* ya Baraza la Wawakilishi *Sport Club*. Hata hivyo, inatambua wazi kuwa mitambo ya mazoezi (*GYM*) nayo kuwa ni kichocheo muhimu katika ushajishaji wa kufanya mazoezi, kwa vile jambo hilo lina gharama, basi linahitaji muda wakujiandaa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 38 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa muda huu bado tunawaomba Waheshimiwa Wajumbe waendelee kufanya mazoezi ya kawaida ya kila siku pamoja na michezo mingine ambayo wameianzisha na huku Ofisi ya Baraza la Wawakilishi ikijiandaa kuanzisha mradi maalum wa kuwa na mitambo ya mazoezi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kuwapongeza Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi pamoja na wananchi wote wanaochukua juhudi za kufanya mazoezi na kuanzisha vikundi mbali mbali vya michezo, jambo ambalo linasaidia kujenga afya zao. Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri naomba niulize swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa katika jibu lake la msingi Mhe. Waziri amesema kwamba serikali imekwama kwa sababu jambo hili lina gharama na akawataka Waheshimiwa Wawakilishi waendelee na kutembea japo wengine ni walemavu wa viungo.

Gharama hizi zinatokana na fedha za walipakodi wa nchi hii na kama walipakodi wa nchi hii ndio waliowaleta Wawakilishi wao katika Baraza hili.Je, lipi bora baina ya gharama ya fedha na afya za hawa Waheshimiwa Wawakilishi waliomo humu na fedha ambazo hupatikana na serikali kupitia kwa walipakodi. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli hakuna mbadala wa afya na mimi nikubaliane na yeye sana kwamba mazoezi ni jambo muhimu na kuwa na mitambo ya mazoezi pia ni muhimu na anachokizungumza yeye suala zima la kuweka mkazo wa kununua mitambo hii ni jambo muhimu. Vile vile ni kweli fedha zinazotumika hapa ni za walipakodi na Waheshimiwa Wawakilishi hawa wanachaguliwa na walipakodi.

Kwa hivyo, kama nilivyomwambia awali kwamba kupanga ni kuchagua nia yetu ni kulifanya jambo hili na yeye ametutanabahisha wakati muafaka. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Mjumbe avute subira na tuwasiliane na wahusika wa Ofisi ya Baraza la Wawakilishi na wengine, ili uwe mmoja katika mradi muhimu tutakaouanzisha katika Baraza la Wawakilishi, kwa ajili ya Wajumbe wa Baraza hili, waweze kufanya mazoezi kwa vizuri kwa kutumia mitambo ya kisasa. *(Makofi)*

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, katika majibu ya Mhe. Waziri amesema kwamba ni muhimu kufanya mazoezi kwa Waheshimiwa na ndio maana Baraza la Wawakilishi likaanzisha Timu ya Baraza la Wawakilishi *Sport Club* kwa ajili ya Waheshimiwa.

Lakini kwa umuhimu huo sio Baraza la Wawakilishi tu hata Mabunge yote ya Afrika na hususan Afrika ya Mashariki wameanzisha *team* za Mabunge na huwa wanashiriki katika mashindano mbali mbali ya Mabunge ya Afrika ya Mashariki.

Je, Mhe. Waziri haoni kwamba ipo haja kwa *team* ya Baraza la Wawakilishi ikafanyiwa mipango na kuwezeshwa kushiriki Mashindano haya ambayo huandaliwa na Mabunge ya Afrika ya Mashariki.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli ni muhimu *team* yetu kushiriki katika Mashindano haya ya Mabunge ya Afrika ya Mashariki na si kwa *team* ya Baraza la Wawakilishi tu, lakini ni muhimu kwa timu zetu zote kuwa na uwezo mkubwa wa kushiriki katika mashindano mbali mbali ya kikanda na kimataifa. Kwa kweli najua tutakapoweza kuimarisha shughuli ya michezo hasa mpira wa miguu, basi jina la Zanzibar litakuwa limekua sana na pia ni kivutio kwa Sekta ya Utalii na siku hizi ni sehemu ya maendeleo makubwa ya kiuchumi na michezo.

Kwa hivyo, wazo lake tunalipokea na tutalifanyia kazi, ili tujipange vizuri *team* yetu hii iweze kushiriki na sio tu katika Mashindano haya ya Kikanda ya Afrika ya Mashariki, lakini iwe na uwezo hata kushiriki kwenye mashindano

makubwa ulimwenguni. Naamini tunao wachezaji wazuri wakiongozwa na Mhe. Hamza Hassan Juma, na wengine na mara hii nitamuomba Mhe. Spika, kwa sababu anayo kawaida ya kukaa *goalkeeper* tuone mambo yake. *(Makofi)*

Nam. 2

Kuenea kwa Plastiki za Viroba na Athari ya Afya na Mazingira

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Kwa kuwa hivi sasa baadhi ya wafanyabiashara wa vileo huleta kwa wingi ulevi wa viplastiki maarufu "viroba" ambao huuzwa kwa bei rahisi na vijana wengi wameanza kujiingiza kwenye matumizi ya vilevi kwa kuanzia na utumiaji huo wa "viroba" vinavyouzwa kama njugu mitaani.

Na kwa kuwa viroba hivi pakiti zake zimeanza kuzagaa mitaani na kuwa tishio kwa mazingira kama vile ilivyokuwa kwa mifuko ya plastiki.

(a) Je, kupitia Baraza hili Tukufu, kwa nini serikali haitoi tamko na katazo rasmi la kupiga marufuku mara moja uingizaji, usambazaji na uuzwaji wa "viroba" Zanzibar ili kulinda afya za wananchi na mazingira.

(b) Kwa nini serikali isirejeshe utaratibu wa zamani wa maeneo ya uraibu wa ulevi kutengwa mbali na makaazi ya kawaida ya watu.

(c) Je, serikali haioni kuacha kuzagaa kwa 'viroba' kunazidi kuwavutia vijana wetu kujiingiza kwenye mitandao ya utumiaji na madawa ya kulevya ambayo tunaimba nyimbo za kupiga vita kila siku.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 2 kwanza naomba nitoe maelezo kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, matumizi ya plastiki duniani yamekuwa makubwa na yanaongezeka siku hadi siku na ni jambo ambalo hivi sasa haliwezi kuepukika. Matumizi hayo yanayoonekana zaidi kwenye utengenezaji wa vifaa mbali mbali vya elekroniki na visivyo vya elekroniki, plastiki hutumika kama (*packaging materials*) kama vile kanga, mashati, viatu hata bidhaa za vyakula mbali mbali zinazozalishwa kwenye viwanda na zinazotoka nje pia. Kutokana na hali hiyo inakuwa ni vigumu kuzuwia uingizwaji wa plastiki

inayotumiwa kwenye bidhaa mbali mbali na inayotumika kwa ajili ya kuhifadhia bidhaa hizo.

Ni vyema ifahamike kuwa kwa wakati huu hapa Zanzibar mkazo uliopo katika Kanuni ya Upigaji Marufuku Matumizi ya Mifuko ya Plastiki, ya mwaka 2001, mkazo umewekwa katika kupiga marufuku mifuko ya plastiki (*plastic carrying bags*) na sio plastiki zinazotumika katika kuhifadhia bidhaa (*packaging materials*). Tukichukua hatua za kupiga marufuku uingizwaji wa plastiki iliyotumika kuhifadhia bidhaa zinazoletwa ni sawa na kusema kuwa bidhaa mbali mbali zisiletwe nchini.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 2 lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Serikali kwa sasa hivi bado haijakataza uingizwaji, usambazaji na matumizi ya viroba kwa madhumuni ya kuhifadhi mazingira kama ambavyo imeruhusu kwa bidhaa nyengine zote zinazoingizwa zikiwa zimefungwa kwenye vifungashio vya plastiki.

   Kuhusu kupiga marufuku viroba, ili kulinda afya za wananchi wetu, suala hili linahitaji kulitafakari kwa kina na kulifanyia utafiti wa kisayansi na wa pamoja kati ya Wizara ya Afya na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, ili kubaini kama bidhaa hiyo haiko salama kwa afya za wananchi wetu. Ikithibitika hivyo serikali itachukua hatua zinazofaa, ili kunusuru maisha ya wananchi wetu.

b) Ni kweli kuwepo kwa maeneo ya uraibu wa ulevi kutengwa mbali na makaazi ya kawaida ya wananchi ni utaratibu mzuri sana na unafaa kuendelezwa. Hivi sasa serikali kupitia Wizara ya Nchi, (AR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum kwa kushirikiana na Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar zinaipitia Sheria ya Vileo, ili kuweza kudhibiti hali iliyopo sasa kwa baadhi ya maeneo ya uraibu wa ulevi kuchanganyika na makaazi ya watu.

   Hata hivyo, bado ipo fursa kwa wananchi ambao wanaona maeneo ya ulevi yamekaribia katika maeneo yao kwenda kwenye Mahakama ya Vileo na kutaka mabaa hayo yaondoke katika maeneo hayo, utaratibu huo bado unatumika.

c) Ni kweli kuzagaa kwa viroba kunazidi kuwavutia vijana wetu kujiingiza kwenye mambo ya mporomoko wa maadili. Natoa wito kwa jamii kwa ujumla, zikiwemo Taasisi za Dini na hasa wazazi

kuwa karibu na vijana wetu na kuwalea katika maadili ambayo yanatukataza kujiingiza katika uraibu wa ulevi na dawa za kulevya, ili kujenga jamii iliyobora.

Hata hivyo, serikali imeliona tatizo hili na hivi sasa serikali kupitia Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto inajiandaa kufanya utafiti, ili kuona jinsi gani kuna ongezeko la matumizi ya ulevi ndani ya jamii, ambapo pia husababisha mporomoko wa maadili na jinsi ya hatua za kuchukua kulipunguza tatizo hilo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri kukiri kwamba suala la viroba watalifanyia kazi, ambapo ukizingaita nalo ni sehemu ya mifuko ya plastiki inayoharibu mazingira. Kwa hivyo, ni lini au muda gani watakaochukua kuliangalia suala hili, kwa sababu linaathiri sana hali hii ilivyo na hasa vijana wetu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa hivi sasa siwezi kutoa kauli ya moja kwa moja ni kipindi gani utafiti huo utakuwa umekamilika, ambao unaweza kubaini hali halisi, kwa sababu kwanza si ofisi yangu ambayo inashughulika kufanya utafiti huo, isipokuwa utafiti huo unaotarajiwa kufanywa na Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza swali la nyongeza Mhe. Waziri. Wakati Mhe. Waziri, alipokuwa akijibu swali la msingi alisema kwamba plastiki zinazofanywa kwa ajili ya vifungashio sio aina ya plastiki ambazo zimepigwa marufuku na kwa sababu plastiki inatumika kwenye maeneo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Kampuni ya Zanzibar *Drop Limited* ilizuiliwa mizigo yao ambayo ilikuwa na vifungashio vya chupa za plastiki pale bandarini, jambo ambalo liliwapa usumbufu mkubwa na kusababisha manung'uniko makubwa kwa serikali. Hivi Mhe. Waziri anataka kunieleza kwamba bado utaratibu wa upigaji marufuku wa aina ya plastiki haujaeleweka hapa visiwani.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, inawezekana kwamba bado ndani ya jamii yetu kuna watu hawajafahamu uhalisia juu ya upigaji marufuku wa matumizi ya mifuko ya plastiki. Kwa hivyo, niseme tu kwamba tutachukua jitihada ya kutosha Kitengo chetu cha Mazingira kutoa elimu hii kwa jamii na hasa katika Taasisi za Serikali kama alivyosema katika suala lililojitokeza bandarini.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa ruhusa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza lenye vifungu (a), (b) na (c).

a) Mhe. Waziri kwa kuwa ulevi ndio mama wa maasi yote, serikali imetuletea mswada juzi tu wa kuunda Baraza la Vijana, ili tuwe na vijana madhubuti watakaoliendesha taifa hili, kuruhusu na huku tunaruhusu uingizwaji wa pombe. Je, lengo la kuwa na vijana madhubuti litafikiwa. *(Makofi)*

b) Kuendelea kuwaachia wananchi kulichapa (kunywa) tembo kwa kuwa linaingizwa kwa wingi. Je, ile dhana ya kujikinga na maambukizi mapya itafikiwa. *(Makofi)*

c) Kuendelea kuletwa pombe kwa wingi hali hii, si kuwaandaa wanywaji wawe wengi.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, Kanuni ya Baraza la Wawakilishi kifungu cha 40(3) kuhusu Maswali ya Nyongeza yanatakiwa yawe mawili sio matatu naomba tukumbushane na tulielewe hilo. Mhe. Waziri naomba ujibu maswali mawili.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, mimi nakubaliana na yeye kabisa kwamba ulevi ndio mama wa maasi hasa unapotumika kwa wingi mno, maana yake wenyewe wanaotumia wanasema ukiutumia kwa wingi ndio unaleta madhara. Lakini kimaadili ambayo mimi na wengi wetu humu tulivyolelewa tunaambiwa kwamba ulevi ndio mama wa maasi na kwa kweli tunatakiwa tusiutumie kabisa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli serikali imeleta Mswada wa Kuanzisha Baraza la Vijana, ni imani yangu kwamba kupitia Baraza hili la Vijana elimu itatolewa, kwa ajili ya kuwaepusha vijana wetu juu ya matumizi ya uraibu wa ulevi na mambo mengine ya mporomoko wa maadili.

Kwa kweli Baraza hili litatusaidia katika kutoa taaluma hiyo, kwa sababu vijana tutakuwa nao karibu zaidi na wao wanaweza kuwafikia wenzao na sisi tunaweza kuwafikia.

Nitakachoeleza hapa ni kwamba sote kwa pamoja tunao wajibu na wala sio serikali peke yake, kuona kuwa kama wazazi au viongozi tunatoa elimu ya kutosha kwa vijana wetu na jamii kwa ujumla kuacha kutumia matumizi ya pombe, ili tuwe na jamii iliyobora.

Kwa hivyo, nawaasa sana Viongozi wa Dini mbali mbali, najua kwamba dini nyingi nazo zimekataza matumizi ya ulevi. Lakini pia natoa wito kwa wazazi kwamba tushirikiane kwa pamoja kutoa elimu juu ya ubaya wa matumizi ya ulevi. Mhe. Mwenyekiti, namuhakikishia Mhe. Mjumbe kwamba ikiwa hakuna watumiaji basi huo ulevi hautoingizwa hapa nchini. Kwa maana hiyo, wajibu wetu ni kufanyakazi kubwa kuona kwamba watu wetu pamoja na jamii kwa ujumla wanasema hapana kwa matumizi ya ulevi.

Nam. 46

Mabadiliko ya Vituo vya Daladala

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kabla ya kujibiwa swali langu Nam. 46, kwanza nataka nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri Mhe. Haji Omar Kheir, kwa kufuatilia majukumu yake na hasa pale anapoulizwa swali na anapotoa majibu katika Baraza hili, basi hwenda *field* kabisa na hivi sasa atajibu swali ambalo ni muhimu sana katika nchi hii.

Sasa chombo hiki bila ya wananchi kisingekuwepo na swali hili ni la wananchi ambao wanaumia kutokana na suala hili hivi sasa. Kwa hivyo, nataka nimpongeze sana nafikiri majibu aliyopangiwa kama yatakuwa sio basi yeye atakuja na jibu lake.

Mwezi wa Novemba mwaka 2013 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye muundo wa Umoja wa Kitaifa imefanya mabadiliko ya Vituo vya Daladala katika makutano ya Barabara katika eneo la Kisiwandui na Baraza la Wawakilishi la Zamani.

(a) Baraza la Manispaa imechukua uzoefu gani katika kupanga vituo vipya kutoka nchi za Afrika Mashariki baada ya kushuhudia usumbufu mkubwa mno wanaoupata wananchi.

(b) Baada ya Kituo cha zamani cha darajani kufungwa, Serikali ina mpango gani wa baadae na eneo hilo au tayari amepewa Mwekezaji Kitega Uchumi kama inavyozungumzwa.

(c) Kwanini eneo la Michenzani Makontena panapojengwa Mnara lisigeuzwe Kituo Kikuu cha Daladala kwa kujengwa miundombinu na vituo vyengine viwe vya kushusha abiria na kupakia.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, na mimi nataka niungane na wenzangu kumpa pole Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi kwa kifo cha mama yake mzazi, Mwenyezi Mungu aijaalie roho ya marehemu ilale poponi, amin.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 46 lenye kifungu (a), (b) na (c) naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Mwenyekiti, Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi baada ya kubaini kuwa eneo la Darajani, limekuwa na msongamano mkubwa wa vyombo vya moto uliochangiwa kwa kiasi kikubwa na daladala, na wakati mwengine ilipelekea kuhatarisha usalama wa wananchi na mali zao na kwa mujibu wa jukumu lililonalo kisheria iliamua kuratibu na kutafuta njia ya kuuondoa msongamano huo.

Hivyo basi, iliandaliwa Kamati Maalum iliyozishirikisha Taasisi mbali mbali ikiwemo Idara ya Leseni na Usafiri, Jeshi la Polisi kupitia Kikosi cha Usalama Barabarani, Vyombo vya Ulinzi na Usalama, Idara ya Mipango Miji, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa na Baraza la Manispaa kutafakari na hatimae kupendekeza nini la kufanya kwa ajili kuondosha msongamano huo. Kamati, hatimae ilikuja na mapendekezo ambayo Baraza inayasimamia kama ambavyo tunayaona.

Kwa bahati, wakati kamati inafanya mapendekezo yake iliwashirikisha wanajumuiya ya daladala na walifahamishwa madhumuni ya zoezi hilo na kukubaliana na uamuzi huo, pia wanafahamu kwamba zoezi hilo ni la muda hadi pale kazi ya utayarishaji wa mpango mkuu wa matumizi ya ardhi utakapokamilika, ambapo itajulikana rasmi wapi kutakuwa na vituo vya kudumu vya daladala.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo sasa kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

(a) Baraza la Manispaa katika kutekeleza hilo limeanza kwa kuangalia uzoefu wa zamani uliokuwa ukitumika hapo Zanzibar, ambapo gari za kutokea namba moja na namba mbili zilikuwa na kituo chake Kinazini, gari za Chwaka na Bambi ambazo hadi leo zinaendelea na kituo chake cha Mwembeladu, gari za namba saba kituo kilikuwa Miembeni na zote zilikuwa zinakuja mjini kushusha na kuchukua abiria tu. Aidha, imeangalia uzoefu wa nchi za Afrika Mashariki ikiwemo Tanzania Bara kwa jiji la Dar-es-Salaam.

(b) Eneo la Darajani penye kituo kilichofungwa kwa sasa ni eneo la wazi kwa matumizi ya wananchi na Serikali, kupitia Baraza la Manispaa litaliingiza eneo hilo katika mpango wa uendelezaji wa eneo zima la Darajani na naomba kulithibitishia Baraza lako tukufu kuwa eneo hilo hajapewa mwekezaji wa aina yeyote.

(c) Eneo la Michenzani limepangiwa matumizi maalum na halitaweza kuwa kituo cha daladala.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu yakusikitisha sana kwa mara yangu ya mwanzo leo kumsikia Mhe. Waziri na ya kuvunja moyo kwa wananchi wa nchi hii. Kwa kweli leo nasikitika sana Mhe. Waziri kwa kuwa suala hili limekuwa kero kwa wananchi na kuleta aibu nchi kutokana na vituo kupangwa katika mazingira ya kusikitisha ambapo hakuna huduma muhimu kama vile vyoo, maji yanatuwama na mengonoyo. Kwa mfano, leo Ofisi ya Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo ndio kituo cha daladala kweli kile, hebu tujipime na wananchi wanayo haki yao pia.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumpa ushauri tu Mhe. Waziri kama kweli tunayo nia njema ya kuwatumikia wananchi. Mbele ya Benki ya *FBME* kuna uwanja mzuri pale, mbele ya *Barclays Bank* kuna uwanja mzuri tu pale na kitu kizuri tulichokifanya cha kupigiwa mfano na tulikuwa tukimshambulia Mhe. Waziri wa Miundombinu bure juzi na hawa wananchi wanayo haki yao katika nchi hii kwa sababu wamo watoto wadogo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, uliza swali.

Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, niko katika swali kwa sababu hili ni suala la nchi ambalo tunalolizungumza na watu wanaumia kule. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, anieleze kwamba katika mipango miji kitu gani kinachokuja mwanzo katika mipango na utekelezaji. Mheshimiwa naomba tuiwasaidie wananchi.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kumsikitikia sana Mhe. Mjumbe ambae ni Mwakilishi wa wananchi anayeonekana kuwa makini, lakini asiyeweza kupima kwamba lipi linawafaa na lipi haliwafai kwa wananchi.

Serikali hii ni makini, tena serikali hii ina watu wanaoweza kufikiri, kupanga na hatimae kutenda. Katika jibu langu la msingi nimesema kwamba vituo hivi ni vya muda tu kutokana na tatizo ambalo limekuwa likitokezea katika

msongamano pale Darajani, na mpaka hapo serikali itakapokamilisha utaratibu wa matumizi ya ardhi kwa mipango miji ya ndani ya mji wetu na hayo masuala yote ambayo ameyasema Mhe. Mjumbe, yatazingatiwa kwa mujibu wa mipango ya miji.

Kwa hivyo, hatuwezi hivi sasa kufanya mambo ambayo ni kinyume na hilo maana haya yanayotokea ni miongoni mwa changamoto ambazo Baraza la Manispaa tunazipata na ni kutokana na kutozingatia hiyo mipango miji.

Sasa Mhe. Mwakilishi ningemuomba awe na subira ili aiachie serikali ifanye wajibu wake wa kufikiri wa kupanga na hatimaye kutenda. Serikali hii inawapenda sana wananchi wake na ndio maana tukafikiria hivyo. Mhe. Mwenyekiti Darajani sote ni mashahidi, wizi wa mifukoni ulikuwa umekithiri, wizi wa kabari ulikuwa umekithiri, watu wengine wakitumia hata silaha ndogo ndogo kuwatisha watu na kuwanyang'anya mali zao. Sasa hii serikali hiyo itakayokuwa haifikirii wananchi wake na kuendelea kuwaacha waendelee kupata tabu.
Sisi tunajua kwamba mpango tuliouweka utawasumbua watu kwa sababu hawajauzoea, kutokana na mazoea ya muda mfupi. Lakini uzoefu wa muda mrefu Darajani hapakuwa na Kituo cha kukaa daladala au kulala daladala. Darajani ni pahala ambapo panatakiwa gari ije, ishushe abiria, ipakie abiria halafu iondoke ndicho ambacho tumekifanya. Mimi ninamuomba Mhe. Mwakilishi alielewe hilo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Swali langu namba mbili hakulisikia Mhe. Haji Omar Kheri, niliuliza katika mipango miji kitu gani kinaanza mwanzo kati ya Mipango au utekelezaji.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Kinachoanza mwanzo ni mipango, unapanga kwanza halafu ndio unatekeleza.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Mwenyekiti nikushukuru na mimi kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti wakati Mhe. Waziri alipokuwa akijibu swali namba 46 kifungu (b) juu ya suala la muekezaji, alisema kwamba Darajani bado hapajakuwa na muekezaji na mimi ninakubaliana na yeye. Lakini moja ya sababu ambazo zinapelekea kulete vurumai au kulete hali ya kutokuwa na mipango mizuri katika mji wetu ni tatizo la fedha na tayari Baraza la Manispaa limeandaa utaratibu mzuri wa eneo zima la Darajani na inasemekana hata michoro tayari imeshaandaliwa.

Lakini tatizo linaloonekana kama kuna *switafahamu* baina ya Baraza na Mamlaka ya Mji Mkongwe katika *design* gani ambayo inaweza ikawekwa

Darajani ili kumpa muekezaji lile eneo. Na kuchelewa kutafuta muekezaji kunapelekea Baraza la Manispaa kutokuwa na uwezo wa kifedha kwa sababu suala la kuekeza lina faida mbili. Moja kupata kipato ili Baraza liweze kujiendesha vizuri lakini la pili kujenga mandhari ya mji wetu. Je Wizara yako haioni kuna haja ya kufanya jitihada ili hizi *switafahamu* zimalizike haraka ili tupate hizo faida mbili kwa wakati mmoja.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti kwanza nataka nilihakikishie Baraza la Wawakilishi kwamba hakuna switafahamu kati ya Baraza la Manispaa na Mjimkongwe, kuna suala la kushauriana kati ya wataalamu wa Baraza la Manispaa na Mjimkongwe, namna ya kuweza kuliendeleza eneo la Darajani. Nakubaliana nae kwamba pindipo Baraza la Manispaa likiweza kupata muekezaji na kuliendeleza eneo la Darajani litakuwa ni sehemu ya kuongeza mapato ya Baraza la Manispaa lakini pia itakuwa ni sehemu ya kukuza uchumi wa nchi yetu.

Hivi sasa Wizara yangu tayari imeshapokea michoro ya awali kwa ajili ya kuliendeleza eneo la Darajani na hapo serikali itakapokuwa ishaipitisha rasmi hiyo michoro kupitia vyombo vinavyohusika basi tunawakaribisha wawekezaji kwa njia ya wazi kuja kuomba tenda na atakaebahatika basi ataweza kupewa ili aweze kuliendeleza eneo hilo.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa naomba nimuulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa maelezo ya serikali ya kuondoa kituo cha daladala pale Darajani ni nia njema ya kupaendeleza ile *corredor* ya Darajani yote. Lakini kwa kuwa mazingira yanaonesha kama serikali haijawa tayari ya kupata muekezaji ama ni mfadhili ama mtu ambaye yuko tayari kujenga na kwa kuwa ndio kwanza Waziri anatwambia ndio sasa hivi wanaanza kujadili michoro iliyochorwa, maana yake hiyo ni kwamba hawajawa tayari kupaendeleza pale pahali. Je, Mhe. Waziri, haoni wamefanya haraka kuwaondolea wananchi ile huduma yao ya daladala pale. Maana sasa ni mwezi wanahangaika au zaidi.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kuliendeleza eneo la Darajani na kupata muekezaji na kuondosha msongamano katika eneo la Darajani ni vitu viwili tofauti. Kuondosha msongamano lina madhumuni yake na serikali imefanikiwa katika kulifanya hilo. Kwa hivyo wananchi niwaombe wawe wastahmilivu kutokana na mipango ambayo imepangwa na serikali kupitia Baraza la Manispaa ya maeneo ambayo yamewekwa kushushia na kupandia abiria.

Naomba nieleweke, serikali haijawakataza wenye daladala wasije kuwashusha mjini na kuwapakia mjini. Kilichoondoshwa ni *stand* ya daladala katika kituo cha Darajani lakini huduma ya kushushwa na kupakiwa abiria ambao ni wananchi ndani ya mji, hiyo ipo katika maeneo tofauti.

Watu wasichanganye mambo na waheshimiwa wawakilishi ninakuombeni sana tuwaeleze wananchi vizuri. Kuna tofauti ya *bus stop* na kuna tofauti ya *bus stand*, serikali ilichokiondosha ni *bus stand* lakini *bus stop* ipo. Lakini kama nilivyojibu kwenye masuala yaliyotangulia ni kwamba serikali ingekuwa haijawa tayari isingeanza kupanga, kwa sababu inapanga ndio iko tayari. Sasa tuacheni tuendelee kupanga na si muda mrefu tutakuja na majibu ya yale masuala ambayo mnayauliza.

Nam. 52

Kutotekelezwa Ahadi ya Kuondosha Ada kwa Gari za Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Itifaki ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi imekuwa ikipewa heshima na uzito mkubwa Tanzania Bara ikiwemo gari za viongozi hao kutolipishwa ada za Uwanja wa Ndege. Wakati gari za viongozi hao zikiendelea kutozwa ada ya Tsh. 500/- zinapoingia uwanja wa Ndege wa Zanzibar.

(a) Kwa nini Waziri ameshindwa kutekeleza ahadi yake ya kuondoa tatizo hilo licha ya kuahidi ndani ya Baraza hili wakati wa Bajeti, ahadi iliyosaidia Bajeti ya Wizara yake kupitishwa kwa urahisi.

(b) Kwanini Wajumbe wa Baraza wapewe heshima kubwa Tanzania Bara kinyume na Zanzibar wakati heshima huanzia nyumbani kama mila na tamaduni za Mzanzibari zinavyojieleza.

(d) Ni lini Serikali itaondoa ada kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ili hadhi yao ya V.I.P iweze kuheshimika kwa vitendo.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako kabla sijajibu suala la Mhe. Jaku Hashim Ayoub naomba nitoe maelezo yafuatayo:-

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar iko kisheria kwa sheria tuliyoipitisha hapa hapa sheria namba 8 ya mwaka 2011 na sheria

ile ina vipengele vingi ambavyo vinasadia kuiendesha mamlaka pamoja na viwanja vyenyewe vya ndege. Naomba ni-*quote* mambo 3 ambayo yangeweza kutusaidia kupata uchambuzi wa baadhi ya masuala kuhusu Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, kwanza tukija katika kifungu cha 11 cha sheria sehemu ya A inataja kazi mojawapo ya Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kama ifuatavyo:-

> "*manage the affairs of the authority in an afficient and cost effective manner"*

Kuendesha shughuli zote za mamlaka katika hali ya ufanisi na kwa bei nafuu, la mwanzo hilo. Katika kifungu cha 23 cha sheria hiyo ambacho kilitaja kwamba inapopitishwa tu sheria ile mikataba yote ambayo ilikuwepo baina ya mamlaka na taasisi nyengine zote zinazofanya shughuli zao ndani ya kiwanja cha ndege kabla ya kuwa mamlaka zitapewa fursa ya kuendelea na *charge* ile ile kwa muda wa miezi 6, lakini ikimaliza miezi 6 kutakuwa na hiari kwa mamlaka kuweza kubadilisha mikataba ile na kutoa matozo mapya.

Kwa hivyo, baadhi ya mabadiliko yaliyojitokeza sio hayo tu yanayoulizwa lakini ya ndani mule, hata wale ambao walikuwa wakifanya kazi zao katika uwanja wa ndege katika kipindi ambacho ni Idara, sheria hii ilipopitishwa walipewa miezi 6 tu kumalizia ile kodi ambayo walikuwa wakitoa kwa wakati ule au malipo waliokuwa wakitoa na mamlaka inapewa nafasi ya kutoza nyengine.

Katika sheria hiyo hiyo Mhe. Mwenyekiti, inatoa nafasi katika kifungu cha 33 kwa Waziri kutunga kanuni za kuendesha mambo yote yanayohusu uwanja wa ndege. Mojawapo katika kifungu (c) *prescribes aeronautical and non aeronautical charges and any other charges as may be deemed necessary.* Kutoa tozo linalohusiana moja kwa moja na shughuli za kiwanda cha ndege au zinazohusiana na maeneo na matozo mengine. Sasa tunapozungumza tunatoleshwa hiki na kile yote hayo yamefanywa katika mipaka ya sheria hii ambayo tumeipitisha wenyewe. Naomba utangulizi huo utoshe,Mhe. Mwenyekiti.

Naomba sasa nimjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake Nam. 52 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Si kweli Mheshimiwa kwamba mimi nilitoa ahadi ya kuondosha kodi ya shilingi 500 na hii hapa *hansard* yangu ninayo ninamtaka kila mjumbe ende kwenye chumba cha *hansard* akachukue *hansard* ya majumuisho yangu ukurasa wa 42 ataona majibu yangu niliyotoa. Mimi nilisema hivi katika majibu yangu nikijibu hoja ya Mhe.

Mbarouk Wadi Mussa, Mhe. Mgeni Hassan Juma, Mhe. Hamza Hassan Juma kuhusu malipo ya maegesho ya magari wanayolipwa madereva wanaohusika katika kiwanja cha ndege cha kimataifa. Utaratibu uliowekwa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kuhusiana na magari yanayoingia ndani ya uwanja ni kwamba, gari zote za binafsi zinatakiwa kulipia zinapoingia ndani. Utaratibu huu umepata baraka za Bodi ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar. Kuhusu magari ya wafanyakazi wanalipa kama magari mengine isipokuwa wao hupata punguzo maalum.

Hili ndio jibu langu na sikusema kabisa kama alivyoni-*quote* Mwakilishi kwamba mimi niliahidi hapa kuwa itaondoka hiyo, si kweli.

(b) Ninaamini mimi kwamba wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi pamoja na Waheshimiwa wengine wote wanapewa heshima zao katika mamlaka ya viwanja vya ndege vya Zanzibar na viwanja vya ndege vyengine. Sasa kama kuna matatizo mengine yoyote niliwahi kusema kwamba suala la *discipline* tusaidiane ili tuwapate wale ambao wamewafanyia vibaya waheshimiwa wapate kushughulikiwa kinidhamu na kisheria.

Na ukenda hata Tanzania Bara gari zote zinalipa ukiingia, ukiwa hutaki ku-*park* unalipa shilingi elfu moja unataka ku-*park* muda wa saa moja utalipa shilingi elfu, ikiongezeka dakika moja baada ya saa moja unalipa elfu mbili na kuendelea. Na hapa kwa sababu aghlabu sisi wajumbe pengine tunaendesha wenyewe yale magari. Kwa hivyo, tunadaiwa sisi lakini tukenda kule tunaendeshewa. Sasa wewe hujui kuwa dereva keshalipa au hajalipa wewe unapita tu.

Kuhusu ukumbi wa *VIP*, uendeshaji wa mamlaka kwa kupitia serikali ndio iliyotoa agizo hili la kulipa ukumbi wa *VIP*, lakini napenda niongeze jambo moja, sisi nchi yetu ni ndogo mambo hatuyajui, lakini kumbi zinaitwa *lounge* ambazo Mashirika ya ndege wenyewe kutokana na tiketi ambayo amekata yule abiria anagharimiwa kuingia katika kumbi hizo. Ndio maana hata huko nje wewe hata ukawa Mheshimiwa bora wende huko *Lounge* utapata *service* nzuri kuliko kutafuta hiyo *VIP* yenye mashaka.

Kwa hivyo, wale wanaosafiri kwenda nje wanajua kwamba ukiwa na *ticket* kuanzia *business class* unapata *facility* ya kwenda kwenye *lounge*. Sasa kutokana na hivyo hapa uwanja wetu wa Abeid Aman Karume ipo *lounge* katika ghorofa ya kwanza, wale wenye *ticket* ambazo ni *business class* waende pale wakadai kwa mashirika, la tunakwenda Dar es Salaam kwa

kupitia hizi ndege zetu ndogo ndogo ambazo ni *overall* hakuna *class* zao, basi tufuate utaratibu ule wa kulipa shilingi 20,000/- kupitia *VIP*. Tumetafuta sisi *document* tumeona kwamba nchi nyingi hasa za Ulaya ukitaka kupitia *VIP* kwa ujumbe maalum kwanza uende ukaombe kibali maalum kwenye ofisi yenu ya ubalozi halafu ilipe malipo ndipo upitie *VIP*. Sasa kwa nini sisi tuwe *exceptional* wakati ulimwengu mzima ndio unavyoendesha shughuli zao.

Kwa hivyo, hebu tutizame kidogo hali inavyokwenda tusipige kelele tu sisi tunataka kwa niaba ya Wizara kuwahudumiia wananchi wote, kuwahudumia waheshimiwa wote, lakini pale ambapo pana kasoro ndio twambieni. Lakini ikiwa kuna jambo ambalo linafana na nchi nyengine basi tulichukulie kwamba linafana.

Kwa hivyo, mpaka sasa hivi kwa kujibu swali (c) bado hakujakuwa na maamuzi ya kuondoa kodi ile katika *VIP lounge*. Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayuob: Pamoja na majibu ya Mhe. Waziri mwenye dhamana wa Wizara hii kutokuwa na afya na ya kusikitisha na kuvunja moyo, nilichomuuliza mimi kwa nini Waziri ameshindwa kutekeleza ahadi yake ya kuondoa tatizo hili na kama *hansard* kasoma upande mmoja tu hakugeuza upande wa pili, aliahidi humu ndani kuwa atalifatilia suala hili. Na hakulifatilia mpaka nimepeleka suala mimi kukumbushia. Ninachosema Mhe. Waziri utakuwa uko tayari mimi kwa nafasi yako kama leo au kesho twende Tanzania Bara kama tutalipishwa pesa mimi na wewe.

Sasa kiongozi ana hadhi gani nchi hii. Juzi Mhe. Mwanajuma Mdachi, aliyefiliwa nimeamua ugomvi mimi na nikamhadithia Mnadhim wa Chama cha Mapinduzi kesi niliyoikuta mimi. Kakamatwa pale mwanamke anataka kuadhiriwa. Sasa kiongozi ana heshima gani nchi hii kwa shilingi 500 na keshalipa anaweka gari pale anateremka kwenda kwenye ndege anaambiwa asiweke gari. Isitoshe kuna mtu mzima katoka Maskat anakwendea magongo ana mkoba mmoja kachukua, kenda kumsaidia mtu tu kuchukua ile mizigo, jamaa kanyang'anywa kitambulisho akaambiwa na *fine* shilingi elfu hamsini au sabiini, huu ndio utendaji bora kweli? Leo Ofisi ya Spika inalia na waheshimiwa humu ndani kupelekwa VIP kulipishwa pale.

Kwa nini itifaki katika nchi moja imesimamia upande mmoja tu kwa Tanzania unapita bila kuonesha kitambulisho chako wala kulipia gari.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti kuna watu duniani wanalipa kodi na kuna wengine hawalipi, sasa ikiwa wale wanaokwepa kodi ndio utasema wale ndio wanaopata au wale wanaolipa.

Shughuli za kiserikali unakwenda na taratibu za kulipa kodi ndio zinavyokwenda.

Mheshimiwa hivi karibuni naomba niwajuilishe Waheshimiwa Wajumbe, katika uteuzi wa wajumbe wakubwa wa kule Marekani kuna masuala mengi huulizwa katika Bunge kubwa lile, mjumbe mmoja kajitoa mwenyewe baada kuandikwa kwamba alikuwa halipi kodi na yeye alikuwa keshateuliwa na Rais katika cheo kikubwa kweli kweli. Sasa inawezekana wewe unapita Dar es Salaam na hawa wanaokupitisha, lakini ndio hawa ambao hawalipi kodi. Lakini mimi binafsi nimeshapita Dar es Salaam mara nyingi sana katika viwanja vyote vya VIP; kile cha Old *Terminal*, ninamuuliza dereva anayenichukua vipi hebu nipe habari tena habari hiyo .....

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Waziri au Mjumbe yoyote aliyeuliza swali ambalo ana madaraka nalo anatakiwa kujibu kwa ukamilifu, usahihi kwa ufupi. Isipokuwa kwamba swali hilo alilotoa Waziri au mmoja aliweza kujibu Waziri mwengine au Mwanasheria. Hapa Mhe. Waziri atueleze kuna kodi na ada, je shilingi 500 ni kodi au ada, naomba atuelimishe.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Shilingi mia tano ni ada, lakini ni sehemu ya kodi ya nchi. Sasa Mheshimiwa mimi nimeuliza hivi asubuhi yule anayenichukua kule Dar es Salaam jibu ni kwamba malipo yapo . Sasa kufanya ushindani wa kwenda haya ni mambo mengineyo. Lakini tukichukua yote yapo au hayapo hapa hiki kiwanja cha ndege hakisimamiwi na sheria iliyo Dar es Salaam, kinasimamiwa na sheria iliopo hapa na Bodi imempa uwezo Waziri kutunga kanuni ambazo zitasimamia uendeshaji wa huo uwanja wa ndege. Sasa hayo ndio maamuzi yaliyopitishwa.

Na ile njia iliyopo pale Mhe. Mwenyekiti ni *excess road* kwa sababu akitaka mtu kutoka Kiembesamaki kwenda kurudi iko nafasi ya kupinda pale, akitaka kuelekea huku katika Baraza la Wawakilishi iko nafasi ya kupita, kwa hivyo sio *main road* ya kusema inam-*block* ni *excess road* ambayo ya kuingia kwenye uwanja wa ndege *purely*, sasa sio kwamba anazuiwa mtu. Ingelikuwa ile *block* imewekwa kati kati ya barabara inaweza kumuunganisha pahali, ingelikuwa jambo jengine. Kwa hivyo, tuitizame ile *excess road* iliyowekwa pale.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Nimemuuliza maswali mawili hakunijibu, nimemwambia kuna mtu anamsaidia mtu mifuko kanyang'anywa

kitambulisho katika uwanja wa ndege, huo huo na alilipishwa *fine*, kumsaidia mtu ndani mule ni makosa. Kamsaidia mizigo kupeleka mpaka pale *checking* .

La pili, nilimwmbia Mhe. Waziri utakuwa tayari kufuatana na mimi mguu kwa mguu kwenda Dar es Salaam kwenda kuthibitisha kama utalipishwa pesa.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mheshimiwa mimi sikuwepo katika tukeo hilo lakini kama lilitokea si tukeo linalokubalika. Kwa hivyo, wale waheshimiwa au wananchi wote wanaoshuhudia mambo hayo waweze kuleta taarifa ili lishughulikiwe. Au yeye anayo ruhusa kumuuliza yule anayehusika pale, jina lake yeye akishatoa kitambulisho chake, atamuuliza jina lake basi atakwenda kulipeleka kunakohusika. Lakini ndani ya Baraza tukishindana namna hiyo itakuwa haiwi.

Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti pamoja na majibu mazuri kabisa na ya ukweli ya Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano naomba kumjibu Jaku Hashim Ayoub, kwa bahati mbaya ametoka, ninafikiri huko aliko ananisikia kwamba mimi niko tayari kwa niaba ya Mhe. Waziri kwenda nae Mhe. Ayoub huko *VIP* anakosema. Inaelekea Mhe. Jaku Hashim Ayoub, hapiti huko *VIP*. *VIP* ukipita ya Dar es Salaam ukifika pale unapokewa na gari chini ya ndege inakupeleka mpaka *VIP* unapokelewa, unatoa *ticket* yako ukimaliza sasa wanakuletea risiti au *voucher* unalipa *cash* au kama hutaki kulipa unaandika hiyo *voucher* Wizara yako, jina lako, na nambari yako ya simu inaletwa huko Wizarani kwako. Kwa hivyo, hakuna kabisa kutokulipa na wala hakuna ugomvi, wao wanakuletea tu ulipe *cash* unapewa risiti, na kwa safari za nje dola 40 Mhe. Mwenyekiti na unalipa unapotoka tu, ukirudi huulizwi. Kwa hivyo, uchaguwe mwenyewe.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Ninakushukuru Mhe. Mwenyekiti na mimi kwa kuniona nataka nimuulize Mhe. Waziri swali moja lenye (a) na (b). Lakini kabla sijamuuliza hilo swali nilikuwa nataka nimwambie tu Mhe. Waziri katika majibu yake hapa alipokuwa akijibu alitumia neno moja si zuri kulitumia kwamba tusipige kelele. Nataka nimwambie kwamba sisi Waheshimiwa Wajumbe hatupigi kelele, tunafanya kazi yetu kwa mujibu wa Katiba. Kazi yetu ni kuuliza maswali na kuisimamia serikali hapa na tunakuuliza maswali kama serikali.Kwa hivyo, hatupigi kelele ni wajibu wetu huo.

Baada ya hilo Mhe. Mwenyekiti sasa ninamuuliza swali langu Mhe. Waziri ile tozo mnayotoza pale nilikuwa nataka kujua ni *parking fees* au ni *gate fees*,

maana kuna viatu viwili tofauti *parking fees* na *gate fees* nyinyi mnatoza kipi kati ya hicho.

(b) Nilikuwa nataka kujua utupe tafsiri ya hili neno *VIP* na kwa nini unatoza kodi kwa kutumia neno hilo. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, kwanza suala lake la mwanzo ni kuwatozo ile *gate fees* kwa kila gari inayopita ambayo ni *private*, itatozwa tozo lile, sio *parking fees*. Kwa sasa *authority* wenyewe wanasema wametoa fursa angalau kwa kipindi ambacho mtu hata aki-*park* atachajiwa ile ile tu mpaka akitoka, basi inakwisha. Kwa hivyo, akienda aki-*park* kule, hachajiwi tena ni ile ile aliyotoa pale tu. Kwa hivyo, yeye mwenyewe ikiwa ata-*park* pale hakuna mtu atakaemwendea kutoa pesa nyengine, lakini akipita anatoa.

Suala la pili la *VIP*, maana yake kwa Kizungu ni *Very Important Person* na wewe ni mmoja wa huyo *very important person*. Lakini maana nyengine ni kwamba kuna fursa maalum uliopewa wewe kutokana na hadhi yako na cheo chako kutumia ukumbi ule au eneo lile kinyume na wale wengine.

Sasa pale pana faida nyingi, unaweza ukenda wewe bado masaa mawili au matatu ya safari unaingia ndani, unakaa juu ya kiti moja kwa moja, unapewa *facility* zote, mizigo yako inachukuliwa inapelekwa, tiketi yako unakwenda kuchekiwa, mambo kadhaa yapo pale na chai ndogo ndogo unaweza kupewa. Ukumbi ule ndio maana yake na wewe huku unazungumza na huku unapoa bukheri hamsa wa ishirini, sasa zile ndio *facility* ziliopo.

Lakini kwa sababu wewe ni mkubwa na mambo hayo na wale wafanyakazi wanataka kulipwa na ile mamlaka inajiendesha na ulimwengu ushachukua *fashion* hiyo. Kwa hivyo, unatozwa zile kugharamia baadhi ya gharama zilizopo pale.

Nam. 27

Mpango Madhubuti wa Kusomesha Wataalam Katika Sekta ya Mafuta Zanzibar

Mhe. Hamza Hassan Juma – Aliuliza :-

Kwa muda mrefu sasa Zanzibar imekuwa ikilalamika kuwa nafasi za ajira katika sekta mbali mbali ikiwemo ya utalii zinachukuliwa na wasiokuwa Wazanzibari na hoja kubwa inayojengwa dhidi ya madai hayo ni kuwa Wazanzibari hawana sifa za kitaalamu za kutosha kwa nafasi hizo.

(a) Serikali ina mpango gani madhubuti na wa muda mrefu wa kuwasomesha Wanzibari katika sekta ya mafuta ili uzalishaji utakapoanza malalamiko ya kuchukuliwa ajira na wasiokuwa Wazanzibari yasije kujirudia katika sekta hii ya mafuta.

(b) Katika miaka ya karibuni, kuna wafadhili walituahidi kusomesha baadhi ya vijana wa Kizanzibari katika fani za mafuta, lakini kwa bahati mbaya mpango huo wa ufadhili ulishindwa kutekelezwa.

Serikali imejiandaa vipi kutenga fedha zake kwa ajili ya kusomesha Wazanzibari katika fani mbali mbali za mafuta kutokana na uzito wa suala hili badala ya kutegemea wafadhili pekee ambao baadae hutuacha mkono.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:-
Mhe.Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 27 lenye kifungu (a), (b) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu kwa mashirikiano makubwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, imeandaa utaratibu maalum kuwahakikishia kupata mikopo wanafunzi wote ambao wana sifa za kuendelea na mafunzo ya mafuta na Gesi na yanayohusiana na hayo. Vile vile, kumeandaliwa zoezi maalum la kuwahamasisha wanafunzi wanaomaliza kidato cha 6 kuelewa na kujipangia katika somo hilo.

(b) Mhe. Mwenyekiti, katika kujibu swali (b), ambalo limefanana na (a), serikali imejiandaa kwa kuhakikisha kuwa fungu la fedha za mikopo katika Bodi ya Mikopo linaimarisha na sekta ya mafuta na gesi inapewa umuhimu zaidi.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba niulize swali dogo la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, pamoja na jitihada inayofanywa na wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuweza kuwapatia mikopo wale wanafunzi ambao wanaotaka kusoma katika masuala yanayohusu nishati ya mafuta na gesi.
Lakini vile vile, Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi kilichopita tulipata taarifa kwamba kuna mashirikiano baina ya Serikali ya Zanzibar na Serikali ya *Ras el Khaimah* katika kusaidia kutoa mafunzo mbali mbali ya vijana wetu hasa katika hii sekta ya gesi na mafuta.
Je, katika haya mashirikiano ya serikali zetu hizi mbili, je, kuna nafasi ngapi za masomo ambazo zinagharimiwa na wenzetu hawa wa *Ras el Khaimah*. Je, mpaka sasa hivi kuna wanafunzi wangapi ambao wanafadhiliwa na Mfuko wa *Ras el Khaimah* na wako katika nchi gani na gani ili tuweze kujua hizo takwimu zao.
Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, bado tunashirikiana na wahisani mbali mbali katika suala hili hususan la mafunzo ya mafuta na gesi. Wapo wanafunzi ambao tayari wako vyuoni kwa ajili ya kusoma na wanafunzi ambao tumewapeleka kusoma katika somo hili ni 29 wakiwemo katika vyuo mbali mbali. Wanafunzi 11 wako katika Chuo Kikuu Dodoma, wanafunzi 12 wako Chuo Kikuu Dar es Salaam, wanafunzi 2 wako China, wanafunzi 2 wako Rusia, wanafunzi 2 wako Sudani na mwanafunzi 1 yuko Uingereza. Kwa hivyo, niseme kwamba

kwa ushirikiano na wahisani pamoja na wafadhili basi tunajitahidi kuwasomesha wanafunzi hawa na tutajitahidi kusomesha wanafunzi wengine pale tu itapobidi kufanya hivyo.

Utaratibu

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, wanafunzi wanaofadhiliwa na Serikali ya *Ras el Khaimah* katika suala zima la nishati na gesi hii amenieleza jumla jumla tu, nilikuwa nataka *specific* ni wanafunzi wangapi wanaofadhiliwa na Mfuko wa Ras el Khaimah.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, wanafunzi waliofadhiliwa na wenzetu wa Ras el Khaimah ni wanafunzi watatu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri na kwa sababu yeye ni mwanamme labda hatanishushua, naomba nimuulize swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, bajeti ya mwaka 2009, 2010, 2011 serikali ilituahidi kwamba ilipatiwa nafasi 10 za wanafunzi kwa ajili ya fani hiyo ya mafuta na gesi katika nchi ya *Ras el Khaimah*, leo Mhe. Naibu Waziri anatwambia kwamba nchi hii imewafadhili wanafunzi watatu. Hebu atwambie Mhe. Naibu Waziri, wale wanafunzi saba ambao tuliahidiwa miongoni mwa kumi, kwa nini hatukupata ufadhili.

Pili, hao wanafunzi 29 ambao tumeambiwa wako katika nchi mbali mbali naomba kujua Mfuko wa Bodi ya Mikopo Zanzibar, walitumia vigezo gani ili kuwapatia wanafunzi hawa 26 kati ya 29 mikopo hiyo na watatumia muda gani wa mafunzo yao kwa fani hiyo ya mafuta na gesi.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, suala la mafunzo kwa *Ras el Khaimah* ni suala endelevu na si suala la mwaka mmoja kwamba ndio litakamilika. Tumeanza na wanafunzi wawatu na mwaka huu wanakwenda watatu na mwaka ujao watakwenda tena wanne, watakuwa kumi wameshatimia.

Kwa upande wa Mfumo wa Elimu ya Juu hapa unasaidia katika mafunzo mbali mbali. Mhe. Mwenyekiti, napenda kumjibu Mheshimiwa kwamba wanafunzi hawa walioko Dodoma wanaosoma wamepata mkopo kutoka Mfuko wetu wa Zanzibar na Bodi ya Mikopo, hapa umetoa upendeleo makusudi kwa ajili ya wanafunzi hao kwa kusoma huko Dodoma. *Course* ya mafuta na gesi inachukua kama *course* za kawaida ya miaka mitatu kwa kuanzia katika Chuo Kikuu kama utaratibu unavyoendelea.

Tunachokifanya sisi sasa hivi ni kwamba, tunawahamasisha wanafunzi wanaosoma Kidato cha 5 na 6 wakishamaliza tu wakitaka kuingia vyuoni wachukue masomo ya mafuta na gesi, tunawahamasisha wafanye hivyo na wanakubali, lakini wanatakiwa wawe wamepasi katika zile *subjects* ambazo zitafaa katika yale masomo yenyewe, wawe wamepasi *chemistry*, *biology*, *physics*, kwa sababu hayo ndio mambo wanayosomea sana katika masuala ya mafuta na gesi. Kwa hivyo, hicho ndicho kigezo tunachokitumia, kama

anakwenda Chuo Kikuu hakupasi masomo hayo, hawezi kuchukua masomo ya mafuta na gesi.

Nam. 11

Hatua za Kulinda Mifugo Zanzibar

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza:-

Zaidi ya asilimia thelathini ya wakaazi wa Jimbo la Wawi katika vijiji vya Furaha, Wawi, Mvumoni, Mfikawa Uwandani, Ng'ambwa pamoja na Vitongoji wameekeza maisha yao katika mifugo ya Ng'ombe, Mbuzi na Kuku. Kwa kuwa miongoni mwa mambo yanayorudisha nyuma ni pamoja na mifugo hiyo kuliwa na mbwa.

Ni lini serikali kupitia wizara yako na kwa kushirikiana na Serikali ya Wilaya na Shehia itawasaidia wafugaji kwa kuwaangamiza mbwa wanaoranda ovyo mitaani.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 11 la Mwanamapinduzi wa Zanzibar. Kabla ya kujibu naomba kutoa maelezo machache.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Mifugo na Uvuvi ina jukumu la kutoa huduma za kinga na tiba kwa maradhi ya mifugo pamoja na ushauri wa ugani (*extension*) juu ya ufugaji bora ili tija iweze kupatikana.Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba kujibu swali kama ifuatavyo:-

Ni kweli lipo tatizo la baadhi ya mifugo kuliwa na mbwa katika baadhi ya maeneo ya Unguja na Pemba na hii hutokana na baadhi ya wafugaji wa mbwa kutokuwapa mbwa wao chakula cha kutosha na kuwaacha wakizurura kujitafutia chakula wenyewe. Wito wangu ni kwamba wafugaji wa mbwa wawadhibiti mbwa wao na Masheha wawe na utaratibu wa kuweka orodha ya wafugaji wa mbwa katika maeneo yao na kujadiliana nao jinsi ya kuzuwia au kupunguza mbwa wanaozurura.

Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu inatoa huduma za kufunga uzazi mbwa na paka. Hivyo, wafugaji wanaweza kuwapeleka mifugo yao kupatiwa huduma hiyo. Aidha, napenda kuwashauri wafugaji wa ng'ombe na mbuzi wapendelee kulaza mifugo yao karibu na makaazi yao badala ya kuwalaza porini kwa sababu tabia hii ndio inayochangia wizi na hujumu kwa mifugo hasa ndama ambao wanashindwa kujilinda dhidi ya mbwa na hususan katika Jimbo la Wawi.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri ambaye swali langu amelijibu kwa umakini wa hali ya juu, naomba nimuulize swali dogo la nyongeza. Kwanza niipongeze serikali kwa kuweza kujitahidi katika masuala ya uzazi wa mpango hata katika mifugo ya mbwa.

Kwa kuwa Mhe. Mwenyekiti, wafugaji wa mbwa katika eneo la Vitongoji hawana uwezo wa kuwadhibiti mbwa wao na kwa kuwa hawa mbwa wengi wanaohujumu hii mifugo yetu ni pamoja na mbwa pori ambao hawana

mabwana na pia siku za nyuma kulikuwa na utaratibu wa watu wawili pale Bwana Abdalla Upepo na Bwana Ajili Khamis, walipewa bunduki za magobole na waliazimwa na Jeshi letu la Polisi, zilikuwa zinasaidia sana bunduki hizi kuangamiza hawa mbwa ambao wanahujumu mifugo ambao moja kwa moja wanapoteza lile lengo la serikali la kupunguza umasikini na kujiongezea kipato kwa wananchi wake, kwani mbwa wanahujumu vibaya sana mifugo hii.

Je, Mhe. Naibu Waziri, ni utaratibu gani wa serikali utakaoandaliwa kuwapatia Bwana Ajili Khamis Abdalla wa Vumba pale na mwenzake Bwana Abdalla Upepo yale magobole ili waweze kuangamiza wale mbwa ukitilia maanani kwamba yale waliokuwa wakiazimwa na Jeshi la Polisi, sasa yameshakuwa nyang'anyang'a hayafai tena wala hayarushi baruti.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, nataka niwaambie Wawakilishi na wananchi wote waweze kutuelewa kuwa serikali imeridhia mkataba wa *WSPA* ambao umetiwa saini mwaka 2000 wa kujua haki za wanyama. Ni vigumu sana sasa kumpiga risasi mbwa. Lakini serikali vile vile, baada ya kutiliana saini mkataba huu inatambua kuwa haki za mnyama zitapatikana, moja ya haki hiyo ni kuwalinda wanyama, kuwapa chakula, kuwatunza, lakini na lengo la wizara ni kuwashajihisha wafugaji wa mbwa sasa waweze kujua mbwa wao ili waweze kukidhi mahitaji ya mbwa wale, lakini kama hawawezi tuweze kuwahasi wasizaane kwa wingi.

Hili la mbwa hawa waliokuwa hawana wenyewe tutalichukua na tulifanyie kazi kwa sababu tumetembelea kule Jimbo la Wawi katika sehemu moja inaitwa Mochari, tulikwenda tukawakuta mbwa wengi sana wanaoranda, lakini hili tutalichukua na tutalifanyia kazi.

Nam. 56

Kutekelezwa Agizo la Mhe. Rais

Mhe. Salma Mussa Bilali - Aliuliza:-

Katika utaratibu wake wa ziara za kila Mkoa Mhe. Rais wa Zanzibar, alitoa agizo kwa Wizara ya Afya kufuata utaratibu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali wa kusaidia nguvu za wananchi pale wanapoanzisha Ujenzi wa Vituo vya Afya.

(a) Je, ni hatua zipi zilizochukuliwa katika utekelezaji wa agizo hilo la Mhe. Rais.

(b) Na katika utekelezaji huo kama umeshapangwa, ni lini Ujenzi wa Kituo cha Afya Mpapa utamalizwa ili kusaidia nguvu za wananchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda na mimi nichukue fursa hii kumpa pole Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi, aliyefiliwa na mama yake mzazi. Mwenyezi Mungu ampe subira kwa sababu tunaelewa uzito wa msiba wake.

Mhe. Mwenyekiti, naomba uniruhusu kwa idhini yako niweze kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam.56 lenye kifungu (a) na (b) kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, agizo la Mhe. Rais wa Zanzibar alilotoa kwa Wizara ya Afya kusaidia nguvu za wananchi pale palipoanzisha ujenzi wa vituo vya afya, limeanza utekelezwaji wake na kufikia hatua zifuatazo:-

1. Kuvitambua na kuviratibu vituo vyote vya afya pamoja na nyumba za wafanyakazi vilivyoanzishwa ujenzi wake ili kujua vipo wapi na vingapi,
2. Kufanya tathmini na kujua ni kiasi gani gharama zinazohitajika kwa ajili ya umalizwaji wa vituo au nyumba hizo ili kukamilisha ujenzi wake,
3. Kutafuta fedha kwa kuweka fungu kwenye bajeti ya miradi ya maendeleo serikalini na kwa kupitia wafadhili mbali mbali wa maendeleo ambao wanafadhili miradi ya afya,
4. Hatimae kuja kupanga ratiba ya ujenzi wa vituo hivyo kwa uhalisia wa kituo, kipi kianze kulingana na mahitaji ya sehemu husika. Kwa mfano umbali wa kituo kingine na kinapojengwa kituo kipya au wingi wa watumiaji watakaotumia kituo husika na kadhalika.

Kwa mantiki hiyo, kituo cha Mpapa kitajengwa baada mipango ya fedha kukamilika na kupangiwa ratiba kwa vigezo vilivyowekwa hapo juu.

Mhe. Salma Mussa Bilali: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kumuuliza swali la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri, kwa kuwa jamii haielewi mipangilio yote hiyo ambayo ameieleza hapa na kwa kuwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali tayari utaratibu wake unaeleweka, endapo ujenzi wake utafikia hatua ya kuezeka, jamii inakabili Wizara ya Elimu kwa kumalizia hatua iliyobakia.

Je, wizara yako inatoa wito gani kwa wananchi ambao wanaazisha vituo hivyo kwa ajili ya kumaliziwa vituo vyao.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Afya na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ni vitu viwili tofauti, taratibu za ujengaji wa skuli na vituo vya afya ni tofauti. Kama mnakumbuka Waheshimiwa kuna semina mlifanyiwa tukaambiwa kwamba vituo vya afya vimetosh, na wananchi wanapojenga mara nyingi hawatuarifu tunakuja kushtukia tu kwamba vituo vimeshajengwa.

Katika ziara za Rais alipopita na kutoa agizo hilo imebidi tulichukue agizo kwa sababu tumeagizwa, lakini kwa utaratibu wa vituo vya afya kama mtu kaamua au shirika limeamua kujenga, sisi kama Wizara ya Afya, utaratibu wetu ni kuhakikisha kwamba tunatia vifaa, tunaweka wafanyakazi, tunalipia huduma za maji na umeme. Hivyo ndivyo taratibu zetu na sio kumaliza vituo ambavyo vimeanzishwa na wananchi.

Lakini kwa vile agizo limetolewa inabidi tulitekeleze. Sisi wajibu wetu tukishakabidhiwa kituo tunakiendeleza kama kinahitaji matengenezo tunakifanyia ukarabati, kwa sababu sasa inakuwa lile tayari ni jukumu letu.

Lakini sio kwamba wajenge wakifika kozi mbili sisi tukamalize, utaratibu huo kwenye Wizara ya Afya haupo.

Na ili kulihakikisha hilo tuna vituo ambavyo tunatakiwa tuvifanyie marekebisho ambavyo vimeshajengwa huko nyuma na ambavyo hivi sasa kabla ya hivyo ambavyo wananchi wamevijenga tunatakiwa tuwe na shilingi bilioni moja, 337 milioni na laki 5 kwa ajili tu ya kuvikarabati vituo hivyo, ukiachilia mbali hivyo vituo ambavyo sasa hivi tumekabidhiwa na Rais ambayo navyo vina mahitaji ya kiasi cha shilingi 352,433,600.

Kwa hivyo, ukichukua mzigo huo ukitizama na bajeti tuliyonayo Wizara ya Afya hatujaelewa ni lini tutavikamilisha, lakini tutajitahidi kufanya hivyo tufanye ukarabati wa vituo na hivyo vilivyoanzishwa vinjengwe.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuuliza swali moja la nyongeza ambalo lina sehemu mbili. Mhe. Naibu Waziri katika majibu yake mazuri alisema kuwa tayari sheria wameshaweka kuwaelimisha wananchi wasiendelee kujenga vituo vya afya. Lakini huku kuna kauli ya Mhe. Rais, kuwa bado iendelee.

Mhe. Naibu Waziri, hapo itakuwa ni kauli sahihi kati ya nyinyi wenyewe mliokwishaweka sheria na kule kuna kauli ya Rais kwa wananchi.

Pili, lakini vile vile hamuoni kuwa hamkumtendea haki Mhe. Rais baada ya nyinyi kutunga sheria na kwenda kumueleza hatua iliyofika mpaka kafika Mhe. Rais kutoa kauli hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, Rais ana mamlaka ya kusema na kuoa amri, kuwa vituo vimetosha. Waheshimiwa tulifanya semina na baada ya kuona kwamba tatizo limejitokeza na katwambia kwamba tumalizie, pia tulikwenda kwa Mhe. Rais tumuonyesha hali halisi ilivyo. Makubaliano ya Rais na sisi ni kwamba tuangalie wale wanaotaka kujenga, sehemu inayotaka kujengwa, haja ya kutaka kujengwa, hatukusema kwamba vituo visijengwe kabisa.

Kama pana watu kituo hakitoshi itabidi tujenge, tunachotakiwa tutoe ushirikiano na wale wanaojenga waje kwetu, tuwape ramani, tuwafuatilie wajenge vituo wamalize na sisi tusifanye kazi hiyo. Si muda mrefu Wizara ya Afya itatoa tangazo ambalo tayari tumeshaliandaa jinsi gani utaratibu huo ufuatwe. Kwa hivyo, amri ya Rais itatekelezwa na hayo mengine pia yatafanywa.

Nam. 64

Changamoto ya Rasilimali Watu Katika Vituo Vya Afya

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Aliuliza:-

Kwa kuwa inafahamika kuwa miongoni mwa changamoto za Wizara ya Afya ni nguvu kazi kutokana na idadi kubwa ya Vituo vya Afya na wingi wa hospitali. Na kwa kuwa inafahamika kuwa Pemba kuna upungufu mkubwa wa rasilimali hiyo.

(a) Je, ni sababu gani zinazopelekea upungufu huo wakati kila mwaka Chuo cha Sayansi ya Afya na vyuo vya nje ya Zanzibar navyo vinasomesha wanafunzi kutoka Zanzibar.

(b) Kuna utaratibu gani wa kugawana rasilimali watu hao wanaotoka vyuoni.

(c) Kwa vile ajira sasa zinasimamiwa na Tume ya Utumishi kwa kutangaza kwenye vyombo vya habari ikiwemo magazeti ya hapa nchini Tanzania na katika tangazo kuna kipengele cha tangazo hilo kwamba anaeomba ajira awe Mzanzibari, hatuoni hicho ni kikwazo kama kutakuwa na mtu nje ya Zanzibar, lakini anataka kutoa huduma Zanzibar kwa uchaguzi wake mwenyewe.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. M wenyekiti, kwa ruhusa yako napeba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam.64 kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, Chuo chetu cha Afya kinatoa wahitimu wa kada tofauti na kwa sasa tuna kada 7 ambazo zinasomeshwa chuoni hapo. Lakini mahitaji ya wafanyakazi wa kada hizo zinazotolewa kwenye vituo na hospitali. Na kwa vile anayetaka kusoma huchagua yeye anachotaka kukisoma, mara nyingi uwiano wa mahitaji na uchaguzi wa wanafunzi vinapishana.Ukiangalia takwimu ya idadi ya rasilimali watu wa kada za afya kuna upungufu kote Unguja na Pemba, lakini kwa kiwango tofauti na Pemba ndiko kwenye upungufu mkubwa zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, sababu kubwa ya hali hiyo ni kama zifuatazo:-

1. Wafanyakazi wa afya kabla ya kuajiriwa wanafunga mkataba na kuapa kwamba watafanya kazi popote Zanzibar, lakini mara tu wakeshaajiriwa wao wenyewe, wazee na jamaa zao na hasa watoto wenye nasaba na wakubwa, wanataka wachaguwe wao wapi wapangiwe kazi badala ya wizara kuwaangalia wapi wana mahitaji kwa mujibu wa ugawaji wa wafanyakazi.

2. Idadi kubwa ya Hospitali na vituo vya Afya ilioko Pemba ukilinganisha na ukubwa wa kisiwa na idadi ya watu walioko, ambavyo vimejengwa kupitia vyanzo mbali mbali bila ya kuzingatia kwamba baadae tutahitaji wafanyakazi katika vituo hivyo.

3. Wahitimu kutoka Pemba kukataa kurudi kufanya kazi Pemba, wakipangiwa hutoa visingizio mbali mbali na ukiwapeleka wanakimbia na kuacha kazi jambo ambalo linawafanya hata wale wa Unguja wanaopangiwa kufanya kazi Pemba nao kukataa. Mfano hai

ni wafanyakazi waliopelekwa Pemba mwaka juzi walikuwa 162 na 36 kati yao walikimbia muda mfupi tu baada ya kupelekwa. Baadae mmoja mmoja wakaanza kurudi Unguja kwa njia na sababu mbali mbali wanazozijua wao wenyewe na waliowarudisha. Na wengi wao wanaotoka Pemba. Ilibidi wale wanaotoka Unguja wachache waendelee kubaki kwa kipindi cha zaidi ya miaka miwili kwani wangeondoka basi ingebidi hospitali zifungwe. Baada ya waajiriwa wa mwaka huu kuanza kwenda Pemba, hivi sasa wafanyakazi 74 waliotoka Unguja wameanza kurudi na kufanya idadi ya wafanyakazi wenye asili ya Pemba waliopelekwa huko mwaka huo waliobaki Pemba karibu sawa sawa na hakuna.

4. Sababu nyengine ni wafanyakazi kuondoka kwenda kusoma Unguja na Pemba bila ya kuzingatia muda wa miaka miwili ya kisheria au zaidi ya kufanya kazi baada ya kuajiriwa na pia kwenda kusoma masomo ambayo sio ya kada za afya, bali masomo ya sanaa au yasiofanana na kada zao za msingi na wakirudi kukataa kufanya kazi yao ya awali na kulazimisha kupangiwa kazi za utawala.

(b) Mhe. Mwenyekiti, tunapata wahitimu wa kada za afya tofauti kutoka Chuo cha Sayansi za Afya Mbweni na vyuo vyengine vya nje ya Zanzibar. Utaratibu wa kuwagawa wafanyakazi hao wakishaajiriwa kwa hivi sasa unategemea mahitaji ambayo yapo katika muongozo uliotengenezwa na wizara yaani *"Minimum Staff Requirement*", ambayo imeweka idadi ya kila kituo au hospitali kuwa na wafanyakazi angalau kwa kiasi cha mahitaji ya msingi ili huduma ziweze kutolewa. Muongozo huo ulitengenezwa baada ya kuona kwamba kulikuwa na mgawanyo wa wafanyakazi usiozingatia mahitaji na kufanya vituo vyengine viwe na wafanyakazi wa ziada na vyengine havina hata wafanyakazi wa msingi. Muongozo huo umeifanya wizara kujuwa ni wafayakazi wa kada gani wanahitajika wapi na kwa idadi gani. Na kwa kutumia muongozo huo ndipo tulipoweza kujuwa kuwa Pemba kuna upungufu wa asilimia 70% na Unguja asilimia 48% ya wafanyakazi wa kada za afya.

Wafanyakazi hao hugaiwa kwa upande wa Unguja na Pemba kulingana na mahitaji kutokana na ukubwa wa kituo au hospitali, idadi ya watu na huduma zinazotolewa. Wafanyakazi hugaiwa kwa upande wa Unguja na Pemba na kwa wale wafanyakazi wanaotokea Pemba wote hupangiwa kazi Pemba na kwa vile idadi haitoshi

kulingana na mahitaji, basi na wafanyakazi kutoka Unguja nao hupelekwa Pemba ili kukidhi mahitaji.

c) Kipengele cha kuwa anaombea ajira sharti awe Mzanzibari, ni sehemu ya sheria iliyotungwa na Baraza hili kwamba nafasi kwanza wapewe hao ili kulinda nafasi chache zilizopo. Lakini hata hivyo kutokana na upungufu wa kazi kwa upande wa kada za afya, Wizara ya Afya inawaombea ajira wote wenye sifa za kuajiriwa bila ya kujali wapi wanakotoka hasa kwa Tanzania Bara.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kumuuliza swali dogo la nyongeza.

Alisema kwamba kuna watumishi ambao wameajiriwa katika mwaka huu na hawajaenda kuripoti katika vituo vyao wakipelekwa hawaendi, nilikuwa naomba kumuuliza. Je, wafanyakazi waliokuwa wameajiriwa hawajaenda kuripoti katika kituo chao kama wizara imechukua hatua gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, kilichopo kwa uhalisia wanafunzi wa Wizara ya Afya wanajisomesha wenyewe, wakishajisomesha Wizara ya Afya inawaajiri inakuwa ni wafanyakazi wa Wizara ya Afya, wanapokuja kuomba kazi tunapitia taratibu zote, tunawaombea kazi na tunawapangia vituo, tukishawapangia vituo kwa mujibu wa mahitaji wakiona hawaridhiki na vituo walivyopangiwa, wakiona wamejaribu kila njia wanayoitaka na hawakufanikiwa, huwa wanaamua kuacha kazi.

Kwa hivyo, tunashindwa kuwalazimisha kuwafanyisha kazi watu wasiyetaka kufanya kazi waliyojisomesha mwenyewe, lakini kwa wale ambao serikali inayowasomesha kupitia ufadhili mbali mbali, hata Rais aliwaambia kwamba kama wewe unajiona hutaki kufanya kazi, basi tulipe pesa zetu.

Kwa hivyo, kwa wale ambao wanajisomesha wenyewe tukiwapangia kazi na hasa ukimpangia Pemba, hata waliotoka Pemba ikiwa hawataki kwenda huko tunawaachisha kazi, tunaweka nafasi zile kwa wengine wanaotaka kuajiriwa waje waajiriwe.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwanza ninataka nimpongeze sana leo Mhe. Naibu Waziri wa Afya, kwamba yupo mtulivu, ametulia kabisa na anatujibu maswali yetu kwa kweli sote tunaridhika na ninaomba aendelee na *style* hiyo hiyo. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kumaliza hilo, sasa ninataka niendelee na maswali yangu ya nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa upande wangu ninataka niipongeze sana serikali hasa kwa kuweza kuwajali wananchi kwa kusaidia nguvu za wananchi wa Jimbo la Kwamtipura, kujenga kituo cha afya. Na sasa hivi tunaishukuru sana wizara kwamba wameirejesha ile kambi ya macho katika Hospitali ya Kwamtipura, kwa kweli hili tunawashukuruni sana. (*Makofi*).

Lakini swali langu lipo hapa. Mhe. Mwenyekiti, katika maswali alipokuwa akijibu Mhe. Naibu Waziri na suala la msingi lilivyokuwa linaelezea kwamba kuna madaktari wengi inaonesha wanaopangiwa kufanya kazi Pemba, aidha wenye asili ya kisiwa cha Pemba au wenye asili ya kisiwa cha Unguja, wanakuwa wagumu kwenda kufanya kazi kwa upande wa vituo vya afya vya Pemba.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, naomba kushauri halafu nitauliza swali vile vile.

Mhe.Mwenyekiti, wizara haioni kwamba kwa kuwa kuna tatizo la wafanyakazi au madaktari kwenda kufanya kazi Pemba. Hawaoni serikali ipo haja ya kutengeneza mazingira maalum (*incentives*) ili kuwavutia wafanyakazi ambao wenye asili ya kisiwa Pemba kufanya kazi Pemba, lakini vilevile na wale wenye asili ya Unguja kuweza kuhamasika na kwenda kufanya kazi kule Pemba.

La pili au swali la (b). Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa kuna malalamiko mengi sana ya vijana wetu kukosa ajira hasa hawa ambao waliokuwepo katika Chuo cha Afya Mbweni. Sasa, je, hatuoni Mhe. Mwenyekiti, kwamba hawa ambao wameshindwa kuripoti katika vituo vyao, sasa hivi ipo haja ya serikali kuangalia mazingira ya kuweza ku-*cover* hili eneo kwa wale ambao mpaka sasa hivi bado hawajapata ajira.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya:

a) Mhe. Mwenyekiti, wafanyakazi wanaopangiwa Pemba ni wafanyakazi wa Zanzibar na wanapewa *incentives* zile wanazozisema kwa mujibu wa wanapofika kule. La kwanza mfanyakazi yule anayekwenda anahakikishiwa anapewa nyumba ya kukaa, kabla hajaondoka anapewa mshahara wake hata hajaanza kazi, anapewa nauli, anapewa pesa ambazo za kujikimu anapofika pale.

Akifika Pemba kwa vile kuna upungufu mkubwa wa wafanyakazi, wale wanashiriki karibu kila semina inayofanyika kule. Lakini si hivyo tu wale wote wanaorudi Pemba huwa tunawafikiria wa mwanzo kwenda kusoma na kati ya hao 74 waliorudi kutoka Pemba, wote wapo vyuoni hivi sasa.

Kwa hivyo, tunajitahidi kama serikali, kukiwa na *on call* wanapewa, kukiwa na *over time* wanapewa, kukiwa na mafunzo wanapewa. Kwa vile wapo wachache kwa asilimia 100 wote wanapata *incentives* zile. Kwa hivyo, tunachokitoa kwa kile ambacho ni kwa kadri ya uwezo wa serikali uliopo na mshahara wao upo kama vile kulingana na kada yao ambayo wamekwenda kwa sababu mishahara itatofautiana na kipi wamesomea.

Kwa hivyo, mimi ninafikiri tunajitahidi kwa kadri ya uwezo unavyoweza kufanya serikali na katika waliorudi Pemba, hakuna

hata mmoja aliyelalamika kwamba alikosa fursa hii. Hivyo, mimi ninafikiri tunajitahidi kufanya hivyo.

b) Wale walioajiriwa, lakini wakashindwa kwenda kuripoti. Tatizo lililokuwa limejitokeza kwamba wakati tunapanga bajeti, tunajua kwamba tuna wafanyakazi ambao watatakiwa kwenda Pemba tukija tukiwaajiri. Lakini kila tulivyopanga bajeti haikukubali kutuachia nafasi ya kusema kwamba hizi fedha tuziweke ili watu waje waende Pemba wakati tulikuwa tuna mahitaji mengine ya lazima tutafanya.

Kinachosubiriwa hivi sasa ikipatikana *OC* ambayo tumeambiwa tutaipata labda leo au kesho ili wafanyakazi hao wapewe mshahara wameshapewa, wapewe nauli yao ya kwenda, posho la kujikimu ili waweze kwenda Pemba na kunatakiwa kama shilingi milioni 17 ili kuwapeleka hao watu.

Kwa hivyo, tukizipata wakati wowote watasafiri kwenda zao Pemba.

HOJA BINAFSI

(Hoja ya Mjumbe ya Kuomba Ridhaa ya Baraza kwa ajili ya KusahihishaMswada wa Sheria ya Utawala wa Baraza)

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba uniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kuweza kuleta taarifa ya Hoja ili niwaombe Wajumbe wa Baraza lako tukufu waniunge mkono katika hoja hii ya kuleta Sheria ya Mswada wa Kuanzisha Sheria ya Utawala na Utumishi ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabla kuwasilisha hoja yangu hii, naomba uniruhusu kutoa maelezo kidogo ili kuweza kukazia hoja yangu hii. Mhe. Mwenyekiti, katika Baraza lako hili kumejengeka utamaduni wa kusubiri miswada yote iletwe na serikali, jambo ambalo linasababisha sheria nyingi kupitwa na wakati na pia kuwaacha wananchi wakilalamika kuwa baadhi ya sheria hazisaidii kuondoa unyanyasaji na dhuluma kwa wahusika mbali mbali. Kwa mfano kuna vitendo vingi vya unyanyasaji na ubakaji wa watoto wadogo ambao hakuna sheria maalum ya kupambana na vitendo hivi. Huo ni mfano mmoja tu, lakini ipo mifano mingi kama hii.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na udhaifu wetu huo tulionao hivi sasa, sisi Wajumbe wako tumeona tuvunje ukimya na tutekeleze wajibu wetu Kikatiba kwa kutunga miswada ya sheria na kuileta hapa Baraza na kuipitisha kuwa sheria.

Mhe. Mwenyekiti, ninaamini kila mtu ana fikra zake, wengine wanaweza kufikiria kuwa mimi kuleta hoja hii labda ninatafuta umaarufu au ninataka nionekane ninajua zaidi na wengine hasa wale wanaojua wajibu wetu sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wataamini kuwa sasa tumeanza kujitambua na huu ndio uwe mwanzo wa hoja nyingi kutiririka hapa Barazani

kwa miswada binafsi ya Wajumbe ili kutekeleza kifungu cha 78 (3) na kifungu cha 81 cha Kanuni zetu za Baraza la Wawakilishi kuhusu miswada ya Wajumbe. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, historia ya nia ya haja ya kuleta hoja hii hapa Barazani ipo kwa muda mrefu zaidi ya mwaka mmoja katika afisi yako, lakini busara zako za kutaka tufanye utafiti katika Mabunge mengine ya nchi za Jumuiya ya Madola, kazi hii ninakuhakikishia kwamba tumefanya utafiti wa kutosha wa sheria za Mabunge kama Katiba yetu ya Zanzibar kifungu cha 77 (4) inavyotaka Baraza lenyewe kutunga sheria yake ya utawala, basi sasa tupo tayari kuleta ishara hii ya Utawala wa Baraza na kuisoma kwa mara ya kwanza katika kikao kijacho cha Baraza. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, pia ninapenda kuwahakikishia Wajumbe wako wa Baraza hili kuwa maandalizi ya kuletwa mswada huu serikali inajua vizuri sana, kwani tulikwenda kumuona Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambaye naye kwa mujibu wa Katiba pia ni sehemu ya Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Na kwa hivyo, tunamshukuru sana alitupa baraka zote, tunamshukuru kwa hilo, lakini pia tumepata mashirikiano makubwa kutoka kwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Mhe. Balozi Seif Ali Iddi tangu maandalizi ya ripoti hii hadi kufikia hatua hii. Pia, Mhe. Mwanasheria Mkuu pamoja na Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, nao katika michango yao katika kufanikisha mswada nitakaouwasilisha katika kikao kijacho. Kwa hivyo, mswada huo Mhe. Mwenyekiti, utakuwa umepata baraka zote na hautokuwa mgumu wakati nitakapokuja kuwasilisha. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo sasa naomba uniruhusu kuwasilisha taarifa yangu hii ya hoja ya kuliomba Baraza lako tukufu kuipokea taarifa hii na kuniruhusu kuleta Mswada wa Sheria wa Utawala wa Baraza na kuusoma kwa mara ya kwanza katika kikao kijacho, hoja yenyewe ni hivi ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Wawakilishi la Zanzibar limeanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 63 cha Katiba ya Zanzibar ya 1984. Majukumu ya Baraza la Wawakilishi yametajwa katika kifungu cha 88 cha Katiba yetu ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, ili majukumu haya ya Baraza yaweze kutekelezwa vizuri na kwa ufanisi mkubwa kuna haja ya kulijengea uwezo Baraza katika nyanja zote, kuanzishwa kwa sheria ya Utawala wa Baraza la Wawakilishi na kuweka masharti juu ya utaratibu wa mfuko wa Baraza na mambo mengine yanayohusiana na hayo ni moja katika hatua muhimu itayowezesha Baraza letu la Wawakilishi kutekeleza kazi zake kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, pia, kutungwa kwa sheria hii ni katika kutekeleza matakwa ya Katiba ya Zanzibar ya 1984 chini ya Kifungu cha 77 (4) kinachotoa

mamlaka kwa Baraza la Wawakilishi kutunga sheria ya mfumo wa utawala na uendeshaji wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi.

Hivyo, sheria hii itatoa mamlaka kwa Baraza kuweka muundo wa Utumishi wa Afisi ya Baraza na uendeshaji wa Afisi hiyo bila ya kuingiliwa na taasisi nyengine yoyote ya nje ya Baraza na pia kujipangia shughuli zake kwa mujibu wa mahitaji ya Baraza ikiwemo uanzishwaji wa Afisi ya Faragha ya Spika ambayo kwa hivi sasa haimo, jambo ambalo linaifedhehesha Afisi ya Spika na Baraza kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, hali iliyopo hivi sasa ya uendeshaji wa Baraza hasa uombaji na uingizaji wa fedha kwa ajili ya matumizi ya kuendesha shughuli za Baraza, inategemea kufuata utaratibu ule ule unaotumika kwa idara ama taasisi yoyote ya serikali. Utaratibu huu umelalamikiwa sana na Waheshimiwa wako wa Baraza lako Tukufu kuwa unachelewesha upatikanaji wa fedha zinazoombwa na hivyo kupunguza ufanisi wa Baraza katika kutekeleza majukumu yake ili kuyasimamia utekelezaji wa shughuli za umma kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 5(a) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yenyewe inakuja hivi:-

Kwa kuwa nchi ya Zanzibar inafuata mfumo wa mgawanyo wa madaraka kwa mujibu wa Kifungu cha 5 (1) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 na kwa kuwa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar ni moja kati ya mamlaka ya tatu ya nchi ikiwemo Mahakama na Serikali.

Na kwa kuwa kwa mujibu wa mgawanyo wa madaraka kama ulivyowekwa katika Katiba, Baraza la Wawakilishi la Zanzibaar ndio lenye jukumu ya kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma kwa mujibu wa Kifungu cha 5 (a) (2) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984.

Na kwa kuwa Serikali inawajibika mbele ya Baraza la Wawakilishi katika utekelezaji wa shughuli zake kwa mujibu wa Kifungu cha 43 (5) cha Katiba ya Zanzibar na pia kuna umuhimu mkubwa wa kuwepo uhuru kwa Baraza la Wawakilishi katika kutekeleza majukumu yake kama inavyoainishwa katika Kifungu cha 5(a) cha Katiba ya Zanzibar.

Na kwa kuwa utaratibu wa sasa wa kuviweka vyombo vya Baraza la Wawakilishi ikiwemo Tume ya Utumishi ya Baraza la Wawakilishi chini ya mamlaka mengine ya muhimili mwengine wa serikali unadhoofisha dhana ya uhuru wa Baraza iliyoainishwa katika kifungu hicho cha 5 (a) cha Katiba ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, na kwa kuwa baadhi ya vifungu vya Katiba ya Zanzibar vikiwemo Kifungu cha 116 na Kifungu cha 76, vinapunguza uhuru huu wa Baraza la Wawakilishi kwa kuliweka Baraza chini ya taasisi nyengine katika muhimili wa serikali (*Executive*).

Na kwa kuwa Zanzibar kwa kupitia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni miongoni mwa nchi za wanachama za Jumuiya ya Madola ambazo zimekuwa zikianzisha sheria, utawala na mifuko maalum ya Mabunge hayo ili kutekeleza kazi zake kwa wepesi na ufanisi mkubwa zaidi.

Na kwa kuwa Mabunge kuwa huru zaidi katika mambo ya utawala na fedha, sio jambo jipya katika mfumo wa Mabunge ya nchi za Jumuiya za Madola.
Na kwa kuwa tangu mwaka 2005 Mabunge mbali mbali ya nchi za Jumuiya ya Madola kupitia Chama cha Wabunge cha jumuiya hiyo *(Commonwealth Parliamentary Association - CPA)* yamekuwa yakijadili namna bora ya kuleta ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya Mabunge hayo kwa kutilia mkazo zaidi suala la Mabunge hayo kuwa na uhuru zaidi katika masuala ya fedha *(Financial Autonomy)* na masuala mengine ya uendeshaji wa Mabunge hayo kwa kuzingatia hali halisi ya uchumi wa nchi husika.
Mhe. Mwenyekiti, hivyo basi kuna haja ya uanzishwaji wa Sheria ya Utawala wa Baraza la Wawakilishi na kuweka masharti juu ya utaratibu wa mfuko wa Baraza na mambo mengine yanayohusiana na hayo ili Baraza liweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo, sambamba na hilo, kuna haja ya kuwepo kwa sheria ya mabadiliko ya Katiba ili kufanya marekebisho katika Kifungu cha 116 kwa tafsiri yake, kinaweka Tume ya Utumishi ya Baraza chini ya chombo chengine cha muhimili wa serikali na pia Kifungu cha 76 cha Katiba ya Zanzibar ambacho nacho kinadhoofisha uhuru wa Baraza la Wawakilishi, yaani kinahusu uteuzi wa Katibu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia madhumuni na sababu ya mswada huu, unakusudia kutekeleza maamrisho ya Katiba ya Zanzibar hasa katika Kifungu cha 77 (2) kinachotoa mamlaka kwa Baraza la
Wawakilishi kutunga sheria kwa ajili ya kuweka mfumo wa utawala na uendeshaji na mambo mengine yanayohusiana na Afisi ya Baraza la Wawakilishi.
Kwa hivyo, madhumuni makubwa ya mswada itakuwa ni kuanzisha Sheria ya Utawala wa Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya utekelezaji bora wa shughuli zake za Baraza na kuweka Tume ya Utumishi ya Baraza itakayosimamia shughuli mbali mbali za Baraza na utumishi wa Baraza na taratibu zinazosimamia utumishi huo, maslahi ya Wajumbe, lakini vile vile pamoja na watumishi wa Baraza pamoja na mambo mengine.
Aidha, mswada huo unakusudia kuanzisha mfuko wa Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya uendeshaji bora wa shughuli zake za Baraza la Wawakilishi. Pia, mswada huu utakuwa umegawika katika sehemu tano yenye jumla ya vifungu 38.
Sehemu ya kwanza itakuwa ni utangulizi, ikijumuisha jina la mswada, muda wa kuanza kutumika na sheria na matumizi ya sheria na tafsiri na maneno mbali mbali yatakayotumika katika mswada huo.
Sehemu ya pili, inaanzisha utumishi wa Baraza unaojumuisha Katibu wa Baraza na watumishi wa Baraza katika Idara, Divisheni na Vitengo na kuweka utaratibu mbali mbali zitakazoongoza utumishi katika Baraza la Wawakilishi ikiwemo taratibu za uajiri, kuachishwa kazi watumishi wa Baraza, maadili na mambo mengine ya utumishi wa Baraza.

Aidha sehemu hii itafafanua kazi na uwezo wa Katibu wa Baraza la Wawakilishi.
Sehemu ya tatu ya mswada huu, itaanzisha Tume ya Utumishi wa Baraza, kuainisha muundo wa Tume hiyo, kazi za tume, utaratibu wa vikao vya tume, jinsi ya kufanya maamuzi wakati vikao vya tume na stahiki za Wajumbe na sekretarieti ya tume.
Pia, sehemu hii itaweka utaratibu wa Wajumbe wa tume kushika dhamana zao na namna ya Wajumbe hao wanavyoweza kusita kuwa Wajumbe katika tume hiyo.

Na sehemu ya nne, itaanzisha mfuko maalum wa Baraza ambao utatumika kuweka fedha zote zitakazoainishwa kwa ajili ya matumizi ya Baraza la Wawakilishi. Sehemu hii pia itaweka utaratibu na utayarishaji wa kumbukumbu za mapato na matumizi ya mfuko kwa ajili ya ukaguzi.
Sehemu ya tano, itafafanua mambo mbali mbali ikiwemo pamoja na kufafanua, kuweka mpango wa bima ya afya za Wajumbe na watumishi wa Baraza, utaratibu wa kinga za Wajumbe na watumishi wa Baraza wakati wa kutekeleza majukumu yao na uwezo wa tume kuita mashahidi.
Pia, sehemu itaweka mamlaka ya Waziri anayehusika na masuala yanayohusiana na Baraza la Wawakilishi kutunga Kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti yaliyoainishwa katika mswada huu. Pia, utaratibu wa kuwasilisha ripoti ya mwaka ya utekelezaji wa kazi zake za tume.
Mhe. Mwenyekiti, kabla sijamalizia nilikuwa naomba kutoa nasaha zifuatazo:
Mhe. Mwenyekiti, Katiba ya Zanzibar kama nilivyoeleza katika vifungu hivyo nilivyovitaja, vimeeleza majukumu ya Baraza la Wawakilishi miongoni mwao, moja katika jukumu la Baraza la Wawakilishi ni kutunga sheria ya utawala wa Baraza.
Lakini vile vile, Kanuni zetu kama nilivyoeleza Mhe. Mwenyekiti, zimeturuhusu kutunga miswada binafsi ya Wajumbe. Sasa historia ya miaka 50 ya Mapinduzi mpaka leo bado hakuna Mjumbe yeyote wa Baraza la Wawakilishi aliyeweza kuleta mswada binafsi ambao ukatungwa kuwa sheria. Kwa hivyo, hii tunakiuka Kanuni zetu wenyewe ambazo tumezitunga.
Sasa nilikuwa naomba Waheshimiwa muijadili ripoti yangu hii kama Kanuni zinavyotueleza ndani ya muda wa saa moja mutumie uhuru wenu ili kuweza kuridhia hoja yangu hii katika kikao kijacho niweze kuleta hii hoja ambayo baadae itakuwa ni sheria.(*Makofi*).
Kwa hivyo, mimi Hamza Hassan Juma, Mwakilishi wa Jimbo la Kwamtipura, naomba Baraza hili tukufu la Wawakilishi litoe idhini kwa mujibu wa Kanuni ya 81 za Baraza la Wawakilishi toleo la 2012 ili niwasilishe mswada wa Sheria ya Utawala wa Baraza la Wawakilishi na marekebisho ya Katiba ya Zanzibar ya 1984 katika vifungu viwili nilivyovitaja.
Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Waheshimiwa Wajumbe. Baada ya kwisha kuwasilishwa kwa hoja hii na Wajumbe mukawa mumeiunga mkono. Sasa hatua inayofuata ni kuwahoji basi Wajumbe wote kwa ujumla wetu, wale wanaokubaliana na hoja hii, wanyooshe mkono, wanaokataa,wanaokubali wameshinda.

Sasa nitoe nafasi kwa Wajumbe ambao tayari wameleta majina hapa ili wachangie madhumuni ya hii hoja yetu na mpaka sasa hivi nina majina matatu na muda wetu wa kuchangia, jina la nne pia limetokeza hapa na muda wetu wa kuchangia ni saa moja.

Naanza na Mhe. Ussi Jecha Simai.

Mhe. Ussi Jecha Simai: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya mwanzo ya kuchangia hoja ya Mhe. Hamza Hassan Juma, inayohusu mswada wa sheria wa kuanzisha Utawala wa Baraza pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uzima wa afya, lakini pia kwa kutujaalia sote hapa kuweza kufanya kazi zetu hizi za kuwatumikia wananchi wa Zanzibar kwa utulivu na amani.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze kwa kuunga mkono hoja iliopo mbele yetu ambayo imetolewa na Mhe. Mjumbe kama niliyemtaja hapo mwanzo. Mhe. Mwenyekiti, nina sababu nyingi tu za kuunga mkono hoja hii ya Mhe. Hamza Hassan Juma.

Ya kwanza, ni kutekeleza matakwa ya Katiba kama alivyozungumza kifungu cha 88 cha Katiba ya Zanzibar, kinatoa jukumu kwa Baraza la Wawakilishi kutunga sheria. Kwa hivyo, moja kwa moja uzoefu uliokuwepo kwa nchi yetu ya Zanzibar kwamba miswada mingi inaanza serikalini na baadae inaletwa Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya kupitishwa ama kutungwa hiyo sheria yenyewe.

Kwa hivyo, kwa sasa wakati umefika tunaona kuwa Baraza lako hili limekuwa na uwezo mkubwa baada ya kupata mafunzo mbali mbali yanayohusiana na masuala

ya utungaji wa sheria. Kwa hivyo, sababu ya kwanza ni hiyo kwamba Katiba inaturuhusu kufanya hivyo kwa Baraza la Wawakilishi kuweza kutunga hiyo sheria.

Lakini la pili, Mhe. Mwenyekiti, Kifungu cha 77 (4) pia kinatoa mamlaka kwa Baraza la Wawakilishi la kutunga sheria ya utawala wa Baraza...

UTARATIBU

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nimeona nisimame kwa Kanuni ya 42 (5) kukumbusha kiti tu kidogo, kwa sababu katika maelekezo uliyoyatoa hapo, umesema kwamba mjadala wake hautozidi saa moja.

Kwa kadri ya ufahamu wangu Mhe. Mwenyekiti, muda wa saa moja ni wa kujadili hoja ya jambo la dharura ambalo lipo katika Kanuni ya 42 na linaongozwa na Kanuni ya 42 (5).

Bahati nzuri hoja hii si hoja ya kujadili jambo la dharura. Imetolewa taarifa mapema na imefuata taratibu zote, imewasilishwa, nilikuwa ninahofia tu na ndio maana nimeona nimkatishe rafiki yangu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Chaani ili asije akajibana sana kuchangia kwa sababu ya muongozo wako wa awali kwamba muda ni mchache.

Ninadhani hoja hii namna ya kujadili ni maelekezo ya kiti chako, lakini tusije tukajikita kwamba ni saa moja ambayo muda uliowekwa kwa kujadili jambo la dharura kama vile ambavyo tuliwahi kufanya mara moja, mimi nilipowasilisha hoja ya namna hiyo jambo la dharura.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe ambaye ume-*raise* hoja yako ya Kanuni ya 42. Kimsingi tunakubaliana nayo, lakini kama mutakumbuka katika *briefing* na mkutano wetu ule wa Kamati ya Uongozi tulikubaliana katika hoja hii juu ya Mjumbe kwamba anakuja kuwasilisha nia yake ya kuweza kuleta maelekezo haya juu ya kikao chetu hiki tulichonacho.

Na jukumu la Wajumbe kwa siku ya leo, ilikuwa ni kuchangia katika madhumuni tu ya mswada huu na mswada kamili utakuja kujadiliwa pamoja na kuchangiwa pale utakapokuwa upo tayari, kwa leo ilikuwa ni kuthibitisha nia na baadae wajumbe wapate nafasi ndani ya saa moja kuchangia madhumuni ya kuletwa kwa nia hii na Mhe. Mjumbe na utakapokuwa mswada wake upo tayari basi utakuja kuchangiwa kwa mujibu wa taratibu za kanuni zetu zinavyotuongoza. Naomba niishie hapo.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, naomba turejee katika kanuni ya 81, 79 na 83. Kanuni hizi Mhe. Mwenyekiti, zinaelekeza utaratibu wa kupelekwa mswada binafsi. Hapa kilichofanyika ni kwamba mjumbe anatakiwa atowe hoja yake na baada ya kutoa hoja yake apate idhini kutoka katika Baraza lako tukufu kwamba hoja hiyo imekubaliwa kuwa alete mswada baadae katika kikao kinachofuata au asilete.

Kwa hivyo, mimi nafikiri kwamba mjumbe anataka idhini, kishakupata idhini ndio utaratibu wa kuandaa huo mswada unafuata, namna gani. Kwanza itabidi tufuate kanuni ya 79 inayoelezea utaratibu wa kupelekwa mswada huo katika ofisi ya gazeti kwa kutangaza na baada ya hapo kifungu au kanuni ya 83 inayoelezea mswada huo kuja kusomwa kwa mara ya mwanzo katika kikao kinachofuata.

Mhe. Mwenyekiti, naomba tufuate utaratibu huo kwamba hivi sasa sio suala la majadiliano, ni suala la kupata idhini ya Baraza kwamba je, tunamruhusu Mhe. Mwakilishi kuleta mswada wake. Tunakubali kumruhusu ili atayarishe mswada, lakini hatuwezi kujadili mswada kwa hivi sasa kwa sababu sio utaratibu wake. Baada ya kumruhusu nafikiri itakuwa suala hili limeshakamilika. Utaratibu utakuwa ni kuandaa mswada kuupeleka katika ofisi ya gazeti, ili katika kikao kinachofuata kwa kutumia kifungu cha 83 yeye atausoma kwa mara kwanza. Mhe. Mwenyekiti, naomba tufuate utaratibu huo.

Mhe. Mwenyekiti: Kama ambavyo Mhe. Waziri wa Sheria na Katiba ametufafanulia kwa mujibu wa kanuni zetu, ndio kama vile tulivyokuwa tumezungumza mwanzo kwamba lengo kuu ilikuwa kwa mjumbe kuwasilisha nia na nia hiyo imewasiliswa, ndio maana pale mwanzo tulitoa nafasi ya kwamba wajumbe watowe madhumuni tu, sio kitu chengine chochote, lakini baada ya maelekezo ya Mhe. Waziri wa Sheria na Katiba, nafikiria tuwahoji sasa wajumbe wanaokubaliana na hoja ambayo imewasilishwa na Mhe. Mjumbe Hamza Hassan Juma juu ya hoja yake hii binafsi katika Baraza la Wawakilishi, ili kuliomba Baraza la Wawakilishi la Zanzibar idhini ya kuwasilisha mswada chini ya kanuni ya 48(2), 49(1) na 81 za kanuni za Baraza la Wawakilishi wanaokubaliana na hoja hii

UTARATIBU

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, naomba ninukuu kanuni ya 81(1) inasema;

Kanuni ya 81(1)

> "Mjumbe yeyote baada ya kuomba na kupata idhini ya Baraza anaweza kuwasilisha kwenye Baraza mswada wa mjumbe ambao sio kwa maslahi yake binafsi"

Kanuni ya 81(2)

> "Maombi ya idhini ya Baraza kwa ajili ya kuwasilisha mswada wa mjumbe, yataletwa kwa njia ya hoja katika wakati unaostahiki kufuatana na orodha wa shughuli za Baraza na mjumbe atataja madhumuni na sababu za mswada huo"

Hayo tayari ameshayafanya Mhe. Mjumbe. Halafu inasema;

> "Taarifa ya hoja itaeleza pamoja na mambo mengine jina la mswada unaopendekezwa madhumuni na sababu za mswada, halafu taratibu zinafuatwa"

Kanuni ya 81(4)

> "Endapo idhini inatolewa baada ya hoja kutolewa na kupitishwa, mswada utatangazwa kwenye gazeti kama inavyotakiwa kwa miswada ya serikali kufuatana na masharti ya fasili ya kwanza, pili na tatu ya kanuni ya 79. Madhuni na sababu yatatiwa saini na huyo mjumbe anayehusika"

Kanuni ya 81(5)

> "Baada ya mswada kutangazwa katika gazeti, mjumbe anaweza kutoa taarifa kuwa nakusudia kuwalisha mswada huo kwenye Baraza, baadae utaratibu unaotumika kwa mujibu wa kanuni hizi, kuhusu hatua nyenginezo zitakazofuata za kushughulikia mswada huo zitafuatwa"

Nimeisoma yote Mhe. Mwenyekiti, ili tuelewane. Lakini si kwa kusimama ni 81(2), unaosema;

Kanuni ya 81(2)

> "Maombi ya idhini ya Baraza kwa ajili ya kuwasilisha mswada wa mjumbe, yataletwa kwa njia ya hoja....."

Halafu nikiunganisha Mhe. Mwenyekiti, kanuni ya 33 inahusu kujadili hati zilizowasilishwa.

kanuni ya 33(1)

> "Wakati wowote baada ya hati yoyote kuwasilishwa kwa mujibu wa kanuni 32, waziri au mjumbe aliyewasilisha hati hiyo au mjumbe mwengine yeyote, anaweza kuomba kutoa hoja kwamba Baraza lijadili hati hiyo"

Mjadala unaweza kuhusia kila jambo liwemo katika hati

(3) Waziri au mjumbe yeyote ambaye anaruhusika kulihutubia Baraza kwa mujibu wa kanuni hizi ikiwa hakuiwasilisha hati yake kabla, basi Spika atamzuwia waziri au mjumbe huyo asisome hati yake hiyo.

Sasa hii hati iliyowasilishwa mezani na mjumbe mwenyewe aliyeiwasilisha kaomba kwamba tuijadilia na baadae tuweze kuidhibitisha. Mimi nadhani Mhe. Naibu Spika, kama ulivyotoa maelekezo awali kwamba tunachojadili hapa ni ombi au hoja ya ombi la Mhe. Mjumbe, kwamba alete mswada. Hatuingii katika maudhui kwa sababu hayo maudhui yenyewe hatuna, lakini tunajadili hoja yake ya kuliomba idhini Baraza ili aweze kuleta mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, nilichokisimamia awali ilikuwa ni muda, kwamba muda wa saa moja uliokuwa umetengwa ambao uliutaja pale awali, ni muda ambao umewekwa kwa ajili ya kujadili hoja ya jambo la dharura na sio hoja ya kawaida kama hii ya mjumbe binafsi. Kwa sababu mimi ninavyoichukulia hii ni hoja kama hoja nyengine yoyote ya mjumbe binafsi, isipokuwa inaongozwa

na kanuni zake kuwa ni hoja ya kuomba idhini ya Baraza kuleta mswada, lakini bado ni hoja ya mjumbe binafsi.

Kanuni ya 81(2) imeweka wazi kwamba mjumbe ataleta ombi lake kwa kutumia hoja binafsi. Kwa hivyo, nilikuwa nadhani wajumbe tupewe fursa ya kujadili nia yake, ni haki yetu vile vile katika kuiongezea nguvu, sasa muda ni mamlaka ya kitu. Niliponyanyuka awali nilisema kwamba tusije tukajikita kwenye saa moja kwa kutumia hoja kwamba ndio kanuni. Kanuni imesema kwamba hiyo ni kwa jambo la dharura. Lakini kama kiti kimeelekeza vyengine, kama Kamati ya Uongozi ya Baraza iliagiza vyengine, sisi sio Wajumbe wa Kamati ya Uongozi ya
Baraza hatuwezikujua mliamua nini huko. Lakini nadhani suala la kujadili hoja hii ya mjumbe ya kuleta ombi la kuwasilisha mswada bado ni haki yetu waheshimiwa, ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiria sio suala la kubishana ni suala la kufuata kanuni. Kanuni ya 81(4) inasema kwamba;

Kanuni ya 81(4)

> "Endapo idhini itatolewa baada ya hoja kutolewa na anayetoa hoja ni Mhe. Hamza Hassan Juma, basi mswada utatangazwa kwenye gazeti kama inavyotakiwa"

Sasa hapa hakuna *issue* ya kujadili, kwa sababu tunajadili kitu gani, kwa sababu hoja aliyotoa ni ile ambayo yeye mwenyewe Mhe. Hamza Hassan Juma, anaitaka, sio hoja nyengine au sio hoja ya Mhe. Bi Mgeni Hassan Juma, ambayo itasomwa hapa. Yeye anaomba idhini ya hiki kitu kifanywe, huu ni mswada.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu, anajua katika sheria kifungu kilichoko nyuma kinatenguliwa na kifungu kilichoko mbele. Kwa hivyo, hiki kifungu cha 33 hakina mantiki kwa suala la mswada wa sheria, utaratibu unaofuata ni kifungu cha 81(4) ndio utaratibu wa uandikajiwa sheria. Kifungu cha mwanzo kinafutwa na kifungu cha mbele. Sasa kwa maana hiyo tukifuata kifungu cha 81(4) ni kwamba Mhe. Hamza Hassan Juma, ameshatoa hoja yake, anaomba wajumbe tutowe idhini.

Sisi wajumbe tunakubali idhini hiyo ili mswada huo anaoutaka uje katika kikao kinachofuata ndio suala. Kujadili tunajadili nini na huu ni mswada ambao hata sisi hatujui utakuja baadae, yeye anataka idhini basi tumpe idhini ili atuletee mswada tuje tujadili baadae au tusimpe idhini, sasa kama hatumpi idhini basi hatumpi.

Kama tunampa idhini ndio baadae atatangaza kwenye gazeti, halafu ndio ule utaratibu utakuwepo, baadae tutakuja kujadili katika kamati kama inavyokua. Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nimemsikiliza kwa makini Mhe. Waziri wa Sheria na Katiba alivyokua akieleza bahati mbaya sikupata fursa ya kumsikia Mhe. Ismail Jussa Ladhu. Lakini yale maeneo aliyozungumza Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, naamini wajumbe wote yamewaingia akilini na naamini wamefahamu kwamba tutapata *forum* ya kuja kujadili ule wakati utakapofika wa kujadili. Sasa hivi hatujui kitambaa chenyewe, hatujui mshono wenyewe. Yatakapoletwa yote hayo sasa ndio tutakuja kusema aah! mshono sawa sawa, lakini kitambaa sicho.

Kwa hivyo, mimi nadhani ni wakati mzuri wa kusema tu, kwamba labda kama haturidhiki na maelezo aliyotoa Mhe. Hamza Hassan Juma ya kuomba idhini, tuseme hatukupi kwa sababu hii. Lakini sidhani kama tuna mjadala wa kusema kuwa tunakupa kwa sababu hii. Mhe. Mwenyekiti, ninavyoona mimi ni hivyo.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nimesimama kuomba muongozo wako na kwa sababu Mhe. Mjumbe amewasilisha hoja na ameeleza madhumuni yake ya kuleta hoja. Kwa maana hiyo mimi kwa maoni yangu ni kwamba tuna haja ya kujadili japo kwa muda mfupi, ili tuweze kumpa hiyo idhini, kwa sababu hatuwezi tu kukubali moja kwa moja tumpe idhini bila ya kujadili na kutoa maoni yetu.

Jengine ni kwamba nakumbuka hoja hii iliwasilishwa kwenye Kamati ya Uongozi, mimi nikiwa mjumbe, Mhe. Abubakar Khamis Bakary, akiwa mjumbe, Mhe. Mwanasheria Mkuu alikuwa mualikwa na hili tumelizungumza kama ulivyolizungumza wewe ukiwa na wewe ni mjumbe, kwamba tumekubaliana kuwa tujadili kwa muda wa saa moja, huku nikiamini kuwa wanasheria hawa wangeweza kutusaidia katika kikao kile na ndio madhumuni makubwa ya kuwemo katika Kamati ya Uongozi.

Kwa hivyo, mimi nimeshaanza kuwa na mashaka juu ya jambo hili na kwa sababu bado linakwenda mbele, tumeshaanza sasa kupindishana, jambo ambalo naona haliwezi kusaidia chombo hiki. Mimi nadhani unataka muongozo kuwa ni aina gani ya hoja kwa mujibu wa kanuni itahitaji kujadiliwa na aina gani ya hoja kwa mujibu wa kanuni haihitaji kujadiliwa. Nadhani kwenye kanuni yetu imetuelekeza wazi kwamba yapo mambo yanahitaji kujadiliwa, na yapo mambo hayahitaji kujadiliwa yatatolewa tu

kama kauli. Kwa hivyo, nilikuwa naomba muongozo wako ili ukisaidie chombo hiki twende vizuri. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, mimi nakubali kuwa tulikuwepo kwenye Kamati ya Uongozi na tulikubaliana haya tuliyozungumza, tukasema kwamba Mhe. Mjumbe alete ombi lake la kutaka idhini kwa mujibu wa kanuni. Lakini hiyo idhini iwe katika mfumo wa hoja, ndio hivi alivyofanya. Suala la kujadili bado. Kule tulizungumza mengi tu, ambapo kipindi chake bado, kwa sababu huu mswada una sehemu tatu. Kusomwa kwa mara ya mwanzo, kusomwa kwa mara ya pili na kusomwa kwa mara ya tatu.

Mhe. Mwenyekiti, kusomwa kwa mara ya mwanzo ni suala unaloliweka tu katika meza, kusomwa kwa mara ya pili mswada ndio unapojadiliwa na pale tulizungumza mengi kama utakumbuka. Namna gani mswada utasomwa na namna gani kama wanataka watu wengine kuuchukua mswada huo au kama mjumbe hataki pia anaweza kusema, sio leo wala sio kesho ni katika kusomwa kwa mara ya pili. Sasa hapa kinachofanywa ni Mhe. Mwakilishi kuomba idhini ya kuleta huo mswada wake, idhini sasa ni kuamuliwa na Baraza kwa mujibu wa kanuni ya 81(4), kama tunakubali kwamba mswada wake uletwe katika Baraza usomwe kwa mara ya mwanzo katika kikao kinachokuja au hatukubali.

Tunapojadili tunaweza kumwambia huu mswada ubadilishe, ukijadili hiyo sababu na madhumuni aliyotoa na wengine wanaweza kusema mswada ubadilishe, lakini sio lengo lake hilo, yeye ameshatayarisha mswada wake, anaomba idhini ya mswada huu alivyouandika pale na madhumuni yake yale, je tumruhusu aulete kwenye Baraza au asilete ndio suala.

Sasa Mhe. Salimn Awadh Salmin anachosema sikifahamu, kwa sababu hatujenda kinyume na mazungumzo ya Kamati ya Uongozi tuliyozungumza. Nafikiri hakuyafahamu au alikuwa wakati huo pengine akifikiri mengine. Nakushukuru.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsanteni sana Waheshimiwa Wajumbe mbali mbali ambao mmechangia katika hoja hii. Mimi nitasimama katika maelekezo yale ambayo tulikuwa tumekubaliana katika Kamati ya Uongozi na maelezo ambayo yalikuwa yametoka chini ya uongozi wa Spika, ambapo kwa kanuni zetu chini ya kifungu 158 kimempa yeye mamlaka ya kutoa maamuzi pale ambapo tunahisi tuna haki ya kufanya hivyo.

Waheshimiwa Wajumbe, katika maamuzi yetu ya Kamati ya Uongozi, tuchokubaliana kwenye kikao kile, mjadala huu baada ya kwisha

kuwasilishwa kwa ajili ya Mhe. Mjumbe kuja kutoa hoja yake ya nia ya kwamba anataka kufanya jambo hili ndani ya Baraza. Wajumbe watapata nafasi ya kuchangia madhumuni, mchango wao kama nilivyozungumza mwanzo unagusa katika madhumuni kitu ambacho tayari kimekwisha kuelekezwa ndani ya mswada huu ambao umewasilishwa kwetu. Muda ambao tulikuwa tumekubaliana katika Kamati ya Uongozi ni saa moja la kujadiliana suala hili.

Naomba tuendelee kukubalianana yale maamuzi ambayo tuliamua katika Kamati ya Uongozi ili suala hili tulimalize kwa salama na amani na baadae tuje kuliripoti kwa Mhe. Spika, kama taratibu zinavyotuelekeza. Naomba kuishia hapa.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum: Mhe. Mwenyekiti, napenda sana kukiheshimu kiti cha Baraza la Wawakilishi. Tatizo
langu ni kwamba inaonekana Mhe. Mwenyekiti, ulishalihoji Baraza na nadhani lilikubaliana na hoja ya mjumbe. Sasa tutakapojadili unaweza kulihoji kwa mara ya pili.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa kanuni ya 154, Spika au kiti kinaweza kikatoa muongozo na maamuzi tukiwa ndani ya Baraza, sio kwenye Kamati ya Uongozi. Kwa hivyo, kiti kinafanya maamuzi ndani ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Ussi Jecha Simai: Mhe. Mwenyekiti, mimi sitaki kurudi huko, lakini nataka kupata tafsiri tu kutoka kwa Mhe. Mwanasheria Mkuu. Kanuni ya 33 inasema hivi;

Kanuni ya 33

"Wakati wowote baada ya hati yoyote....."

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa naomba tafsiri ya hii hati, kwa sababu mimi kwa akili yangu ya kitoto, niliona kwamba miongoni mwa hati ni ile moja ambayo imewasilishwa na Mhe. Mjumbe.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, tukija katika kifungu cha 81 hiki kimetaja moja kwa moja kuhusiana na mswada, huku kuna hati na huku kuna mswada. Kwa hivyo, leo hapa Mhe. Hamza Hassan hajaleta mswada ameleta hati. Kwa hivyo, nataka ufafanuzi kwenye vifungu hivi.

Kifungu kimoja cha 33(1) na chengine hiki cha 81. Sasa hapo nipate ufafanuzi Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe uliyemaliza nimekusikia na Mhe. Waziri ambaye ulitoa maelekezo pia nimekusikia. Lakini ninachokiomba kwa Waheshimiwa Wajumbe, naomba mkisaidie kiti na ninaomba wale wajumbe ambao nilielekeza kuwa wachangie, basi waendelee kuchangia na baadae tutaendelea na utaratibu mwengine kama zilivyo taratibu zetu. Mhe. Ussi Jecha Simai.

Mhe. Ussi Jecha Simai: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kuonesha msimamo wako. Tunakuamini umepevuka sasa.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea mbele katika kuunga mkono hoja, nilikuwa nazungumzia kifungu cha 77(4) ambacho kinatoa mamlaka kwa Baraza la Wawakilishi la Kutunga Sheria. Kwa hivyo, hapa bado naona Mhe. Mjumbe alitumia ule wajibu wake kama Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Vile vile, kifungu cha 5A(2) kinaonesha ule mgawanyo wa madaraka ambapo Baraza la Wawakilishi ni chombo ambacho kinahusika na utungaji wa sheria.

Mhe. Mwenyekiti, kwa haraka haraka ili na wenzangu wapate muda wa kuchangia na wao. Historia inaonesha kwa muda mrefu sasa, yaani mimi sijawahi kusikia kwamba kuna mjumbe siku moja alileta mswada binafsi hapa. Lakini kwa sababu ya kupevuka kwa sisi wajumbe wetu kutokana na mafunzo mnayotupa, basi tumeelimika na hivi sasa tunaanza, huu ni mwanzo. Sasa hivi wajumbe tuna nia ya kuziangalia sheria nyingi zenye mapungufu, basi tutakuwa tunaleta miswada mingi tu katika Baraza Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, hili linatokana na kwamba serikali kwa muda mrefu inakuwa na mambo mengi na majukumu mengi, kwa hivyo kuna baadhi ya sheria zina mapungufu au nyengine hazijatungwa bado, lakini kutungwa kwake kunachelewa kutokana na majukumu ambayo wanayo.

Mhe. Mwenyekiti, sababu nyengine ya kuunga mkono hoja hii ni kuhusu ziara zilizofanywa na wajumbe wako katika Mabunge mbali mbali ya *Commonwealth* yameona kwamba kuna miswada mingi ambayo inatungwa na wajumbe. Zaidi kwa mswada kama huu unaohusiana na utawala wa Baraza ama Mabunge, basi mara nyingi unatokana na wale wajumbe wenyewe. Kwa kusema hivyo ni kuonesha wazi kuwa Baraza la Wawakilishi ndilo lenye jukumu la kutunga sheria, lakini mara nyingi miswada inatoka serikalini.

Kwa hivyo, kwa hili ambalo linahusu moja kwa moja Baraza la Wawakilishi, ni vyema mswada huu ukaletwa na Mhe. Hamza Hassan Juma, lakini pia mswada huu ukabaki huko huko na serikali ikatusubiri kwa hili watuachie sisi

wenyewe tumalize mswada. Kwa mujibu wa kikao chetu cha juzi kwamba taratibu nyingi zimekamilika kilichobakia sasa katika mswada huu ni kupata ile tafsiri ya lugha ya Kiingereza.

Mhe. Mwenyekiti, hili lisiwatie watu mashaka, kwa sababu watu wanaona mbona sasa hivi tena Baraza linataka kukiuka utaratibu. Kama zilivyozungumza zile sheria pamoja na kanuni ambazo zinaturuhusu kufanya hivi.

Mhe. Mwenyekiti, Waheshimiwa Wajumbe sasa hivi wana uwezo mkubwa wa kuweza kujaribu angalau kuleta hii miswada. Lakini watu watakuwa na wasi wasi, kwa nini sasa hvi Baraza linaanza kuandika miswada yake. Jambo hili kama lilivyozungumziwa ni kwamba sheria zinaturuhusu kufanya hivyo na kwa kuwa mswada huu unalihusu Baraza lenyewe Basi ni vyema basi tukajaribu kwa huu mswada ambao unahusu Baraza letu la Wawakilishi tukauleta hapa ili kuweza kuonesha ule uwezo ambao tunao na tukiona kuwa tunaweza kweli basi miswada mingine mingi tutajaribu kuitunga sisi wenyewe, ili tusaidie baadhi ya kazi ambazo serikali inaonekana kuwa zinachelewa na zinachukua muda mrefu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia kabisa mimi naunga mkono hoja hii na mswada huu nasisitiza kuwa ubaki kwa Mhe. Mjumbe binafsi, ili tuweze kuushughulikia na hatimaye tuulete hapa ujadiliwe na baadae uwe sheria ili tulisaidie Baraza letu la Wawakilishi. Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwakilisha.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa hai na wazima, tukijadili hoja binafsi ya mjumbe aliyeileta ambayo kwa mujibu wa waraka wake amesema kwamba ametumia kanuni ya 48(2), 49(1) na 81.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, kwa kutumia kanuni hizo bado naamini inatupa haki ya kujadili suala hili. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, kanuni ya 48 maelezo yake ya pembeni yanasema, mijadala kuanzishwa kwa hoja. Kwa hivyo, msingi wake ni kwamba hoja zilizoletwa zinapelekea kuwepo mijadala kama ilivyoelezwa pale.

Suala la pili Mhe. Mwenyekiti, nikiombe kiti tu kwamba mara nyengine kauli zetu zimetoa mamlaka kwa kiti kuamua hoja za wajumbe. Sasa inapotolewa hoja kuhusu utaratibu ukaruhusu mjadala kidogo baina ya wajumbe tofauti, tunakuwa pia tunazikiuka kanuni zetu. Hiki chombo ni kikubwa tumekuwa tunasema mara nyingi Mhe. Mwenyekiti, nadhani mjumbe anapozungumza kuhusu utaratibu basi nijukumu la kiti kutoa maelekezo. Lakini kiti kikialika

mjadala kuhusu utaratibu basi tunakuwa tunazikiuka kanuni zetu vile vile. Kwa hivyo, nafikiri Mhe. Mwenyekiti, tujitahidi katika hili.

Nikiondoka hapo Mhe. Mwenyekiti, nije katika msingi wa hoja. Nasisitiza Mhe Mwenyekiti, kwamba hapa hatujadili mswada, tunajadili hoja ya mjumbe ya kuomba idhini ya Baraza kuleta mswada binafsi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi binafsi naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja, ili kumruhusu mjumbe kuleta mswada binafsi kwa sababu ambazo amezieleza vyema katika hoja yake hii binafsi.

Mhe. Mwenyekiti, sote tumeshuhudia kwamba kwa muda mrefu kidogo kumekuwa kukijitokeza malumbano mbali mbali, baina ya wajumbe wa Baraza na serikali, kuhusu ni yepi hasa mamlaka na nafasi ya chombo hiki katika nchi yetu. Mhe. Mjumbe kataja kwamba katika katiba yetu ya Zanzibar, kifungu cha 5A(1) kinasema;

Kifungu cha 5A(1)

> "Zanzibar itafuata mfumo wa mgawanyo wa madaraka kati ya mamlaka tatu. Mamlaka ya utendaji, mamlaka ya kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma na mamlaka ya kutekeleza utoaji haki"

Kifungu cha 5A(2)

> "Mamlaka ya Utendaji ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar,Mamlaka ya Kutunga Sheria na Kusimamia Utekelezaji wa Shughuli za Umma ni Baraza la Wawakilishi na Mamlaka ya Kutekekeza Utoaji Haki ni Mahakama". na

Kifungu cha 5A(3) ambacho ndio msingi hasa kinasema;

> "Hakuna mamlaka itakayoingilia mamlaka nyengine, isipokuwa kama na kwa kadiri ilivyoelezwa katika Katiba hii"

Mhe. Mwenyekiti, mara nyingi kumekuja mgongano wa mawazo na tafsiri baada ya marekebisho ya kumi ya Katiba ya Zanzibar hasa kuhusiana na kifungu cha 116 ambacho kilianzisha Kamisheni ya Utumishi ya Umma. Kifungu kile kilionekana kama vile kimeziweka zile tume za Utumishi zote nyengine chini yake, lakini mara nyengine tumegongana mawazo (tafsiri) humu ndani kwa sababu ukitizama lugha iliyotumika katika kuelezea Tume hizi. Kwa mfano kifungu cha 117 cha Katiba kinachozungumzia Tume ya Utumishi Serikalini.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mheshimiwa naomba nitoe taarifa, hatujadili Mswada sasa hivi, Mswada hatuujui. Tume za Utumishi zilizomo

humu na Tume za Utumishi zilizomo katika sheria hii aliyoileta Mhe. Hamza Hassan Juma, hatuzijui. Ndio maana tukasema hatujadili hivi sasa.

Naomba Mhe. Mwenyekiti, tujue hivi sasa hatujadili. Tume ya Utumishi imo kwenye Katiba, Tume ya Utumishi anayotaka kuianzisha Mhe. Hamza Hassan Juma, hizi hazimo na hivi sasa hatujadili Mswada. Nakuomba Mhe. Mwenyekiti, twende katika utaratibu.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaomba Waheshimiwa Wajumbe tujadili hoja tuliyokuwa tumewasilishiwa hapa kwa mujibu wa madhumuni ambayo yameelekezwa. Tunaendelea.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, natetea haki yangu najadili hoja. Hoja hii Mheshimiwa tunayo, naomba nitaje maeneo machache ambayo nayajadili. Hoja yenyewe kwa kuwa ukurasa wa mwanzo imeanza na kifungu cha 5(1) (a) cha Katiba ya Zanzibar, ndicho nilichokisoma hapa Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, lakini katika vifungu mbali mbali vya hoja hii kafanya rejea ya vifungu mbali mbali vya Katiba ili kujenga hoja ya idhini ambayo anaiyoiomba, ndivyo ninavyovijadili hapa. Sijadili Mswada maana Mswada hata mimi sina. Leo namuona kidogo kaka yangu Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria labda hakuamka vizuri, lakini nadhani ninachokijadili kimo ndani ya hoja ya Mjumbe. Labda Kiti chako kingeniongoza yepi katika alama zilizomo katika hoja hii ya Mjumbe tujadili na yepi tusijadili, lakini humu ndani kataja.

Naomba Mheshimiwa niseme msingi wa hoja hasa, maana yake ile kwa kuwa ni hoja zake lakini mwisho kabisa anasema nini Mheshimiwa Mjumbe.

> "Kwa hivyo, mimi Hamza Hassan Juma, Mwakilishi wa Jimbo la Kwamtipura, naomba Baraza hili la Wawakilishi litoe idhini kwa mujibu wa Kanuni ya 81 Kanuni ya Baraza la Wawakilishi toleo la mwaka 2012, ili niwasilishe Mswada wa Sheria ya Utawala wa Baraza la Wawakilishi na Mswada wa Marekebisho ya Katiba ya Zanzibar katika vifungu vilivyotajwa katika hoja hii"

Ukienda hapo juu kataja kifungu cha 116 ambacho ndicho tunachokitumia kujengea hoja yake, kwamba kifungu hicho kinaleta mtatizo wa tafsiri. Mimi ninachozungumza mimi hapa Mhe. Mwenyekiti. Kwa hivyo, ndio maana nikasema mara nyingi kwamba tukianza kuzungumza halafu ikawa wewe Kiti unatualika tunajadili taratibu huku nyuma unakuwa unatupa kazi Mhe. Mwenyekiti, ni jukumu lako kuzitambua Kanuni na ututolee maamuzi wewe. Ukituachia sisi wenyewe tuamuliane juu ya taratibu zetu utakuwa unaliyumbisha sana Baraza Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: *Inshallah* nimekusikia.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, naomba Baraza lako linipe tafsiri ya neno idhini. Hapa Mhe. Hamza Hassan Juma, anaomba idhini. Idhini ni kumruhusu mtu. *Subject matter* hapa ni idhini sio hoja. Naomba idhini ya kusoma hitma, yaani wewe unipe idhini ili nisome, ndio *subject*

matter sio suala la hoja kujadili. Hii hatuijadili tunaomba idhini, sasa idhini tunampa huyu au hatumpi ndio *issue*.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe sote humu ndani ni watu wazima, na ni watu ambao kila mmoja ana jukumu ambalo amekabidhiwa na wananchi au umekabidhiwa na Rais. Lengo na madhumuni ni kufanya kazi ya kuwatumikia wananchi wetu. Kwa msingi huo ningeliwaomba sana wale ambao watakaokuwa wanapata fursa ya kuchangia wachangie kwa mujibu wa *paper* ambayo imewasilishwa na Mhe. Mjumbe. Hapa penye madhumuni ndio pahala pa kutembea.

Najua kwamba Mhe. Ismail Jussa Ladhu, amesema yeye hana Mswada kwa hiyo haoni sababu kwa nini anaambiwa anazungumzia kuhusu Mswada ambao hana na hajapewa. Lakini kuna vipengele ambavyo Mhe. Waziri wa Sheria na Katiba anahisi kwamba anaingia katika maeneo ya ndani ya kuchambua Mswada wenyewe. Sasa kwa ruhusa ambayo ilikuwa nimeitoa mimi naomba Wajumbe tukubaliane kujadili madhumuni na sababu ya kuletwa kwa Mswada huu. Hapo ndipo ambapo tunapaswa kupazungumza. Nakuombeni sana Wajumbe. Ahsante.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, leo labda tuna ile hadithi aliyoisema Mwanasheria Mkuu kuwa Baraza limekanyaga chechele. *(Vicheko)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba ili niridhishe Kiti, mimi sitaki nimridhishe Mjumbe mwengine yeyote humu ndani nataka nikiridhishe Kiti na naomba tena Kiti kisiyumbe Mhe. Mwenyekiti. Naomba nisome ukurasa wa pili hivi ndio ya mwisho kabisa. Ili niridhishe kwamba najadili hoja, narejea tena sijadili mswada ambao mimi siujui, na nashangaa hata Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria anasema kwamba najadili mswada, labda yeye kauona. Maana ukinambia najadili Mswada kwamba Mswada anaujua maudhui yake ni nini. Sasa mimi sina Mswada. Kwa hivyo, ukinambia najadili Mswada, Mswada upi na miye sina. Sasa kama yeye kauona miye sijui Mhe. Mwenyekiti.

Narejea tena ukurasa wa pili chini kabisa. Hoja ya Mheshimiwa Mjumbe ndio tunayoijadili hapa. Naomba nisikilize tena hii ninayosoma ni hoja ambayo ndiyo tunayoijadili hapa, hoja ya kutaka idhini ndiyo iliyoletwa hapa na Kanuni ya 48 inasema wazi kwamba mjadala unaanzishwa kwa hoja. Mhe. Mjumbe kaleta hoja ndiyo tuijadili humu.

Mhe. Mwenyekiti, narejea tena Kiti kisiyumbe. Ukurasa wa pili chini inasema:

> "Hivyo basi kuna haja ya kuanzishwa sheria ya utawala wa Baraza la Wawakilishi na kuweka masharti juu ya utaratibu wa mfuko wa Baraza na Mambo mengine yanayohusiana na hayo, ili Baraza liweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Sambamba na hilo, pia kuna haja ya kuwepo mabadiliko ya Katiba ili kufanya marekebisho katika kifungu cha 116 ambacho kwa tafsiri yake kinaiweka Tume ya Utumishi wa Baraza chini ya chombo chengine cha mihimili ya

serikali, na pia kifungu cha 76 cha Katiba ambacho nacho kinadhoofisha uhuru wa Baraza la Wawakilishi"

Sasa naomba unielekeze maana yake vyenginevyo naona nitakuwa siwezi kuchangia, maana kila nikisema sentensi moja nakatizwa. Uniongoze, unaturuhusu tujadili hili ama tuliache tuwaachie wengine waendelee. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na nakuomba uendelee kufuata mfano huo

Mhe. Mwenyekiti, narejea tena kwamba kifungu cha 116 cha Katiba ambacho kiliingizwa na marekebisho ya 10 ya Katiba ya Zanzibar, kilileta dhana hii ya Kamisheni ya Utumishi wa Umma ambayo imeonekana kama vile kwamba imetoa madaraka ya kusimamia Tume nyengine za Utumishi. Lakini nasema Katiba hii, kifungu cha 117 kwenye Tume ya Utumishi ya Serikali lugha yake haina maelezo inasema tu kazi zake zitakuwa kwa mujibu wa sheria itakayotungwa na Baraza la Wawakilishi.

Hivyo hivyo katika kifungu cha 102 kinachozungumzia Tume ya Utumishi ya Mahakama inazungumza hivyo hivyo, na vile vile katika kifungu kinachozungumzia Tume ya Utumishi Idara Maalum. Lakini kifungu cha 77 ambacho Mhe. Mjumbe katika hoja yake kakitaja kinachozungumzia Ofisi ya Baraza la Wawakilishi kipo tofauti. Kifungu cha 77 kimetoa maelezo ya kina tofauti na vifungu vyengine vyote juu ya Ofisi ya Baraza la Wawakilishi na utaratibu wake na pia kinaelezea haja ya kuundwa hiyo sheria ambayo Mhe. Mjumbe ameomba idhini ya Baraza ili kuleta Mswada binafsi kwa ajili yake.

Mhe. Mwenyekiti, nilichokuwa nikitaka kusema ni kwamba ombi la Mhe. Mjumbe ni sahihi. Na kama nilivyotangulia kusema awali kwamba mimi naliunga mkono binafsi kama Mjumbe. Naamini naliunga mkono kwa niaba ya wananchi ambao naamini wanataka chombo hiki kiweze kupata mamlaka yake ya kutekeleza shughuli zake ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijakaa katiba yoyote huwa inaelezea nini malengo ya wale waliotunga Katiba ile. Na katika Katiba yetu yapo maelezo ya utangulizi, na katika maelezo yaliyomo katika utangulizi wa katiba, karibu na mwisho kule kunasema.

"Na kwa kuwa misingi hiyo inaweza kutekelezwa katika jamii yenye demokrasia ambayo serikali yake husimamiwa na Baraza la Wawakilishi lenye Wajumbe waliochaguliwa na linalowawakilishawananchi.Pia,yenye Mahakama huru na utekelezaji wa kutoa haki bila ya woga wala upendeleo wowote, na hivyo kuhakikisha kwamba haki zote za binaadamu zinadumishwa na kulindwa na wajibu wa kila mtu unatekelezwa kwa ukamilifu"

Katika hoja zilizojengwa moja ni kuwa na Baraza la Wawakilishi ambalo Wajumbe wake wanachaguliwa la linawakilisha wananchi. Sasa chombo hiki ili kiweze kufanya kazi yake kikamilifu kinahitaji kupewa mamlaka yake inavyopaswa, kinahitaji kupewa uhuru wake kwa ukamilifu, kinahitaji kuwa na uwezo wa kuamua kuendesha shughuli zake kwa mujibu wa bajeti ambayo

kinaisimamia wenyewe kama muhimili mmoja miongoni mwa mihilimi mitatu ya serikali.

Kwa hivyo, nadhani ni sahihi kwa Mjumbe kufikiria kuleta Mswada binafsi ambao utatoa fursa kutekeleza mamlaka hayo ambayo yametajwa ndani ya Katiba, katika utangulizi na katika Katiba yenyewe. Naamini Mhe. Mwenyekiti tukifanya hivyo tutasaidia sana nchi yetu ili kuwa na chombo ambacho ni huru, kinajitegemea, kinafanya maamuzi, hakipangiwi maamuzi yake na mtu mwengine. Kwa hivyo, niwaombe Wajumbe wenzangu kwamba tuunge mkono hoja ya Mhe. Mjumbe huyu na tutoe idhini ili tumruhusu kuleta Mswada.

Nimalizie Mhe. Mwenyekiti, kwamba tunasikia sikia ingawa haijatoka rasmi, kwamba kuna pendekezo kwamba serikali iuchukue Mswada huu. Mimi namuomba sana mtoa hoja, kafanya kazi kubwa sana na kajenga heshima ya chombo hichi kama alivyosema mwenyewe kwamba sasa tunaanza kutengeneza Kanuni pale ambapo tunaruhusiwa kuleta Mswada binafsi tuweze kufanya hivyo.

Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Mjumbe kwamba abakishe Mswada huu kwake ili uwakilishe ile dhamira njema katika kipindi hiki wakati nchi yetu inatimiza miaka 50 ya Mapinduzi, kwamba chombo hiki kinatekeleza majukumu yake ikiwemo ya kuwapa nafasi Wajumbe kuleta Mswada.

Nadhani kwa uzito wa Mswada anaopendekeza kuuleta ni muhimu sana ukaletwa na Wajumbe ambao si sehemu ya serikali ili kulinda ile haki yetu ya kulinda muhimili huu na mamlaka yake kwa ukamilifu. Kwa hivyo, niwaombe Wajumbe tuikubali hoja hiyo ya kuomba idhini na nimuombe Mhe. Mjumbe alinde haki yake, Mswada huu ubakie kwake ili utakapoletwa hapa kusomwa mara ya mwanzo, mara ya pili na mara ya tatu uwe umesimamiwa na Mjumbe kutoka miongoni mwa Wajumbe *backbenchers* wa Baraza hili.

Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti nashukuru kwa kunipa fursa hii, na nasema tena naunga mkono hoja ya kuomba idhini na namtakia kila la kheri Mheshimiwa Mjumbe katika kufanikisha lile alilolikusudia kwa niaba yake mwenyewe lakini pia kwa niaba yetu sote ambao tunawakilisha katika chombo hiki.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, naomba na mimi nitoe mchango mfupi sana kwenye hoja hii ya Mhe. Hamza Hassan Juma juu ya haja ya kuanzisha Sheria ya Utawala wa Baraza.

Mhe. Mwenyekiti, ili na mimi nisije nikachafua kwa sababu huu Mswada unaleta mgongano wa kisheria naomba nitoe mafupi sana ambayo nahisi nitilie mkazo kwenye hoja hii ya Mhe. Hamza Hassan Juma, lakini kwanza nimpongeze sana kwa kutimiza wajibu wake kwa mujibu wa Katiba na kwa mujibu wa Kanuni za Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, ni vyema na sisi tukajenga msimamo wa kujisifia. Dunia hivi sasa imekuwa ikimsifu Mhe. Marehemu Mandela kwa jinsi alivyoweka

historia katika ulimwengu huu. Kwa hivyo, na Wazanzibari si vibaya miaka 50 ijayo mbele kumsifu Mhe. Hamza Hassan Juma, kama mwanzilishi wa hoja binafsi kuhusu Mswada wa Sheria, nadhani kama kuna fahari ya kujivunia Baraza hili wahisani wetu wa *UNDP* na wengine wataona kwamba Baraza limefanya wajibu wake ni pale Wajumbe wanapoleta miswada binafsi na hoja binafsi za Wajumbe kwa ajili ya kufanya ufanisi wa Baraza letu.

Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Wawakilishi limeanza mwaka 1979 kama sikosei sasa ni miaka karibu arubaini na zaidi, lakini hakuna Mswada binafsi ulioletwa na Mjumbe tangu Baraza la Wawakilishi lianze. Sasa ni fahari ilioje kwangu mimi kumuona Mwakilishi wa Kwamtipura Mhe. Hamza Hassan Juma, kwamba ameanza kuleta Mswada huu wa mwanzo na naamini na wa Kiwani, Mkwajuni, Makunduchi, wataweza kufuata mfumo huo ili tulete miswada ambayo inawagonga wananchi badala ya kuiachia serikali yenyewe kuleta Miswada pale wanapoona kuna haja.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo nadhani niseme tu kwamba Mhe. Hamza Hassan Juma amezungumza sababu nyingi. Sababu moja ambayo ametaja ukurasa wa kwanza ni tabia ya serikali au dhana iliyopo kwamba serikali imekuwa ikiingilia muhimili huu wa dola wa Baraza la Wawakilishi kinyume na kifungu cha 5 cha Katiba ambacho kimeweka wazi mgawanyo wa madaraka kwenye Katiba ya Zanzibar.

Tuseme kweli Wajumbe wengi wamekuwa wakilalamika kwamba wakati mwengine hata pale maamuzi ya Baraza yanapohitajika tumekuwa tukikwama kwa sababu ya kukosa nyenzo za Baraza la Wawakilishi. Hoja kubwa tunaambiwa kwamba Baraza halina fedha au pengine hatuna nyenzo fulani.

Lakini nadhani tukiweka Mswada huu Mhe. Hamza Hassan Juma, ambao atauleta tukijaaliwa, atayazingatia hayo kwamba ataleta Mswada ambao utajenga uwezo wa Baraza kiutendaji kwa maana ya wataalamu, kifedha na kiutawala kwa ujumla kwa ajili ya kuleta mgawanyo wa madaraka ili tuende sambamba na ulimwengu huu.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Hamza Hassan Juma pia ameeleza kwenye hoja yake hii kwamba tumekuwa tukishiriki vikao mbali mbali vya *CPA*, Mabunge ya Jumuiya ya Madola, lakini kwa hakika hasa sisi tutashiriki kama *associate member* hatujui hasa msimamo wetu, wakati mwengine unaalikwa basi huna hata nyenzo. Tumekuwa tukishuhudia Wajumbe wanaalikwa hapa watu wanavutana kwamba je watakwenda wangapi, fedha ziko wapi.

Kwa hivyo, nadhani Mswada huu wa Mhe. Hamza Hassan Juma akiuleta na tukiwa kuna Mswada ambao umezingatia ujenzi wa Ofisi yetu, nadhani dosari hizi za Wajumbe kushiriki katika mikutano ya kimataifa kutakuwa hakuna dosari kubwa. Nimalizie kusema kwamba Mswada huu Mhe. Hamza Hassan Juma, utakapouleta nikushauri sana.

Serikali wametunga Miswada tangu 1964 hatujawaingilia kuwa Wajumbe binafsi. Mswada huu nikuombe kama ile hoja ya Mhe. Ismail Jussa Ladhu, kwamba usikubali kuwa ni sehemu ya serikali. Ukileta kama sehemu ya

serikali itakuwa hiyo historia na lengo unalotaka kulijenga litakuwa halina nguvu.
Nikuombe sana tafuta wataalamu Barazani, wataalamu wengine wa serikali wakusaidie kama Mhe. Hamza Hassan Juma, Mjumbe binafsi kutoka jimbo la Kwamtipura Mswada huu uulete mapema iwezekanavyo, na nikuombe kwamba serikali imekuwa ikiahidi Miswada kama hii itakuja muda mfupi lakini huchukua muda mrefu. Ili ujenge historia nzuri Mhe. Hamza Hassan Juma nikuombe Januari na si zaidi ya Aprili basi Mswada huu uwe tayari umekamilika. Tuje hapa tuupitishe kama sheria.
Ili historia yako ioneshe kwamba kumbe Mjumbe binafsi ni tofauti na serikali. Kumbe Wajumbe binafsi wanaweza zaidi kuliko serikali. Kuonesha kwamba mtu akiwa binafsi yeye hakuna urasimu katika mambo ya utekelezaji wa haki za wananchi.
Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo niseme kwamba historia hii itaandikwa. Mhe. Hamza jipange na wataalamu wako naamini unao na kama huna tafuta wataalamu uwakodi Barazani na nje ya Baraza. Ili Mswada huu ulete ukombozi kwa Baraza la Wawakilishi na ulete ufanisi kwa Wajumbe wote. Lakini nikushauri kwamba ukitunga Mswada wako basi usisahau kuzingatia nafasi ya waandishi wa habari. Waandishi wa Habari ni muhimili wa nne wa dola, watu wanaamini hivyo. Sasa nikushauri kwamba ukitunga sheria yako hiyo usisahau nafasi ya waandishi wa habari juu ya kupata uwazi na nafasi nzuri katika maslahi ya Baraza la Wawakilishi.
Tumeshuhudia mara kadhaa waandishi wa habari humu wamekuwa wakitumika bila ya mafao au kucheleweshwa. Sasa Mswada wako ukiutunga uzingatie jinsi waandishi wa habari watakavyotumika ndani ya Baraza la Wawakilishi na kupata maslahi yao kama waandishi wa habari wa nchi hii. Nakushukuru sana.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyowasilishwa mbele yetu na Mhe. Hamza Hassan Juma. Mimi kwanza nimpongeze Mheshimiwa huyu kwa ujasiri aliouonesha kwa kuweza kuiandaa hoja hii na kuileta leo kuomba ridhaa kwenye chombo chetu. Mimi naunga mkono mia kwa mia. Mswada huu aulete Mhe. Hamza Hassan Juma, nimeangalia madhumuni na sababu nimeridhika nazo. Tosha kabisa kwamba Mswada huu aulete na atakapouleta tutaujadili, tutauchangia na hatimaye tutaupitisha. Maana huu Mswada ni wetu, wala hatuna wasi wasi. Nakuomba sana Mhe. Mwakilishi kwa hili ndugu yangu, Mwakilishi wangu, maana mimi nimeshakaa Kwamtipura kule, kwa hivyo nakuomba Mswada huu uulete.
Lakini Mhe. Hamza Hassan Juma, ametufunua macho. Na mimi nataka niseme nina azma ya kuja kuifanyia marekebisho Sheria Nam. 4 ya mwaka 2007, nitaleta hoja yangu, Mhe. Mwenyekiti mimi natangaza kabisa. Yeye

ameanza ametuonesha njia.Kwa hivyo, na sisi tutakuwa tunaanza kupenya penya.
Mhe. Mwenyekiti, sina haja ya kwenda mbali sana katika hili, maana muda umeshakuwa mwingi na wachangiaji wapo wengi na sote tunatakiwa tupate kidogo kidogo. Mimi nimekubaliana na madhumuni na sababu zilizomo. Naunga mkono mia kwa mia. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.
Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru mimi nilikuwa nataka kuuliza maswali lakini nikawa naona hii aliyoeleza ni dhamira ya kuomba idhini. Sasa nikaogopa sana nikaja nikaingia kwenye ile *subject* yenyewe, nikawa natafakari sana kwamba haya nitakayouliza naona kama yatakuwa yana maudhui kidogo pengine na huo Mswada wake, haidhuru sijauona, lakini nikaona bora
niahirishe. *Inshaallah* Mwenyezi Mungu akinipa uhai hapo utakapokuja huo Mswada ndio nitakapokuja kuchangia. Naogopa kwenda mbali zaidi wakati hapa inayoombwa ni idhini tu. Ahsante.
Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikupongeze kwa kukalia vizuri kiti chako. Kwa kweli jambo hili ni jipya, kwa hivyo jambo lolote likishakuwa jipya lina matatizo yake. Kwa hivyo, upya huu ndio unaotusababisha huyu anasema hivi, huyu anasema hivi, lakini hatimaye imefika pahala tukaelewana.
Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza nimpongeze sana mtoa hoja Mhe. Hamza Hassan Juma, kwa kuleta nia ya kuwasilisha Mswada wa Sheria ya Utawala wa Baraza katika Baraza hili. Mimi nampongeza sana kwa sababu jambo hili analotaka kulileta ni jambo jema. Pamoja na mamlaka tuliyopewa na Kanuni ya kuwasilisha Mswada, bado fursa hii hatujaweza kuitumia vizuri. Historia ya chombo hiki inaonesha hivyo.
Wenzetu Waingereza ambao ni *supreme* katika nchi za *Commonwealth* karibu asilimia 90 ya Miswada inayojadiliwa katika Bunge lile ni Miswada binafsi, ni asilimia ndogo sana ambayo Miswada yake inawasilishwa na serikali. Kwa kuwa mambo yetu mengi kigezo chetu ni mifano inayotokana na nchi hizi za *Commonwealth* basi mimi nimpongeze sana Mheshimiwa kwa kuandika historia hii ya kutaka kuwasilisha Mswada.
Niungane na Waheshimiwa Wajumbe wale wanaosema kwamba Mswada huu bado Mhe. Hamza Hassan Juma utakapofika hakuna haja tena ya kuchukuliwa Mswada huu na serikali. Bado watuachie wenzetu wa serikali tumalizie jambo hili, kwa sababu sote nia yetu ni moja, serikali na Baraza la Wawakilishi lengo letu sote ni moja, kwa sababu ya mfumo wetu wa kikatiba, ndivyo alivyoeleza mtoa hoja juu ya mgawanyo wa madaraka kwa mujibu wa kifungu cha 55(a)(1). Kwa hivyo, tunatekeleza yale matakwa ya vigawanyo. Kwa hivyo, bado wamuachie Mheshimiwa Mjumbe awasilishe huu Mswada, na kwa sababu ni mzuri, badala ya kuchukuliwa na serikali.
Mhe. Mwenyekiti, nataka niwaambie Waheshimiwa Wajumbe kwamba hoja hii ni yetu pamoja, na kwamba kaiwasilisha Mjumbe mmoja kwa sababu

hatuwezi kuiwasilisha sote pale. Lakini hoja hii ni yetu Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Na kama nilivyosema tutajenga historia ya chombo hiki na itabaki kwenye maandiko.

Nakumbuka Mhe. Mwenyekiti, chimbuko la hoja hii alivyotaka kuiwasilisha Mhe. Hamza Hassan Juma. Mhe. Spika, alitaka kwanza Waheshimiwa Wajumbe wakajifunze katika nchi mbali mbali za *Commonwealth*, na kwa bahati Wajumbe tulipata fursa ya kutembelea nchi karibu saba kuona wenzetu wanafanya nini katika jambo hili. Kwa hivyo, tumejifunza mambo mengi. Tukasema kwamba yapo mambo ambayo yale mazuri tutayaiga na yale mabaya tutayaacha, na yale mazuri ambayo yanafaa ya kwetu tunaweza tukayaingiza ili na wenzetu wengine ambao hawajaanzisha kitu kama hichi wapate fursa ya kuja kujifunza kutoka kwetu. Kwa hivyo, tumekwenda tumejifunza tumerudi.

Lakini kizuri zaidi Mhe. Mwenyekiti, si hilo tu kama alivyosema mtoa hoja, pia tulipata nafasi ya kuonana na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na kumueleza nia hii ya kuwasilisha Mswada huu. Tunamshukuru sana Mhe. Rais jambo hili alilipokea kwa mikono miwili na akalikubali na akatoa maelekezo namna gani liweze kufanyika. Hoja yake Mhe. Rais alisema hatuwezi kubakia nyuma, kwa kuwa wenzetu wanakwenda mbele sisi hatuwezi kubakia hapa tulipo. Lazima twende kadiri wenzetu wanavyokwenda.

Kwa maana hiyo sisi tunaamini kwamba pande zote mbili; upande wa Baraza la Wawakilishi kama muhimili na upande wa serikali kama Rais pia jambo hili tumekubaliana. Kwa hivyo, tunaomba jambo hili liende vizuri, na kwa sababu ni zuri ili umalizikaji wake umalizike vizuri. Jambo hili sisi sio tunaolianzisha, wenzetu nao waliotangulia wamelianzisha baada ya kuona kwamba jambo hili ni jema.

Mimi nimpongeze sana na nimuombe sana Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria mwenzetu Mhe. Abubakar Khamis Bakary atusaidie katika hili ili tuone kwamba azma hii inatekelezwa kwa manufaa yetu. Tutakavyoweza kufanikiwa hili basi naamini na muhimili mwengine kwa sababu mihimili iko mitatu. Kuna utendaji, kutunga sheria na utoaji wa haki.

Kwa hivyo, tutakapomaliza hili na muhimili nao pengine tutauandalia mazingira ya kwenda katika utaratibu kama huu wa kuweza nao kuwa *separate* kama sisi, ili tuone kwamba tunatekeleza vizuri ile dhana ya mgawanyo wa madaraka ambayo yapo kwenye Katiba yetu. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi nakubaliana na mtoa hoja tukubali tumuidhinishie hili jambo na hoja zake nyingi nimeziona, ni za msingi kabisa sina haja ya kuzirudia, ila kubwa tukubaliane na hoja zake ili tuone mswada huu unakwenda utakapofika, tutaujadili na tutauchangia.

Humu kuna jambo moja kubwa sana ambalo jambo hili kwa mujibu wa maelezo ya mtoaji, linakusudiwa kuwemo kwenye mswada huu, hili jambo

moja muhimu sana ambalo tumeanza kulijadili tokea katika Baraza lile lililopita, suala la kuanzisha mfuko wa Bima ya Afya. Waheshimiwa Wajumbe, hili jambo muhimu sana. Katika Baraza lililopita tuliwahi kumpoteza Mwakilishi wa Jimbo la Magogoni, aliumwa maradhi yake yakawa yanajulikana, lakini alishindwa kupelekwa katika matibabu India kwa sababu ya ukosefu wa fedha, tulimpoteza mwezetu hivi hivi.

Na tulifika pahala Waheshimiwa Wajumbe, kwenye vikao vyetu vya Chama tukataka kuwajibisha baadhi ya Mawaziri juu ya kifo kile, lakini tena mambo yakawa yapo nyumbani tukayamaliza. Kwa sababu suala la kuanzisha Mfuko wa Bima ni suala muhimu kwa sababu hili ni kwa ajili yetu, siku hizi maradhi mengi. Sisi Wawakilishi tunapata maradhi ya *pressure* na sukari, wakati mwengine tunahitaji kusafirishwa kwenda nje. Lakini unapokwenda serikalini, serikali inakwambia hakuna fedha.

Kwa hivyo, sheria hiyo itakapokuja na kwa madhumuni aliyozungumza Mhe. Mjumbe, itatusaidia kuanzisha Mfuko wa Bima ya Afya ambayo Mhe. Mjumbe ukitakiwa sasa kusafirishwa kwenda nchi za nje, tena hakuna vikwazo kwa sababu tayari tutakuwa tumeshajenga mazingira ya kupata matibabu.

Mhe. Mwenyekiti, gharama ya Mwakilishi ni kubwa mno anapopoteza maisha, fedha nyingi sana zinatumika katika kurejesha Mwakilishi mwengine, pengine kumsafirisha Mwakilishi kumpeleka katika matibabu India ni milioni arubaini. Lakini kufanya uchaguzi mwengine kwa ajili ya kujaza nafasi ile haipungui milioni mia tano za serikali na hayo tumeyashuhudia.

Kwa hivyo, mimi Mhe. Mwenyekiti, niunge mkono hoja ya Mhe. Mjumbe, tukubali aulete mswada mwenyewe tuje tuujadili kama panapohitaji marekebisho,

tufanye marekebisho ili tuone kwamba sheria hii inakuwepo kwa ajili ya madhumuni yale ambayo yamekusudiwa.

Baada ya maelezo hayo, mimi sina zaidi na kwa sababu muda wenyewe ni wa saa moja, basi nikubaliane na hoja ya Mhe. Mjumbe na niwaombe Waheshimiwa wenzangu wote wa nyuma na wa mbele wakubali kwa sababu hili jambo ni zuri.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

HOJA YA MJUMBE

Hoja ya Mjumbe wa Kuliomba Baraza la Wawakilishi Kutoa Azimio Dhidi ya Vitendo vya Udhalilishaji wa Watoto Zanzibar

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, naomba uniruhusu kuwasilisha hoja ya kuliomba Baraza lako tukufu kutoa maazimio dhidi ya vitendo vya udhalilishaji wa watoto Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imekuwa na dhamira ya dhati ya kuwalinda watoto wa Zanzibar kwa kuchukua hatua mbali mbali ikiwemo ya kuwa na Sheria namba 6 ya 2011 na kuhakikisha kupatikana kwa haki zao ikiwa ni pamoja na kuwapatia elimu bora, makaazi, mavazi, chakula na kuwalinda dhidi ya aina zote za udhalilishaji.

Na kwa kuwa, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeridhia mikataba inayohusiana na haki za watoto duniani ambayo Zanzibar inahusika katika utekelezaji wa mikataba hiyo ili kuona azma ya kuwalinda watoto inafikiwa,

Na kwa kuwa, kumekuwepo na ongezeko kubwa la kesi za udhalilishaji wa watoto, ikiwa ni pamoja na kesi za ubakaji na ulawiti hapa nchini,

Na kwa kuwa, kwa mujibu wa takwimu za Mahakama Kuu ya Zanzibar inaonesha kuwa katika mwaka wa 2010 kesi zipatazo 48 zilifunguliwa, ambapo kesi 35 zilitolewa maamuzi, kesi 13 zinaendelea kusikilizwa na katika kesi zilizotolewa maamuzi ni kesi 2 tu ambazo washtakiwa wake walipatikana na hatia na kuhukumiwa adhabu ya kifungo na 7 kulipa faini na kesi 28 washtakiwa wake wameachiwa huru,

Na kwa kuwa, Kwa mwaka 2011 kesi 74 zilifunguliwa ambapo ni pamoja na kesi 18 za kuingiliwa kinyume na maumbile na kesi 56 za ubakaji, kesi zinazoendelea ni 38 na kesi 36 zimetolewa maamuzi na kati ya hizo zilizotolewa maamuzi ni kesi 2 tu ambazo washtakiwa wake walitiwa hatiani na kupewa adhabu ya kifungo na 2 kulipa faini na kesi 32 washtakiwa wake wameachiwa huru,

Na kwa kuwa, Kwa mwaka 2012 kesi 72 zilifunguliwa zinazojumuisha kesi 10 za kuingilia kinyume na maumbile na kesi 62 za ubakaji ambapo kesi 61 zinaendelea kusikilizwa na kesi 11 zimetolewa maamuzi ambapo kati ya hizo

kesi 2 washtakiwa wake wametiwa hatiani na kupewa adhabu na 1 kulipa faini na kesi 8 washtakiwa wake wameachiwa huru,

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa takwimu za tafiti zilizofanywa na taasisi mbali mbali zikiwemo asasi za kiraia zinaonyesha kuwa kesi nyingi zaidi zimekuwa zikiripotiwa polisi, lakini zimeshindwa kufikishwa Mahakamani kutokana na sababu mbali mbali zikiwemo za kukosekana kwa ushahidi,

Na kwa kuwa, mbali na takwimu za Mahakama kutoonyesha hali halisi ya matukio mengi ya udhalilishaji wa watoto hapa Zanzibar, bado inaonyesha kuwa tatizo hilo ni kubwa sana nchini,

Na kwa kuwa, kesi nyingi zinazofikishwa Mahakamani zimeshindwa kuthibitishwa kutokana na sababu mbali mbali na hivyo kupelekea washitakiwa wengi kuachiwa huru na hatimae kupelekea kuongezeka kwa vitendo hivyo vya udhalilishaji kwa watoto wetu,

Na kwa kuwa, Serikali inapaswa kuchukua hatua madhubuti ili kuwalinda watoto hao dhidi ya udhalilishaji na pale inapotokea watoto hao kufanyiwa vitendo hivyo vya udhalilishaji, kuhakikisha wahusika wa vitendo hivyo wanachukuliwa hatua kali kwa mujibu wa sheria ili kukomesha kabisa vitendo vya udhalilishaji kwa watoto wetu,

Na kwa kuwa, hali halisi ilivyo sasa hasa katika uendeshaji wa mashtaka ya wanaotuhumiwa kufanya udhalilishaji wa watoto, inaonyesha kuwa bado tunashindwa kulikabili tatizo hili na hivyo wahusika wengi wa vitendo hivyo kuendelea na vitendo hivyo bila ya kupatikana na hatia kutokana na udhaifu wa mfumo mzima wa utoaji haki katika kesi za aina hii,

Na kwa kuwa, endapo hatua madhubuti hazitochukuliwa katika suala hili, watoto wengi wanaweza kuathirika kiafya na kisaikolojia na hivyo kuathiri maendeleo ya watoto hao na pia kuwafanya waathirika wa matukio haya ya udhalilishaji watoto kupoteza imani na mfumo mzima wa utoaji haki,

Hivyo, mimi, Mgeni Hassan Juma, Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi nafasi za wanawake, chini ya kanuni ya 27(1)(n), 27(3), 49 (1) na kanuni ya 50 ya kanuni za kudumu za Baraza la Wawakilishi toleo la 2012, naliomba Baraza hili tukufu, kwa kutumia mamlaka iliyonayo, liridhie kupitisha maazimio yafuatayo:-

1. Kuitaka serikali ianzishe Mkakati wa Kitaifa wa Kupambana na Kutokomeza Udhalilishaji wa watoto utakaojumuisha Wawakilishi wa makundi mbali mbali katika jamii wakiwemo viongozi wa dini,

polisi, makundi ya wanasheria, asasi za kiraia, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Wakuu wa Wilaya, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Wizara nyengine zinazohusika,

2. Kwamba katika bajeti ya serikali ya mwaka 2014/2015 na bajeti zitakazofuata, Mkakati wa kupambana na kutokomeza udhalilishaji wa watoto, uwe ni miongoni mwa vipaumbele vya serikali ili hatua za kupambana na udhalilishaji wa watoto zinazohitaji rasilimali fedha ziweze kutekelezeka bila ya vikwazo,

3. Kwamba miongoni mwa majukumu ya msingi ya Mkakati wa Kupambana na Kutokomeza Udhalilishaji wa Watoto yazingatie utoaji wa taaluma kwa jamii kwa ujumla kuhusu namna ya kuwalinda watoto dhidi ya vitendo vya udhalilishaji na pia namna ya kushughulikia matukio ya udhalilishaji watoto pale yanapojitokeza,

4. Kwamba kutokana na udhaifu ulioonekana katika kushughulikia kesi za udhalilishaji watoto, serikali ianzishe utaratibu wa mafunzo ya pamoja ndani na nje ya nchi katika vipindi maalum kwa wahusika wanaosimamia mfumo wa utoaji haki katika kesi za watoto wakiwemo mahakimu, waendesha mashtaka, polisi, madaktari na makarani wa Mahakama ili kuyajengea uwezo makundi hayo katika kushughulikia kesi za udhalilishaji watoto na pia kuleta uratibu wa pamoja (*coordination*) miongoni mwa taasisi hizo,

5. Kwamba serikali iingize katika mitaala ya elimu hasa katika ngazi ya elimu ya awali na elimu ya msingi suala la udhalilishaji watoto na namna ya kujikinga dhidi ya udhalilishaji huo,

6. Serikali iwekeze rasilimali zaidi ili kuziimarisha Mahakama za Watoto kwa kuweka idadi ya kutosha ya Mahakimu wa kudumu wa Mahakama hizo, majengo, samani na mambo mengine yatakayofanya kesi hizo zisikilizwe katika muda mfupi na kwa kuzingatia haki,

7. Serikali ifanye mapitio ya Sheria ya Mtoto na sheria nyengine zinazosimamia uendeshaji wa kesi za udhalilishaji wa mtoto ili kuleta tija katika uendeshaji wa kesi hizo ikiwemo kuweka muda maalum ambapo kesi hizo za udhalilishaji zitapaswa kuwa zimemalizika,

8. Katika kurahisisha upelelezi wa kesi za udhalilishaji wa watoto, serikali ihakikishe ndani ya kipindi kifupi kijacho mashine ya uchunguzi wa vinasaba (*DNA*) inapatikana hapa Zanzibar,

9. Kwamba serikali ilete kila mwaka katika Baraza la Wawakilishi ripoti ya hatua zinazochukuliwa katika kulikabili tatizo la udhalilishaji wa watoto, itakayoonyesha hatua zilizochukuliwa katika kuzuia tatizo hilo na matokeo yake na pale matukio ya udhalilishaji yalipojitokeza, hatua zilizochukuliwa na matokeo ya hatua hizo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mjumbe kwa kutoa hoja yako na vile vile Wajumbe kwa kui-*support* na sasa.

UTARATIBU

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwa mara ya pili, naona leo ndio maana kunatokezea mkanganyiko, nadhani hoja ikishawasilishwa, utaratibu ni kwamba ijadiliwe kwanza halafu ndio utuhoji. Sasa ukishakutuhoji kwanza, halafu tunashangaa tunajadili nini.

Kwa hivyo, nadhani Mhe. Mwenyekiti tupe fursa tujadili halafu baada ya kujadili, utatuhoji.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nataka kwa mara nyengine niendelee kukushukuru kunipa nafasi hii nikaweza kuchangia hoja hii ya Mheshimiwa ndugu yangu Mhe. Mgeni Hassan Juma, hoja hii ni muhimu sana na kwa kweli Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa nataka niseme kwamba sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi humu ndani kila mtu kaingia kwa tiketi yake na tunaishukuru sana ofisi yako Mhe. Mwenyekiti kupitia kwa Mhe. Spika. Katika kipindi ambacho Baraza la Wawakilishi limetoa mafunzo ya kutosha kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi basi hili Baraza lako la kipindi hiki cha awamu ya saba.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nipo katika Baraza hili hii awamu ya tatu, nimeingia mwaka 2000, 2005 na 2010 nimeingia tena na *inshaalla* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu ninaamini nitaendelea kuwemo. Sasa Mhe. Mwenyekiti, kwanza tujiulize huko majimboni tunakotoka huku tunakuja kufanya kazi gani. Hilo ndio la mwanzo la kujiuliza, tukishajijua tumekuja kufanya nini, basi naamini tutaweza kufanya kazi zetu kwa vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, tulipofika hapa Barazani tulikabidhiwa mambo mawili. Kwanza Katiba ya Zanzibar, lakini vile vile na Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Lakini vitu hivyo haviwezi vikatekelezeka moja kwa moja bila kufuata na Kanuni. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, kwa muda mrefu tumekuwa sisi watu wa *hewalla*, sisi tunasubiri kuletewa tu, kila siku tuletewe tu. Sasa mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti, bado wananchi wetu waliotuleta hapa tutakuwa hatujawatendea haki.

Mhe. Mwenyekiti, leo kwa mara ya mwanzo na sisi tumeandika historia, tumeleta hoja ya mswada wa Baraza ingawa kuna baadhi ya Wajumbe walikuwa na hofu kuiunga mkono ile hoja, lakini mimi nataka niseme kwamba kwa mfumo wetu wa Zanzibar sote humu ndani ni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, pamoja na Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na yeye ni Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Sasa kwa kuwa Mhe. Rais wetu aliunga mkono nia hii, sasa mimi bado sina wasiwasi kama atakuwepo Mjumbe atakaekuwa na wasiwasi au gati gati wa kuunga mkono ile hoja. Kwa sababu kwanza tunatekeleza majukumu yetu kikatiba na hili linalofanyika sasa hivi Mhe. Mgeni Hassan Juma, hoja yake aliyoileta hii, ni kadhia ambayo tumeshasema sana, lakini kama tutaendelea kulalamika sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao wananchi wetu ndio wametuchuja wakaamini kwamba sisi tunaweza tukaja tukawakilisha mawazo yao na kuwaondolea kadhia katika maeneo yetu.

Sasa ikiwa sisi bado tunaendelea kulalamika wao wakimbilie wapi. Mhe. Mwenyekiti, mimi nakubaliana na hoja hii ya Mhe. Mgeni Hassan Juma, lakini pia na mimi nitatoa maoni yangu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza suala la kesi za ubakaji, yaani sasa hivi imekuwa ni kitu cha kawaida kabisa yaani wale wabakaji wameshaota suguru, hawaogopi wala hawajali. Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani sisi ndio tunaotunga sheria, tuangalie ni maeneo gani ambayo yana udhaifu katika sheria zetu na kama tulivyoanza leo tusiisubiri serikali. Mhe. Mwenyekiti, nimejaribu kuangalia moja katika hoja ya Mhe. Mgeni Hassan Juma, katika yale mapendekezo yake namba 7, anasema:

> "Serikali ifanye mapitio ya Sheria ya Mtoto na sheria nyengine zinazosimamia uendeshaji wa kesi za udhalilishaji"

Mhe. Mwenyekiti, serikali ina mambo mengi kama kutuletea maendeleo na huduma za jamii, sasa hizi kazi nyengine kwa kuwa na sisi kanuni zetu zinaturuhusu tuzipitie, tuitafute Sheria hii ya Watoto na tuipitie, tuijadili,

halafu tutoe mapendekezo kisha tulete *draft* ya marekebisho, serikali hii Mhe. Mwenyekiti, kwanza hakuna mtu aliyezaliwa akawa Waziri, kila mtu kama nilivyosema kaingia humu kwa tiketi yake. Umeletwa na wananchi, wanawake au na nyumba kubwa, sote kwa ajili ya kuwatumikia wananchi wetu.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba sana kwamba haya mapendekezo ambayo tuliyoyatoa, serikali ifanye, lakini tusiiachie serikali peke yake, tuanze kuandaa *draft* tofauti tofauti na Mhe. Mwenyekiti, juzi nilikuwa ninafuatilia katika utendaji wa serikali, mimi sasa hivi ninashukuru, wenzetu Wizara nafikiri inayoshughulikia *NGO'S* na Wizara inayoshughulikia mambo ya Utawala Bora, hivi karibuni walifanya tafiti, wakagundua Zanzibar kuna *NGO'S* zaidi ya 1000, lakini walipokuja sasa kufanya uhakiki hivi karibuni, wameanza kufanya uhakiki, wamekuta *NGO'S* nyingi zimo ndani ya *briefcase*, wakati *NGO'S* hizi mwenzangu Mhe. Salmin Awadh Salmin, alizungumza.

Uingereza miswada mingi inapelekwa na Wabunge, lakini wale sio kama wanakaa tu wanapeleka, ile miswada mengine inapelekwa na hizi *NGO'S* na hizi *NGO'S* zinakuwa kama ni *pressure group*, wao wanakaa wanajadili kwa sababu *NGO'S* zina *specific issue*. Kuna *NGO'S* zinazoshughulikia mazingira, kuna *NGO'S* za ukimwi, kuna *NGO'S* za masuala kama haya ya watoto na mambo mbali mbali. Sasa hawa wenzetu *NGO'S* wasibakie kusubiri fedha za wafadhili tu, wakae wajaribu kuangalia zile kadhia kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, ninavyokwambia *NGO'S* wao wanafanya kazi kubwa zaidi.

Wanakwenda kwenye *grass root*, wanatafuta matatizo mbali mbali ya wananchi. Juzi alikuja ndugu yetu Mzuri Issa, tunamshukuru sana, amekuja ametufanyia semina, ametuonesha utafiti, udhalilishaji unaofanywa na sisi wanaume tunaowafanyia wanawake, amekwenda vijijini, ameugundua amekuja kutwambia pale.

Sasa utakuta wenzetu hawa sio wafanye utafiti tu halafu waje na *summary* ya mapendekezo, *summary* ya mapendekezo sisi ndio tutakaosababisha kuangalia, je, tatizo hili liko katika Wizara gani, sheria gani na mapungufu ili tuwaletee mawaziri ili waweze kutusaidia hii kazi. Kwa hivyo, bado mimi nataka niseme kwamba sasa hivi wakati tu wa kusubiri hodi hodi nyumbani tuupunguze tufanye kazi yetu tuliyojia hapa. Kuna sheria mbali mbali Mhe. Ali Mzee Ali, hodari sana wa mambo ya historia sijui yuko wapi, sasa hivi tunataka tumpe kazi ya *research* ya sheria, tushamuona katika kufanya *research* ya mambo ya historia, kwa kweli yuko vizuri sana.

Sasa hivi ninafikiri tutaanza kumtumia, tutamtengenezea ofisi moja hapa ili sasa aanze kutufanyia kazi ya *research* za sheria za ukoloni zilizokuwa bado hazijarekebishwa na sheria zinazoleta udhalilishaji hapa Zanzibar ili tuweze kufanya marekebisho, *otherwise* Mhe. Mwenyekiti, tukiendelea kulalamika hapa sote wananchi wetu watakuwa hawana pakukimbilia.

Mheshimiwa, Mhe. Mgeni Hassan Juma, hapa ametoa takwimu mbalimbali, kesi za ubakaji wa watoto, mimi nataka nikwambieni siku zote tunalaumu mataifa ya magharibi, wanasema oo maana yake tunaletewa sheria ambazo baadae tunaambiwa sijui, maana yake hivi karibuni mataifa makubwa waliwahi kusema kwamba mataifa yale ambayo hayathamini haki za makundi madogo, basi zinaweza zikapunguziwa misaada au zikakosa misaada.

Na tafsiri ya haya makundi madogo Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi yamo katika hii takwimu makundi haya yamo. Maana yake hapa Mhe. Mwenyekiti, unapozungumza ubakaji wa watoto wadogo hasa wa kiume, sikusudii kwamba ninaposema hasa wa kiume, wakike wadhalilishwe hakuna. Kwa sababu hawa wa kiume, maana yake takwimu hizi baadae wakishafanyiwa lile tendo, baadae watakuwa na hisia za kufanya majaribio mengine.

Pale walifanywa kwa nguvu, je, wakifanywa kwa hiari, inakuwa vipi matokeo yake, inakuja mwisho wanazoea, baadae wale watakuja kuunda umoja wao. Dar es Salaam wenzetu wameshafanya mkutano hapo, wakaenda hawa tunaowaita sasa makaka poa, wamekwenda na wameanza kudai haki zao. Kenya wenzetu hapa Mhe. Mwenyekiti, tayari wamefika mpaka kuandamana, wao pale wana siku maalum wanafanya sherehe. Tena walifanya maandamano wakawalani Polisi, wanasema wanawaingilia katika shughuli zao.

Sisi leo tumekuwa tukiwalaumu hawa watu makaka poa, lakini tujiulize leo tunamlaumu yule tulimjua kaanza vipi, wengine Mheshimiwa, wanaanzishwa na wazee wao, ni tatizo. Sasa Mhe. Mwenyekiti, tusilaumu tulivyoangukia, tulaumu tunapojikwaa. Mheshimiwa, wengi wao ukiangalia historia yao, walifanyiwa mambo ambapo walikuwa hawana maamuzi, walikuwa bado watoto wadogo, lakini baadae yakawakolea na wakaendelea. Sasa mimi naomba Mhe. Mwenyekiti, maana yake haya tunayosema tusiletewe sheria hizi za kulazimishwa, lakini hawa wakeshakuwa wengi watakuja kusimama barabarani watakuja kudai haki zao.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kitu ambacho ninachotaka kukisema, kwamba udhalilishaji sasa hivi wa watoto umekuwa mkubwa, wananchi hawana pakwenda, vituo vya Polisi wameshachoka kwenda maana yake wanatolewa katika vyombo vya habari, nimemkuta mama analia na mtoto wake, kuna mmoja hivi karibuni pale Mahakamani kesi imetolewa hukumu, yeye alau kashukuru anasema alau Mahakama imetoa hukumu, lakini mtoto wangu, je, mtoto keshaharibiwa, Mahakama imeshatoa hukumu, lakini Mahakama ikishatoa hukumu ina maana yule mtoto lile tendo alilofanyiwa ina maana linafutika hakufanyiwa tena.

Mhe. Mwenyekiti, nataka kusema mwanamme ni mwanamme, kuna mambo mwanamme ukeshafanyiwa, unakuwa tena hujisikii kusimama mbele ya hadhara ya watu na ukajinasibu kwamba wewe mwanamme. Sasa leo hawa tukisema tunawaachia Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani kwa kweli tutakuwa tunaumiza taifa letu na haitoweza kutusaidia. Sasa kitu ambacho ninachotaka kukisema, Mhe. Mgeni Hassan Juma, umefanya jambo zuri, umefanya takwimu na takwimu hapa umetuletea kwa kweli hizi takwimu zinasikitisha sana.

Sasa mimi kitu ninachotaka kukiomba wenzetu hasa Jeshi la Polisi, Jeshi la Polisi tumesikia na wao wakilalamika, maana yake sisi Wawakilishi tunalalamika na Jeshi la Polisi wanalalamika, Jeshi la Polisi wanalalamika nini, wao wanalalamika Mhe. Mwenyekiti, wanasema aa wakati mwengine hapa jambo limeshafanyika, mzazi kafanyiwa mtoto wake tendo lile, kisha anakuja mzazi anasema aa basi tushakubaliana. Kweli wazazi wana haki ya watoto wao, lakini wana haki vile vile ya kukubali kupewa pesa ili iwe suluhu ya kudhalilishwa watoto wake.

Sasa mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti tuwaombe na wenzetu Jeshi la Polisi wafate taratibu za kisheria, tena hizi kesi zina hukumu nzuri tu, kesi za udhalilishaji hizi miaka 35 na sheria ipo tayari. Lakini sasa tujiulize kwa nini hii sheria haifanyi kazi ipasavyo. Mimi nampongeza sana Mhe. Asha Bakari Makame, sijui yuko wapi.

Mhe. Asha Bakari Makame, kuna kipindi alikuwa Waziri anayeshughulikia mambo ya watoto, alikuwa akimsikia mtu kambaka mtoto, anamganda mpaka ajue dakika za mwisho, Kitangi nafikiri alikufia jela, ilikuwa kesi kubwa kwenye vyombo vya habari. Sasa mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi kweli mambo haya yanatakiwa ushahidi kamili na vitu vingine, ushahifi mtoto keshaharibiwa, unamkuta anakwenda kama kaa, tena ushahidi gani unaotakiwa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba sana haya mambo ya muhali na vitendo hivi mara nyingi hasa wale wazee wanaokwenda polisi sana ni wale wanaofanyiwa ndani ya familia, mwengine unaweza ukamkuta sijui mjomba wake, kaka yake au baba yake mdogo.

Hivi juzi ndani ya wiki hii tulisikia kuna mtoto wa miaka minne kabakwa na mtoto wa miaka 20, huyu miaka 20 si mtoto tena, anajua anachokifanya, hebu tuangalie mtoto ana miaka minne. Lakini pia kuna kesi nyengine miaka miwili. Mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti, ifike pahala sasa hivi lazima tuisaidie serikali yetu kuangalia kwenye mapungufu ya sheria tuwakumbushe ili kuhakikisha kwamba hayo masuala yanamalizika.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, katika suala la ushahidi. Mhe. Mwenyekiti, mazingira ya ushahidi kwa kweli bado imekuwa kitandawili. Maana yake hapa tuliambiwa kimeanzishwa kituo cha *One Stop Centre* Hospitali ya Mnazi Mmoja na pale tunaambiwa unamkuta daktari, polisi, sijui mtu wa sheria, lakini bado pamoja na jitihada zote hizo kuna kitu kinachobakia. Kwa sababu mtoto unaambiwa ukishamkuta kafanyiwa vitendo viovu, umpeleke katika kituo cha *One Stop Centre* bila ya kumsafisha.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mtoto anatoka kijijini keshafanyiwa vitendo vibaya mpaka anakauka anakwenda pale keshakauka kafanya magamba, yaani kwanza kile kitendo cha kumtoa mtoto kule kijijini mpaka ukamleta pale tayari keshadhalilika kwa kiasi kikubwa, utu wake tayari umeshaondoka. Mwisho wake hapo *One Stop Centre* unakujakuambiwa hakuna kipimo cha *DNA*. Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba sana.

Rafiki yangu Mhe. Waziri wa Afya, mwaka uliopita tulivutana hapa kidogo katika suala la *ICU* na alitishia kujiuzulu, akasema kwa kipindi cha miezi sita kama *ICU* itakuwa bado haijatengenezwa atajiuzulu. Lakini tunashukuru serikali yetu na tunamshukuru sana Mhe. Waziri wa Fedha, kwa sababu alisimama na yeye akaahidi atashirikiana na Mhe. Waziri wa Afya, ili kuitengeneza mashine ya *ICU*. Tunashukuru kwamba *ICU* iliweza kutengenezwa pamoja na mambo madogo madogo, lakini angalau tuliona zile jitihada za serikali.

Mhe. Mwenyekiti, mwezi ujao hapa tutakuja tena katika Baraza na tutajadili Ripoti za Kamati katika eneo moja ambalo tutaitaka serikali kuhakikisha inaacha shughuli zake zote na kututafutia mashine ya *DNA.* Mhe. Mwenyekiti, sisi ndio tunaopitisha bajeti.

Hivi karibuni nakumbuka Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, alipokwama kwamba Zanzibar tutaachwa nyuma kutoka kwenye

analogy kwenda katika *digital*, tunamshukuru Mhe. Rais wetu kwa sababu Mheshimiwa yeye ndiye anayesema hataki tuonekane tuko Zanzibar ya zamani anataka twende na wakati, alikubali akatoa kibali karibu shilingi bilioni nane Mhe. Waziri wa Fedha, alizitoa kwa mujibu wa maelezo ya Mhe. Waziri, tukaweka mitambo ya *digital* na sasa hivi mambo yako mbioni, ndio mabadiliko lazima yataleta changamoto na hizo changamoto sisi tunazikubali.

Sasa ili Mhe. Waziri wa Afya, asije akatishia tena kujiuzulu, tunaomba sana katika bajeti ya mwaka huu serikali ituletee fedha, itutengee tuone katika fungu la Wizara ya Afya inanunuliwa mashine ya *DNA*.

Mhe. Mwenyekiti, madaktari wetu wanakwenda kupeleka *DNA* Dar es Salaam, kule hiyo mashine yenyewe ya *DNA* iliyokuwepo sijui kama moja au mbili hazitoshi, tunaambiwa kuna foleni unaweza ukakuta kuna watu 150. Kuna kamati yetu pamoja na Mhe. Mgeni Hassan Juma na ndio maana akaamua kuvuta na kuleta hoja hii, kwa sababu kuna kesi ya udhalilishaji tuliifuatilia, hayo magamba yaliyopelekwa kule kwenda kufanyiwa *DNA*, maana yake sio rojo tena yashakuwa magamba, maana hata hicho kifaa chenyewe cha kuhifadhia hakitambulikani.

Lakini baada ya kupelekwa kule Mhe. Mwenyekiti, ndani ya miezi tisa haijaletwa jawabu. Sasa leo jamani bajeti ya Serikali ya Zanzibar na bajeti ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni bajeti mbili tofauti, sisi tunajitegemea 100% mapato yetu Zanzibar, bajeti yetu sisi hatutegemei fungu kutoka Jamhuri ya Muungano.

Sasa leo tunashindwa kukamilisha mambo yetu mpaka twende Muhimbili kwenda kufanyiwa *test* ya *DNA*. Mimi nadhani bado hatujawatendea haki wananchi wetu. Sasa naomba sana, kwa sababu haya yote tunayoyazungumza unatakiwa ushahidi kamili, ushahidi kamili ni *DNA*.

Mhe. Mwenyekiti, naomba usiniambie bado dakika tano nishakuona, namalizia dakika tano zilizobakia. Mhe. Mwenyekiti, naamini ikiweza kupatikana mashine ya *DNA*, zile sababu ambazo hazina msingi kwa sababu hata wale madaktari wetu pale weshachoka, wanasema jamani siku zote mnatuletea vitoto tunavipekua, tunavichungulia halafu matokeo yake hakuna jawabu. Sasa mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti, tufike pahala.

Leo imekuwa watoto wetu baada ya kuwavisha *uniform* asubuhi kwenda skuli, roho mkononi mpaka mtoto arudi, leo imekuwa vitoto vya siku hizi kushikwa shikwa nyuma si kitu cha kushangaa. Zamani sisi unakwenda huna historia ya kushikwa shikwa nyuma, lakini leo mtoto kila akienda akirudi umpekue, je, vipi hajapitiwa. Hii ndio hali tuliofikia. Sasa mimi nadhani

imefika pahala kwamba hawa wanaofanya vitendo hivi vya ubakaji hasa watoto wetu wadogo, kwa kweli wajue kwamba Wawakilishi wapo wamechachamaa, wanawatetea wananchi wao ili suala liweze kukoma mara moja.

Mhe. Mwenyekiti, lakini sio suala la watoto tu na hata walemavu. Mhe. Mwenyekiti, ulemavu uko wa aina nyingi, kuna ulemavu wa viungo, lakini pia kuna walemavu wa akili. Mhe. Mgeni Hassan Juma, hoja yake zaidi imehusu watoto, lakini udhalilishaji hauko kwa watoto peke yake, kuna walemavu hawa wenye ulemavu wa akili, wanabakwa ovyo na ndio kama hivyo ushahidi Mahakamani mtu aliyekuwa akili zake pungufu, unakuwa hauchukuliwi sana.

Kwa hivyo, bado tuna matatizo mengi, mimi nafikiri iko haja ya kuziangalia upya sheria zetu ili kuhakikisha kwamba hii *One Stop Centre* ishughulikie kesi za ubakaji watoto wadogo, lakini vile vile kesi za udhalilishaji na watu wenye ulemavu hasa ulemavu wa akili.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho kabisa mimi nataka niombe, Mhe. Mbarouk Wadi Mussa, leo aliomba marekebisho ya lugha hapa katika suala la kupiga kelele, mimi nasema Mhe. Mwenyekiti, tumeshasema sana na sisi maneno yetu kama taratibu tulizozipitisha na uchunguzi wowote tunaoufanya, basi hauwezi ukachukuliwa kama ni ushahidi Mahakamani.

Sasa tunaomba basi wenzetu Jeshi la Polisi na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, lakini zaidi Mahakama Mhe. Mwenyekiti, na kiti chako tupate semina. Serikali walifanya semina moja kubwa ya maridhiano baina ya serikali na Baraza la Wawakilishi, bado tunahitaji tupate semina nyengine ya watendaji wakuu wa serikali, Mahakama, Mawaziri pamoja na sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kwa sababu sisi vyenginevyo itakuwa huku kazi yetu ndio kupiga kelele tu, unasema jambo na ushalitungia sheria, halitekelezwi itakuwa sawa sawa na kelele. Maana yake unapiga makelele ikisha inaishia hivi hivi. Lakini hapa sisi tunasema na kwa kuwa tunasema tuna *hansard*, hapa tangu ezi za Marehemu Mhe. Hamad Ali Fadau *hansard* zao ukienda zipo, aliyesema sijui nani makobe yatiwe rangi, kila kitu kinakuwa kipo. Sasa haya sio makelele, hizi ni hoja, sisi tunajenga hoja na ndio maana hoja zetu zinakwenda na kanuni, ukikiuka unapigiwa buti mpaka unakaa sawa unaendelea.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, naomba sana kama sisi hatujakaa na watu wa Mahakama kwa sababu unajua wenzetu wa Mahakama pengine na wao wana sababu zao, pengine hizi sheria tunazozitunga tukawapelekea kwa sababu wao wale wanatafsiri tu, pengine hizi sheria tunazozitunga haziwasaidii kuweza

kutoa hukumu kwa wakati muwafaka. Mimi kitu ninachosema naomba hili Mheshimiwa, kwa kuwa serikali itakuwa inachelewa ofisi yako iweze ku-*facilitate,* tuandae kitu kama hicho, tuweze kukaa pamoja.

Mimi naamini tukikaa Mahakama, Mkurugenzi wa Mashtaka, Jeshi la Polisi, sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na serikali, haya tutayazungumza na kwa sababu kila mmoja ana sheria zake, polisi atasema mimi sheria hii ndio inayonisababisha nishindwe kuleta ushahidi, Mkurugenzi wa Mashtaka na yeye atasema vyake, serikali watasema na sisi Baraza la Wawakilishi tukiondoka pale tutaondoka na kitu kimoja. Kwa hivyo, tutatunga sheria kuondoa kabisa masuala ya udhalilishaji.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache mimi naunga mkono mapendekezo haya aliyoyaleta Mhe. Mgeni Hassan Juma, na naomba sana Wajumbe tuichangie kwa sababu watoto wanaoharibiwa ni watoto wa Kizanzibari, hatutaki baada ya miaka 20 tujetuwe na Wazanzibari kundi likaja likaanza kudai haki zao, kundi lile tutakuwa tumelitengeneza sisi.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi hii naunga mkono hoja.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa kwa mara ya pili leo kusimama kuchangia hoja za Wajumbe binafsi. Lakini vile vile, naomba nimshukuru na kumpongeza kwa dhati kabisa Mhe. Mgeni Hassan Juma, Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kupitia nafasi za viti maalum kwa kuona uzito wa suala hili na kuleta hoja binafsi ndani ya Baraza hili.

Mhe. Mwenyekiti, leo nina furaha sana kwa sababu chombo chetu kinaonesha jinsi kinavyokua kidemokrasia. Mara nyingi nilikuwa napata tabu sana ninapoona mara nyengine Wajumbe tunapotaka kuleta hoja binafsi inakuwa ni kama vile unaomba hisani wakati hili ni suala ambalo ni haki yetu katika kanuni zetu.

Mhe. Mwenyekiti, kanuni zetu kanuni ya 27(3) inasema:

> “Bila ya kuathiri masharti mengineyo ya Kanuni hii, kutakuwa na muda maalum kwa ajili ya Baraza kushughulikia hoja za Wajumbe ambao utakuwa ni siku moja katika mkutano wa kawaida wa Baraza na siku tatu katika Mkutano wa Bajeti ya mwaka ya Serikali”

Mhe. Mwenyekiti, kanuni hii mara nyingi pamoja na kwamba imetoa maelezo ya wazi kabisa kwamba kunataka kutengwe muda wa siku moja katika mkutano wa kawaida kama huu tunaoendelea nao na siku tatu katika mkutano

wa bajeti. Mara nyingi imekuwa Wajumbe tukitaka kuleta hoja binafsi, tunaambiwa bajeti ni ndogo hakutakuwa na muda wa kuongezea suala kama hilo, wakati kanuni zetu ziko wazi.

Kwa hivyo, nafurahi kwamba kuanzia mkutano huu tumeweka historia kwamba leo tumepokea hoja tena hoja nzito, hoja inayohusu Mjumbe kuomba idhini ya Baraza ili kuleta mswada binafsi kwa mujibu wa kanuni ya 81 ambayo historia hiyo kaiweka Mhe. Hamza Hassan Juma na ataingia katika historia.

Lakini vile vile, kwamba katika siku hii hii moja tuna hoja ya pili ambayo ni ya Mhe. Mgeni Hassan Juma, ambae ameleta kuhusiana na suala zito linaloathiri jamii yetu hivi sasa, suala la udhalilishaji wa watoto hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, hoja ni ya kina na imefanyiwa utafiti na ushahidi wake ni takwimu ambazo zimo katika maelezo ya utangulizi wa hoja hii. Hoja hizi Mhe. Mwenyekiti, kwa nini Mhe. Mjumbe, kaona kuna haja ya kuleta suala hili hapa. Kwa mtazamo wangu mimi nilivyofahamu ni kwamba Mhe. Mjumbe kashitushwa na kesi ambazo zinapelekwa katika vyombo vya kusimamia sheria iwe ni Polisi au Mahakama, lakini baadae ukitizama takwimu ya kesi ambazo zinamalizika kwa kupata hukumu zimekuwa ni idadi ndogo sana kulinganisha na kesi ambazo zinafikishwa katika vyombo hivi.

Kwa hivyo, zinatisha, katoa takwimu za mwaka 2010, 2011 na 2012; na ikiwa mtiririko wenyewe ndio huu Mhe. Mwenyekiti, kusema kweli hali inatisha sana.

Sasa yako maswali ya kujiuliza kwamba kwa nini, kwanza kuna uchache wa idadi ya kesi ambazo zinafikishwa, ukilinganisha na ukubwa wa tukio au matukio ambayo tunayasikia katika mitaa na vijiji mbali mbali vya nchi yetu. Je, kuna muamko mdogo, je, ni muhali, je, jamii yetu bado haijaelimika kuona kwamba hili ni tatizo kubwa linapaswa kuchukuliwa hatua. Hivyo, hii ni hatua ya mwanzo kwa maana ya kuripoti kesi hizi.

Lakini la pili, kuna sababu gani zinazokwaza kwamba zile kesi ambazo zinafikishwa katika vyombo vya kusimamia sheria iwe ni polisi au Mahakama ikawa hatimaye hukumu zinakuwa chache sana, na hivyo, kwa mujibu wa Mjumbe aliyeleta hoja hii akaona kwamba ni sababu inayopelekea washitakiwa wengi kurudi katika jamii na pengine kwa sababu wanahusika, lakini ushahidi haukutosheleza wakaendeleza vitendo vile na tatizo likaendelea kukua mwaka hadi mwaka.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niungane na Mhe. Mjumbe, aliyemaliza kuchangia punde Mhe. Hamza Hassan Juma, kwamba tatizo hili lipo. Mhe. Mjumbe, hakuleta hoja ya kuzuwia watu kustarehe baina ya watu wazima huko, lakini kaeleza hisia zake kwamba hivi tumefika pahala katika jamii hii yenye ustaarabu Zanzibar kwamba tumeshindwa kutafuta njia ya mtu kumaliza matamanio yake mpaka aende kwa watoto, ndio kiini cha hoja hii. Mhe. Mwenyekiti, nchi hii imeweka historia nyengine mwaka 2011 ilipoleta sheria ambayo inalinda haki za mtoto.

Sasa Mhe. Mjumbe, kaomba Baraza hili lipitishe maazimio nambari 1 hadi 9 ili kwa mujibu wa imani yake kwamba haya yakichukuliwa hatua yataonesha kwamba angalau chombo hiki kinajali na kiko pamoja na wananchi katika kushughulikia tatizo hili. Lakini vile vile, kitatoa maelekezo kwa serikali juu ya hatua za kuchukuliwa ili angalau kuonesha kujali na kukabiliana na tatizo hili kwa upande wa serikali.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza niseme nayaunga mkono maazimio yote 9 aliyopendekeza Mhe.Mjumbe, lakini nilikuwa naomba kuongezea indhari katika maeneo machache na mengine kuyawekea msisitizo. Kwanza naomba nizungumzie azimio alilopendekeza nambari 3.

Hapa kasema kwamba miongoni mwa majukumu ya msingi ya mkakati wa kupambana na kutokomeza udhalilishaji wa watoto, yazingatie utoaji wa taaluma kwa jamii kwa ujumla kuhusu namna ya kuwalinda watoto dhidi ya vitendo vya udhalilishaji na pia namna ya kushughulikia matukio ya udhalilishaji watoto pale yanapojitokeza.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, naliunga mkono suala hili kama nilivyosema nayaunga mkono yote, lakini hapa nataka nimuombe Mhe. Mjumbe, sijui kama ataweza kufanya marekebisho kidogo, lakini nadhani kuna haja vile vile ya kuongeza ama hapa au pengine azimio jengine la kutaka serikali kupitia Wizara ya Habari,
Utamaduni, Utalii na Michezo, kusimamia vyombo vyetu vya habari viwe vya serikali au vya binafsi vizingatie maadili ya jamii yetu katika kutangaza vipindi vyake.

Matukio haya mengine Mheshimiwa, yanakuja kwa sababu mambo yaliyokuwa wanaonekana ni ya siri, mambo yaliyokuwa hayajazoeleka katika utamaduni wetu na sasa yanaonekana dhahiri.

Mimi nataka kutahadharisha jambo moja Mhe. Mwenyekiti, kuna watu walikuwa wakisema katika nchi hii kwamba huu utalii iko siku utageuka utakuwa utalia. Mimi sipingi utalii, naamini na naheshimu kwamba ni moja

katika sekta kubwa inayochangia uchumi wetu hivi sasa, lakini isiwe utalii holela. Leo Mhe. Mwenyekiti, katika jamii yetu tunashuhudia kwamba katika kuwafurahisha hao watalii, tunaandaa matamasha mbali mbali.

Niliwahi kusema nafikiri mwaka juzi katika kuchangia bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo ,kwamba moja katika kosa letu katika jamii yetu Mhe. Mwenyekiti, ni kuchukua suala la kusimamia utamaduni wa nchi na tukawaachia wageni, utamaduni roho ya jamii Mhe. Mwenyekiti, seuze jamii ambayo ina mizizi ya ustaarabu kama jamii ya Kizanzibari. Sasa leo sisi wenyewe hatulisimamii tumeacha matamasha ya kiutamaduni yote yanasimamiwa na wageni, takriban yote hata ukimuona Mzanzibari kawekwa pale kama ni Mwenyekiti, kawekwa ili kuhalalisha tu, lakini twende ukatizame bodi za matamasha haya.

Sasa wao kwa sababu wanachokitizama ni nini Mheshimiwa, ni kutafuta fedha basi, wala si kuitangaza Zanzibar ni *commercialization of the cultural aspect* ya jamii yetu. Sasa matokeo yake nini Mhe. Mwenyekiti, matokeo yake katika kutaka kuendelea kutafuta fedha mpaka mambo yaliyokuwa katika jamii zetu, yalikuwa ni siri wakiyajua wenyewe tu, sasa yanawekwa hadharani kwa kuoneshwa. Kuna vipindi Mhe. Mwenyekiti, kuna *documentaries*, kuna *DVD*, kuna matamasha yanafanywa mpaka mambo ya unyago ambayo kinamama walikuwa wakiyajua wao tu, sasa yanaoneshwa hadharani.

Sasa jamii ilipoweka mambo yale kwamba ni ya siri, ilikuwa ina sababu zake kwamba ni watu wa aina fulani tu ndio ambao wanapaswa kupata elimu ile, lakini ukiyaweka hadharani yanaondosha aibu na yanakwenda mpaka kwa watoto wetu Mhe. Mwenyekiti. Sasa watoto wakishaona mambo ya kawaida utazuiaje na mtoto ni mtoto, halafu anapoona mambo fulani anakwenda na anataka kujaribu sasa mambo ambayo anayaona.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nasema nilikuwa naomba katika hili azimio nambari 3 tuzingatie na vyombo vya habari na hasa Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, ione haja ya kusimamia utangazaji wa vipindi, lakini pia matamasha haya yasivuke mipaka katika kutaka kutumikia utalii ikawa tunauza utamaduni wetu na maadili yetu kwa sababu ya kutaka kufurahisha watalii. Naomba sana Mhe. Mwenyekiti, hilo moja.

La pili, Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Mhe. Mjumbe, kwa pendekezo lake la azimio nambari 4. Hili linasisitiza juu ya kuongeza mafunzo na kuongeza uratibu wa vyombo mbali mbali ambavyo vinahusika katika kusimamia sheria za kumlinda mtoto na mfumo wetu wa kisheria vile vile. Hapa nipongeze, mimi nadhani labda tukifanikiwa kulipata hili, basi yale

matatizo ya kupelekwa kesi nyingi zikaripotiwa, lakini baadae hukumu zikawa chache labda zitapata angalau unafuu na kupunguza uzito wa tatizo lenyewe. Kwa hivyo, nalipongeza na naomba serikali hili ilizingatie kwa umakini sana.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, napongeza sana pendekezo lake la azimio nambari 5 ambapo kataka suala la udhalilishaji watoto lipelekwe katika mitaala yetu skuli. Watoto tangu wanapoanza elimu yao waweze, kufundishwa kwamba haya ni mambo ambayo hayakubaliki na vile vile, inapokuwa kuna majaribio ya kutaka kuwadhalilisha basi wajue hii ni hatari kwao waweze kuyaripoti na pengine hata namna ya kukabiliana nayo na jamii zinafanya hivyo.

Karibuni kulitokea tatizo kubwa sana la ubakaji India, watu wakaingia mabarabarani kwamba kama ni kwetu hawaridhi na mfumo wa utoaji haki India katika kesi zinazohusu udhalilishaji wanawake. Na Jumuiya zisizo za kiserikali zikawa zimesimama mstari wa mbele ili kutaka Mahakama zijirekebishe. Kwa hivyo, ilikuwa nadhani ni muhimu na sisi tukiongeza uelewa huo katika skuli zetu na jamii ikapata mwamko kwa sababu mtoto tangu mdogo anapata kuelimishwa nafikiri tutapata uelewa mpana zaidi na itapelekea vyombo vijue kwamba jamii ina jukumu.

Mhe. Mwenyekiti, muda unakimbia naomba niunge mkono vile vile pendekezo lake nambari 7 kwamba serikali ifanye mapitio ikiwa sheria ya mtoto na sheria nyenginezo ili kuupa nguvu zaidi mfumo wetu wa usimamizi wa sheria, kama kuna mianya katika sheria zetu ambayo kutokana na maadili ya jamii yetu ilivyo,mambo mengine ni muhali inayopelekea kutopatikana hukumu, basi tuone vipi tunaweza tukarekebisha mfumo huo.

Lakini kubwa Mhe. Mwenyekiti, naomba liwe la mwisho katika mchango wangu ni azimio la 8 alilopendekeza Mhe. Mjumbe. Nimuunge mkono kabisa Mhe. Hamza Hassan Juma, kwamba tumeshachoka kusema katika Baraza hili na kuahidiwa na serikali kwamba itashughulikia suala la kupatikana kifaa cha *DNA,* tumechoka Mhe. Mwenyekiti.

Mimi kabla ya kuingia katika Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, kipindi cha mwanzo nilikuwa katika Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, wanakumbuka waliokuwa Wajumbe wenzangu katika kamati ile, katika kila majumuisho ya kazi za kamati tukisisitiza kwa Wizara ya Katiba, Sheria na Utawala, tunajua pengine sio inayopaswa kununua, lakini ishirikiane na wizara nyengine ikiwa ni Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto, ikiwa ni Wizara ya Afya kifaa cha *DNA* kipatikane.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hatua iliyofikia sasa kwa Zanzibar na hili si katika suala la udhalilishaji wa watoto tu, kuna na janga jengine katika nchi yetu suala la kesi za utumiaji wa dawa za kulevya zilizoongezeka. Pia, zinapata matatizo kumalizika na mara nyengine kupata hukumu zisizofaa kwa sababu hakuna kifaa cha *DNA*.

Sasa nasema serikali yetu ya awamu ya saba tunaiomba katika bajeti ya mwaka huu itafute popote itapokata, lakini katika bajeti liwemo fungu la kununua kifaa cha *DNA* na tumwambie kabisa Mhe. Waziri wa Fedha, kama hilo halitakuwemo basi bajeti yoyote moja tutaitoa kafara katika hili. Ikiwa inahusika na Wizara ya Afya kama ni katika masuala ya usimamizi wa haki Wizara ya Katiba na Sheria au kama ni udhalilishaji wa watoto Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto, yoyote katika hizo, lakini hatuwezi kuendelea kupokea ahadi. Tangu mimi naingia ndani ya Baraza hili, tunapokea ahadi za serikali kwamba kifaa cha *DNA* kitanunuliwa, lakini hatukioni.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana kwamba azimio hili tunalipitisha na mimi nawaomba wenzangu wote tulipitishe hili na mengine yoyote, lakini tuiambie na serikali kwamba utekelezaji wake tutaupima wa mapendekezo kutoka humu humu. Kwanza kwa kuona katika bajeti hii kifaa cha *DNA* kinanunuliwa katika mwaka huu wa fedha.

Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, niseme naiunga mkono hoja hii, nampongeza tena Mhe. Mgeni Hassan Juma na inaonekana haya majina ya Hassan Juma yana barka katika siku ya leo, maana mmoja mtoto wa Mzee Hassan Juma na Mhe. Hamza Hassan Juma, kaleta hoja binafsi kuhusu mswada, mwengine mtoto wa Mzee Hassan Juma, Mhe. Mgeni Hassan Juma, kaleta hoja ya udhalilishaji wa watoto, basi *inshaallah* na sisi tukizaa watoto tutawapa majina ya Hassan Juma ili wazae watoto wa kheri kama hawa. Mhe. Mwenyekiti. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsanteni sana Waheshimiwa Wajumbe kwa namna tulivyoshirikiana pamoja katika kupitisha hoja zetu zote mbili na hali ya kwamba hoja ya pili bado inaendelea na wakati tunaondoka hapa tuna idadi ya wachangiaji watatu. Mhe. Hija Hassan Hija, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk na Mhe. Suleiman Hemed Khamis.

Tunaomba na wale wengine ambao wanataka kuchangia jioni, wakifika hapa waendelee kutoa maombi yao ili waweze kuchangia. Hoja hii ni muhimu na inamgusa kila mmoja wetu. Baada ya maelekezo hayo sasa tunaakhirisha Baraza hili hadi sasa 11:00 jioni. Ahsanteni.

(Saa 7:00 Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)
(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, ninachukua fursa hii kukushukuru jioni hii kunipatia nafasi ya mwanzo kabisa ya kutoa mchango wangu juu ya hoja hii ya Mhe. Mgeni Hassan Juma. Hoja ambayo kwa kweli ni ya umuhimu kwetu na umuhimu kwa taifa letu.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijatoa mchango wangu naomba nikuombe binafsi kwamba kutokana na umuhimu wa hoja hii juu ya maslahi ya watoto wa Zanzibar, nikuombe ukubali kwamba tuendelee kuchangie hoja hii leo na ikiwezekana tuimalize kesho kwa majumuisho, ili kila mjumbe aweze kutoa mchango wake kwenye maslahi ya mtoto. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, kila mjumbe hapa ni mzazi na kila mzazi analazimika kuyatizama maslahi ya mtoto kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niingie kwenye mchango wa hoja hii ambayo Mhe. Mgeni ameileta leo. Nichukue nafasi hii binafsi kumpongeza Mhe. Mgeni kwa jinsi ya

ujasiri wake, naamini kwamba madhumuni ya Mhe. Mgeni ni kuendeleza mapambano na utetezi wa mtoto wa Zanzibar kama ambavyo taifa letu limedhamiria.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa kwanza wa Mhe. Mgeni amejaribu kutoa takwimu zinazoonesha jinsi ya kesi za ubakaji na udhalilishaji wa watoto zinavyoongezeka Zanzibar. Ameelezea mwaka 2012 kesi 72 zilifunguliwa na kesi 10 zilikuwa ni kinyume na maumbile wakati kesi 62 zilikuwa ni za ubakaji wa kawaida.

Mhe. Mwenyekiti, kesi 61 zimewahi kusikilizwa, kesi 11 zilitolewa maamuzi na kati ya hao, watuhumiwa wanne ndio waliotiwa hatiani. Mhe. Mwenyekiti, mwaka jana tulipokwenda kwenye kamati Pemba, mimi kabla ya kuacha Kamati ya Ustawi wa Jamii, tulishuhudia Chake Chake tu kwa kipindi cha miezi sita paliripotiwa kesi 78, kati ya hizo miezi sita yote basi kesi 2 ndizo zilizopelekwa Mahakamani na kesi 1 ndio iliyotolewa maamuzi.

Hatukuona ule wingi wa kesi ambazo zilipelekwa Polisi zilizofika Mahakamani, ni kesi 2 na kati ya hizo basi ilikuwa 1 tu ndio iliotolewa maamuzi. Sasa ikiwa miezi 6, kesi 78 zimekwenda kesi 2, maana yake kwa *speed* hiyo mwaka mmoja zitakwenda kesi 4. Jambo ambalo kwa kweli linaashiria kwamba ile dhamira ya serikali ya kulinda mtoto wa Zanzibar basi itakuwa ni vigumu kufikiwa.

Kwa hivyo, takwimu za kadhia hii za udhalilishaji wa watoto Mhe. Mwenyekiti, kadiri ambavyo utazitafuta basi zipo nyingi sana. Kuna wale ambao wanaripoti katika vituo vyetu vya *one stop centre*, Polisi, kwa Masheha na kuna wengi ambao wanaona aibu kuziripoti kesi hizi. Kwa hivyo, takwimu za kesi hizi hapa Zanzibar Mhe. Mwenyekiti, zipo nyingi sana na

lazima zifanyiwe maamuzi magumu kama ambavyo Mhe. Mgeni amependekeza.
Mhe. Mwenyekiti, sasa kwa msingi huo niungane na maoni ya Mhe. Mgeni ya kutoa maazimio katika Baraza la Wawakilishi ili tuiagize serikali kuwa na sauti moja katika kusimamia maslahi ya mtoto.
Sasa katika hilo Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mgeni ametoa mapendekezo ya maazimio tisa. Naomba nichangie baadhi yake na niongeze mengine matatu, Mhe. Mgeni aangalie kama kuna uwezekano wa kuyaongeza.
Mhe. Mwenyekiti, pendekezo la pili kwamba katika bajeti ya serikali ya mwaka 2014/2015, na bajeti zinazofuata, mkakati wa kupambana na utokomezaji wa udhalilishaji wa watoto uwe ni miongoni mwa vipaumbele vya serikali kwani hatua za kupambana na udhalilishaji wa watoto zinahitaji raslimali fedha ili ziweze kutekelezeka bila ya vikwazo. Baraza hili hili kupitia Afisi ya Baraza na kupitia wahisani wetu, mara kadhaa tumeambiwa kwamba bajeti nzuri ni ile bajeti inayozingatia maslahi ya mtoto.
Mwaka jana ukiangalia Mhe. Mwenyekiti, kwenye bajeti ya serikali ilitengwa asilimia 20 tu kwa maslahi ya mtoto. Sasa Mhe. Mgeni anakumbusha kwamba kuna haja ya kuangalia bajeti ya serikali vipi imezingatia maslahi ya mtoto. Na mimi niwaombe wenzangu Waheshimiwa Wawakilishi kwamba kutokana na wito huo wa Mhe. Mgeni, basi tukutane mapema kabla ya bajeti ijayo tukijaaliwa tuamue kwamba kipaumbele cha kwanza kwenye bajeti hii inayokuja ni maslahi ya mtoto.
Na katika wizara inayohusika Mhe. Mwenyekiti, kama jambo hili halikuzingatiwa angalau kwa asilimia 20 ya bajeti, basi niwashauri wenzangu kwamba bajeti hiyo tusikubali kuipitisha. Kwa sababu ni dhahiri kwamba wizara husika inayoshughulikia masuala ya mtoto imekuwa haifiki kwa walengwa kwa sababu ya uchache wa bajeti. Muelekeo wa dunia ni kwamba nchi nyingi huwa wanatenga bajeti kubwa kwa ajili ya maslahi ya mtoto, ninadhani Mhe. Mgeni anatukumbusha Kifungu Nam. 2 naq sisi tuelekee huko. Na mimi ninaungana naemkono kwa hilo.
Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ambalo limezungumzwa ni pendekezo la nne ambalo wenzangu wamezungumza suala zima la *co-ordination*. Mhe. Mwenyekiti, jambo hili la udhalilishaji watoto ni jambo ambalo linahusu taasisi zote. Ni vyema Mhe. Mwenyekiti, serikali ikawa na utaratibu mzuri kwa ajili ya kuweka *co-ordination* inayokubalika kwamba kila mmoja katika nchi hii ashiriki katika kupambana na udhalilishaji wa mtoto. Kwa hivyo, azimio hili Nam. 4 Mhe. Mwenyekiti, ni azimio ambalo pia ninalikubali na lazima Baraza litoe azimio hili ili kuweza kuwa na usahihi wa jambo hili.
Lakini azimio Nam. 5 Mhe. Mwenyekiti, la kuweka mtaala katika mambo ya elimu. Mimi Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Mhe. Mgeni kwamba ni kweli sera ya elimu imesema wazi kwamba sasa elimu ya lazima ni kuanzia elimu ya maandalizi. Watoto wetu unapowafundisha athari za ubakaji na nini

ubakaji katika hatua ya maandalizi Mhe. Mwenyekiti, ninadhani itakuwa taifa limejenga msingi madhubuti wa kuelimisha watoto wetu, kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, elimu ya utotoni ni sawa sawa na nakshi katika jiwe. Kwa hivyo, ninakubaliana nae Mhe. Mgeni ili wajue kwamba nani mbakaji na nini athari ya suala zima la ubakaji.

Mhe. Mwenyekiti, agizo au pendekezo Nam. 8 kupatikana kwa mashine ya *DNA*. Mhe. Mwenyekiti, niungane kabisa na Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwamba wizara husika kama ni afya, kama ni wizara ya Ustawi wa Jamii basi kipaumbele cha mwanzo kwa mwaka huu 2014/2015 kiwe ni upatikanaji wa mashine ya *DNA*.

Mhe. Mwenyekiti, ninajua serikali imekuwa ikisema mara nyingi kwamba *DNA* machine ni ghali, lakini kuna ughali gani kuliko ule ughali wa kupoteza maisha ya watoto wetu. Kupoteza hadhi ya taifa letu? Sasa Mhe. Mwenyekiti, niwaombe sana Waheshimiwa Wawakilishi kabisa kwamba wizara husika itapokuja mwaka 2014/2015, kama hakuna bajeti maalum kwa mashine ya *DNA*, basi bajeti hiyo ya wizara hiyo naomba irudi. Na hili jamani si tusi, si aibu, lazima kiwepo kipaumbele ambacho kinaonekana kwamba Wawakilishi wameamua kuwatetea watoto.

Mhe. Mwenyekiti, leo kesi nyingi haziendi, kesi za watoto, kesi za madawa ya kulevya na mambo mengine, hata kesi za jinai kwa sababu ya ukosefu wa kifaa cha *DNA*. Serikali uwezo wa kununua mashine hii wakiamua wanao na lazima tuamue kufanya suala hili kwa maslahi ya mtoto wetu.

Mhe. Mwenyekiti, mapendekezo yote 9 ya Mhe. Mgeni ninaunga mkono lakini naomba niyaongeze matatu na yeye mwenyewe kama mtoa hoja atayaangalia, kama inawezekana kuongezwa natuongeze, kama ataona hayana umuhimu basi nipo radhi kuyaachia.

Mhe. Mwenyekiti, ninadhani jambo jengine ambalo linalowavutia wahalifu hao wa ubakaji ni suala zima la utamaduni wa mavazi. Watoto wetu mara nyingi wamekuwa wakivaa mavazi ambayo yanavutia sana kwa watu wahalifu wa aina hii. Sasa niombe Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mgeni aangalie uwezekano wa kutoa azimio jengine juu ya uhuru wa mavazi hasa kwa watoto wetu uangaliwe upya. Tuweze kuwa na mfumo maalum kuwadhibiti watoto wetu katika mavazi. Tusiige utamaduni wa nje kwamba kila vazi anafaa kuvaa mtu yeyote.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo ningependekeza liwemo ni kwamba miaka ya tisini nakumbuka wabakaji wa mwanzo mwanzo wale walikuwa wakioneshwa hadharani na walikuwa na jina maalum "Kitangi". Kule kwetu jirani yangu mmoja alipata mtihani huo na alitembezwa siku mbili tatu kwamba ni Kitangi.

Sasa ninapendekeza kwamba tuangalie uwezekano wa kuongeza azimio hili kwamba anayekamatwa kwa wale sugu, kwa sababu wapo watu masugu katika jambo hili, ninapendekeza kwamba watembezwe na waoneshwe hadharani kwamba hawa ni vitangi. Badala ya kufichwa, kwa sababu

unapowaficha wanapambana na mkono wa kisheria, wanatafuta nyenzo za kujiokoa rushwa na mambo mengine, lakini wakiwekwa hadharani kwamba hawa ni vitangi sugu basi ninadhani taifa litawajua na litawakwepa.

Mhe. Mwenyekiti, ninajua kwamba itazungumzwa kuwa ni haki ya binadamu. Lakini kuna haki gani ya kulindwa ikiwa yeye anavunja haki za wenzake, anadhalilisha jamii, anasababisha ukimwi pengine, anasababisha ulemavu wa watoto. Nadhani kwa sababu yeye hakulinda haki ya binadamu mwenzake na yeye asilindwe kwa msingi wowote ule.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la tatu ambalo ninapendekeza, ninajua serikali wataliona baya, lakini limefika wakati, watoto wetu wamekuwa wakisababishiwa madhara mengi. Kuna wale ambao wanaosababishiwa athari za kimaumbile, ukimwi, uja uzito na kukosa masomo na hatimae kesi Mahakamani haziendi katika *speed* ya kuridhisha. Mhe. Mwenyekiti, mimi napendekeza kwamba wale ambao wamethibitishwa, serikali ikubali kuwahasi ili wakose haki moja ya msingi ya kujitawala katika maisha yao. Mhe. Mwenyekiti, nadhani hii itakuwa ni dawa moja ambayo kwa kweli itatusaidia.

Sasa baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, *unless* kuwe na utaratibu mwengine wa kisheria. Naunga mkono hoja hizi na mapendekezo yangu matatu ni hayo ambayo ninadhani Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mgeni angeyazingatia.

Ninakushukuru sana. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Hija Hassan Hija, kwa kuzingatia muda. Sasa ni nafasi ya Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, baadae Mhe. Suleiman Hemed Khamis.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwanza nimpongeze Mhe. Mgeni kwa kuliona hili na kwa uchungu kuona watoto wetu wanadhalilishwa kiasi kikubwa sana na wanawapotezea maadili yao ya huko mbele.

(Sauti ya mlio wa simu ilikuwa ikilia na kuleta usumbufu)

Mhe. Mwenyekiti, sijui simu ya nani hiyo na spika zetu zinaingiliana ingiliana.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli ni suala ambalo hoja hii kwa kweli imekuja wakati ndio. Mimi nina mambo mawili mpaka matatu.

La kwanza, amenifilisi mheshimiwa wangu, Mhe. Hija Hassan Hija, na mimi nilikuwa na agenda kama hiyo lakini nitaitilia mkazo kwa aina yake. Mhe. Mwenyekiti, leo asubuhi hapa Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo alikuwa anatuhadithia jinsi gani wanyama wanavyotaka kupunguzwa kasi na akaeleza wazi jinsi ambavyo wanavyowafanya.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa serikali imeweka agenda kama hizo za wale wanyama ili wasiwe wengi, basi wahasiwe. Je, hawa watu wanaofanya vitendo kama hivyo. Kwa nini na hawa wasiwekewe *special* sheria hiyo wakapelekwa huko kunako mifugo nao wakenda kuhasiwa.

Mhe. Mwenyekiti, siku moja mimi nilikwenda hospitali. Nilikuwa nimempeleka mgonjwa pale katika matibabu ya kutiwa *POP*, lakini kwa bahati nzuri nikakutana na kijana mmoja tukawa tunasalimiana, eeh! bwana vipi, akasema nimekuja hapa kuja kufanya uchunguzi watoto wamebakwa.
Mhe. Mwenyekiti, nilitokwa na machozi, watoto wadogo wa kiume. Lakusikitisha ni watoto wa kiume wa kutegemea, mtu anakwenda kuwaharibu watoto kama wale anakusudia nini? Mhe. Mwenyekiti, hapa serikali isiwe na huruma, kweli kuna mambo mengi ya haki za binadamu lakini na hawa wana haki zao.
Tusiwaregezee Mhe. Mwenyekiti, leo hapa dada yangu Mhe. Mgeni anasema kuna kesi chungu nzima za kulawitiwa zimeletwa hapa. Zinapanda siku hadi siku, hatupo *serious* mimi ninasema siku zote. Tunatunga sheria lakini inakaa kwenye *table*, ufuatiliaji wake ni mdogo sana, sheria haiondoki, usimamizi ndio unaotakiwa wa sheria.
Mbona kwenye ulinzi wa karafuu tunakuwa tupo serious kabisa. Thubutu leo karafuu utoke nayo hapa nchini uone. Lakini vitoto vyetu vinaingiliwa, vinafanyiwa mambo maovu, tunaachia tu hivi hivi.
Mimi ninaamini kila mzazi akisimama na akichangia anatokwa na machozi ya ndani, kama kasa anavyocheza, kwa sababu ni aibu leo kutoka machozi, hata mimi leo ninatokwa na machozi lakini ndio nitafanya nini, watu wote wataona Mshimba huyo analia sasa hivi, lakini huwezi kujua ndani ya nafasi yangu ninalia. Mimi nina watoto si chini ya saba na mwenzangu ana wengine kuliko hao, kama sikumuhurumia mwenzangu. Haiwezekani Mhe. Mwenyekiti.
Nigeuke upande wa pili. Mhe. Mwenyekiti, wazee wasiwatume watoto biashara ndogo ndogo. Mhe. Mwenyekiti, *wallahi* Mwenyezi Mungu anajua, kila siku mimi ninawakuta watoto wanauza zile mboga ndogo ndogo, wanatokea sehemu za jeshini huku, Mpendae. Mimi ni miongoni mwa wanaonunua, thamani yake ni shilingi elfu tatu na mia tano, ninanunua kwa uchungu, usifikirie ninanunua kwa utajiri, hapana au ninanunua kwa kutaka kwenda kula, hapana, ninamfikiria kwamba yule ni mtoto mdogo.
Pale pengine mzazi kishamkatisha maisha yake ya skuli, mzazi kajiona ni *beautiful girl* hawezi kutembeza biashara ile, anawadhalilisha watoto na hawa Mhe. Mwenyekiti, hawa wazee wakamatwe, kwani hawa ndio chanzo.
Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli inasikitisha sana. Karibuni hivi kule Kiwengwa kulitokea tatizo hilo, mtoto ni mdogo sana wa kiume, kakutwa anatoka mwituni mtwana limekimbia, na sijui mpaka leo kesi ile ikoje. Ninakuja kupewa habari ile, basi ninasema kama ningekuwa na bastola ningemua, sisemi uwongo, hasidi, maana yule mtoto kishamuawa, tena mimi nimwachie nini, anayeuwa na yeye auliwe, na mimi nikasema potelea mbali. Halafu leo tunaambiwa tuna Jeshi la Polisi!
Mimi ninaomba Mhe. Mwenyekiti, Jeshi la Polisi likapelekwe Marekani jinsi gani ya watu wanavyochunguza kesi hadi kukamilika kwake. Ninamuomba sana Kamishna huyo aliyekuwepo hivi sasa Mhe.Mwenyekiti, Jeshi letu la

Polisi liende likapate *training* mafunzo ambayo ya kuweza kuchunguza *in time* ya kuweza kumtia mtu mashakani, sio leo uone picha tu, useme huyu mtu anaingia hatiani, haiwezekani Mhe. Mwenyekiti, inauma.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, wallahi hili suala linasikitisha sana na ninaomba sana vyombo vya sheria, ushauri wangu mara nyingi sana watu wanaona hili jamaa halikusoma, lakini Mwenyezi Mungu ananijaalia ushauri wangu unakuwa ni mzito sana na una mantiki sana.

Ushauri wangu ninaomba sana Waziri wa Sheria, Mwanasheria Mkuu, Muendesha Mashtaka, Kamishna wa Polisi, vyombo hivi kama havijakaa pamoja basi hakuna utendaji wa kasi. Naomba kila baada ya *one week* wakae wabadilishane mawazo kutafuta mbinu mbadala. Lakini si vibaya hata kidogo wakanihusisha na mimi, tena sitaki nilipwe, nipo *free* mimi, ili kuwasaidia maarifa hili suala tuliondoe, lakini kwa njia nyengine yoyote haiwezekani.

Ushauri wa pili twende katika sheria zetu hizi. Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa tuna Polisi Jamii lakini Polisi wetu jamii niseme kuwa bado serikali hapa, haijatoa support kubwa sana na njia ni rahisi sana kuondoa matatizo haya. Wapewe mafunzo kupitia Ofisi hii ya Makamu wa Pili wa Rais itenge *special fund* kuwapelekea hawa Polisi Jamii kwa ajili ya mafunzo. Wanasaidia sana.

Lakini, mkuu huyu wa sasa naamini atakuwa active kabisa katika masuala ya Polisi ya Jamii. Tutaondokana na ubakaji. Ninaomba hilo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, pia ninataka kutoa tahadhari, hawa wabakaji ni mahodari niseme wana *experience* na wana akili kubwa sana. Siku moja nilikuwepo pale hospitali kwa bahati nzuri kuna kitoto kidogo cha kike, maana yake ukimuona mtoto huyo Mhe. Mwenyekiti, ukiambiwa kama ni mwanamme utakubali lakini ukiambiwa ni mwanamke utakataa, kwa sababu halioneshi lile umbile lake kama huyu ni mwanamke kuwa katimilia.

Lakini uchunguzi unaambiwa anambeba mtu! Haki ya Mungu, kitoto kidogo kabisa. Huyo mtoto tulimtisha, akatishiwa kupigwa. Lakini *Wallah* kala yamini yule mtoto, kashindwa kusema, alivyokuwa kapewa mafunzo na matisho makubwa sana. Lakini mwisho wa habari kafundishwa amseme rafiki yake yule jamaa mtendaji. Inavyoonesha alimuona yule mtoto na akaoneshwa kuwa huyu ni rafiki yangu, ikitokezea kukamatwa basi mtaje huyu na mtoto akafanya vile vile.

Mhe. Mwenyekiti, yamekwenda yale matatizo, bahati nzuri kuna polisi anajua kucheza na yale mambo basi akafanya mambo yake. Ilibidi pale yule polisi atokwe huruma kabisa, kumbe yule jamaa tunamuangamiza wala siye maskini ya Mungu. Mtoto yule akaja akataja fulani. Huyo jamaa Mhe. Mwenyekiti, hafai! Halafu leo mtu huyo usimuasi! Hatari kwenye jamii anagombanisha na jamii nyengine. Huyo jamaa maskini ya Mungu alilia vibaya sana. Alizuiliwa yule jamaa na watu 20 asiende kuuwa kwa tendo alilomzushia.

Sasa na wewe utahadhari hiyo, hawa ni walimu wa walimu kwa sababu ni mahodari wa kuwa-*treat* wale watoto. Sasa na hili naomba tulione ndio maana

nikasema kuwa, hapa tuwe na elimu, askari wawe na elimu kubwa sana, tusione tabu serikali kutoa mafungu ya fedha kuwapeleka askari wetu wakaenda kufundishwa njia au mbinu kama hizo. Lakini kama si hivyo tutakuja kumalizika hapa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia nitoe ushahidi hai. Siku moja kama saa 5:00 za usiku nilipigiwa simu mimi, mheshimiwa njoo kuna janga kubwa sana huku. Kwa bahati nzuri mimi nikatoka na ndugu yangu mmoja tukachukua mapanga mawili. Tulipofika kule sheha akaniambia tumewaita polisi tangu jioni hawajaja. Mimi nikaenda kuwachukua polisi katika kigari changu kidogo, nikawatia na wao wakawa na *sub machinegun*, wawili hao na sisi tukawa wanne.

Mhe. Mwenyekiti, siku hiyo nilijipongeza mwenyewe. Tukaizunguka ile nyumba, Mhe. Mwenyekiti kusema ni aibu, lakini sitoona aibu. Kitoto kidogo maskini ya Mungu, jamaa kenda kakipachika mbegu, niseme sijui wa miezi miwili yule. Kitoto kidogo sana aah!

Mhe. Mwenyekiti, ile nyumba tuliizunguka. Basi Mwenyezi Mungu alinio tesha ndoto akaniambia hebu kaa hapo, mimi nilikaa kama hapa pembeni sikuwa na matumaini kama atapenya yule mtwana pale. Mhe. Mwenyekiti, mimi ni mwanamichezo sana, lakini nashukuru u-*goalkeeper* sikuwahi kukaa. Basi alikuja kupenya pale nilipo Mhe. Mwenyekiti, nilijikunjua nikamrukia kama *goalkeeper*, nilimbana piiip! Tukabiringishana huku napiga kelele, huyu huku ninaye na mtwana sio mdogo Mhe. Mwenyekiti, sio mchezo lakini ninaye, ujasiri ulivyonipa.

Nikakumbuka enzi zangu nilivyokuwa mtundu, nilimtia kabari tukabiringishana kwenye miwa mpaka askari wakaja mbio na ndugu yangu yule akaja mbio. Tukamtia pingu, tukaondoka nae. Mhe. Mwenyekiti, basi tukenda zetu hospitali.

Namalizia Mhe. Mwenyekiti, zimebakia kama dakika mbili.

Basi kufika kule hospitali tukaambiwa kuwa hajaingiliwa, lakini kapewa ishara iliyokuwa siyo, basi ile kesi ilivyokwenda mpaka leo siijui. Vitu vya ushahidi vya kutosha vilikuwepo. Sijui ni ushahidi gani tuliokuwa tunautaka, ammalize yule amuuwe kabisa au kitu gani. Mhe. Mwenyekiti, wataalamu watanisaidia na Mwanasheria, sijui hapa tulikuwa tunataka nini.

Mhe. Mwenyekiti, namalizia hapa. Mimi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Kitope tumekasirika sana kuhusu suala hili. Hivi sasa wananisikia na tutaweka ulinzi mkali kabisa, isiwe kwamba watu wengine wanafanya vituko

vyao, halafu wanasingizia majimbo mengine. Mhe. Mwenyekiti, hili linafanyika na hizi ndio mbinu za sasa hivi za hatari. Mhe. Mwenyekiti suala hili tunawaomba wahusika wawe waangalifu sana ili kuweza kujua sheria.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa unanitizama, naomba kumalizia hapa naunga mkono kwa asilimia mia kwa mia, ahsante sana. (*Makofi)*

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nachukua nafasi hii kukushukuru wewe kwa jioni hii kuweza kunipatia nafasi ya kuweza kutoa mchango wangu katika mada inayozungumziwa.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kuanza hiyo mada ambayo inahusika, kwanza nataka nizungumze hoja ambayo ilianza asubuhi ambayo ni hoja binafsi ya kumpongeza Mhe. Hamza Hassan Juma, ambapo mjumbe huyu alileta hoja binafsi.

Mhe. Mwenyekiti, hii ni kuonesha jinsi gani Baraza lilivyopevuka na kuwa na uelewa mzuri, kielimu na kisiasa na kuweza kujitegemea zaidi kwa kuleta miswada yenye hoja binafasi. Mhe. Mwenyekiti, nia na madhumuni ya hoja ya Mhe. Hamza Hassan Juma ilikuwa ni nzuri, tumefahamu vya kutosha kuwa Baraza kama muhimili, basi liweze kujitegemea lenyewe. Baraza liwe na mfuko wake kwa shughuli zake zote bila kuingiliwa na taasisi nyengine. Hiyo ndio dhamira ya mswada huo na ni muhimu sana kwa sababu Baraza lina mipango mingi na linataka kusimamia utekelezaji wa shughuli zake za umma. Tunakushukuru sana Mhe. Hamza Hassan Juma.

Vile vile, nichukuwe nafasi hii kumshukuru Mhe. Mgeni Hassan Juma na yeye kwa kuleta mswada wake, ambapo yeye ametoa hoja yake ya kuliomba Baraza juu ya maazimio dhidi ya vitendo vya udhalilishaji wa watoto Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, hapana shaka serikali imeonesha dhamira yake ya kuwalinda watoto wote chini ya sheria nambari 6 ya mwaka 2011. Sheria hii ni kwa ajili ya watoto kupata haki zao kamili, ikiwemo elimu, makaazi, mavazi, chakula na
kuwalinda na udhalilishaji. Mhe. Mwenyekiti, pia tunaamini sote kwamba Zanzibar imeridhia mikataba ya dunia chini ya mwamvuli wa Jamhuri ya Muungano kulinda haki za watoto.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na jitihada za serikali za kulinda na kupunguza udhalilishaji wa watoto wa jinsia zote zinavyoendelea hapa Zanzibar, Mhe. Mwenyekiti, tunasikitika sana kwamba hivisasa Zanzibar imebadilika na takwimu zinaonesha kuwa vitendo vya udhalilishaji vinazidi kupamba moto,

hasa kwa watoto wetu wadogo. Hapa inaonesha kuwa kesi zilizokwenda mahakamani mwaka 2011 ni kesi 74. Kati ya hizo, kesi 56 za ubakaji na kesi 18 ni zile ambazo zimefanywa kinyume na maumbile ya mwanadamu. Zote hizo ni udhalilishaji. Lakini kama zingeanza mwaka 2008, 2009, 2010 bila shaka takwimu hizi zingeonesha jinsi ya hali ilivyokuwa ni mbaya zaidi na siku hadi siku takwimu zinazidi kwenda juu.

Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa kesi hizi ambazo zimeendeshwa, nyingi katika kesi hizi hazikuweza kwenda sawa sawa kwa sababu ya ushahidi. Wazee wengi wanashindwa kutoa ushahidi ili kuthibitisha kesi hizi. Kwa hivyo, tunaomba wazazi, walezi na sisi sote kwa jumla, mambo haya tusiyafungie macho, kwa sababu hii ni hasara kwa taifa letu.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, sisi ni Wawakilishi wa wananchi na viongozi mbali mbali tuna dhima juu ya suala hili, kwa sababu tutakwenda kuulizwa tumekabidhiwa nchi safi na lazima tupate watu safi. Hii inaonesha kuwa maadili ya nchi yameanza kuporomoka. Tumesahau tulikotoka kwenye tabia nzuri, khulka safi, mila zetu na utamaduni wetu wa Kizanzibari, na tumeingia katika masuala ya watu wengine. Kwa sababu sasa hivi dunia iko huru, watu wana nafasi ya kutembea katika nchi mbali mbali, wanaona mambo huko wanakuja nayo hapa. Kwa hivyo, sisi hatutokubali kuona watoto wanadhalilishwa ambao hawana hatia yoyote.

Zanzibar ni nchi ya Kiislamu, itakuwaje sisi Wazanzibari tushabikie mambo ya watu wa nje ambapo sisi sio tabia zetu wala hayatuhusu, sisi ni Waislamu asilimia mia kwa mia.

Watu wameingia katika mabadiliko ya kiteknolojia za kisasa ambazo pia zinatupa hatari kubwa kwa watoto wetu. Hizi *TV* zetu, makompyuta tuliyokuwanayo, ma-*internet* pamoja na simu. Ni mzee gani hivi sasa anayeweza kumzuwia mtoto mwanamke asitumie simu.

Aliyekuwa waziri wa elimu Mhe. Haroun Ali Suleiman, alifanya kila jitihada kwamba watoto wa skuli wasiwe na simu, hizi simu ni moja ya chanzo cha kuwaharibu watoto. Kwa sababu wanaanza ku-*chart* kabla wakati haujafika.

Vile vile, Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme pamoja na sisi viongozi kutilia mkazo kwenye suala hili, pia nataka niwapongeze masheikh wetu wa Zanzibar ambao wanafanya bidii ya kutuelimisha kila siku. Tujifahamu kwamba sisi ni Waislamu, tunatakiwa tusiziharamishe ndoa zetu, ili watoto wetu waje safi. Kila wakati wanasema kuwa suala hili limejitokeza kwa nguvu. Hata hivyo, masheikh washaanza kujinasua, wanautupa mzigo huu

kwa serikali na vyombo vyake vya dola kwamba ichukuwe kila hatua ya kuona udhibiti wa watoto wetu uko wa hali ya juu.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na hali ya ubakaji vijana wetu wengi wa kike wamechukua mimba za utotoni. Mimi nasema naomba sheria ichukuwe mkondo wake. Mtu akibaka watoto 10, 20 afungwe miaka 30, awekwe jela, abakie huko huko ndani asitoke tena nje.

Pia, Mhe. Mwenyekiti, tunaiomba serikali iangalie familia ambazo zina hali ngumu za kimaisha. Wapewe miradi ya kujiendesha. Ndio maana baadhi ya wazazi wanawafanyisha watoto wao kazi mbali mbali nje kwa ajili ya kwenda kutafuta riziki, watoto wadogo wadogo. Hata katika Qur-ani inasema wapo *masaakini wal fukaraa*, yaani wapo mskini na mafukara ndio tunavyoambiwa.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi unaambiwa hapa mjini si kuna *saloon* za wanawake, pia kuna *saloon* za vijana wanaume wanaokwenda wakipodolewa huko, hii hali itakuwa vipi jamani, na huko kupitiwe kwenye ma-*saloon* hayo ya watoto wakiume. Jamani tutakuwa na jamii ya aina gani.

Mhe. Mwenyekiti, tunataka serikali iweze kuchukua hatua ya kuona kuwa tunaleta mabadiliko. Watoto wetu ,vijana ndio wanaowaharibu takriban, vijana wengi ndio wanaopewa dhamana ya kukaa na watoto, hawa ndio mara nyingi wanawaharibu watoto. Hata katika vyuo, imeshatokezea sana wanaopewa dhamana ya kusomesha *Qur-an* wameshawaharibu watoto.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe malizia hapo.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Ahsante. Mzigo huu ni wetu pamoja Baraza la Wawakilishi, viongozi waliopo juu katika serikali, wananchi kwa jumla, vijana ni waharibifu.

Halafu Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiri sio mbaya kupata *facilities*, lakini hizi fursa tunazozipata ndani ya nchi yetu, madisko haya na mambo kadhaa yaliomo mule ndani, pia yanawaharibu watoto, yanahitaji kuchunguzwa.

Mhe. Mwenyekiti, kule Bara kuna watoto wanawake ambao wako Chuo Kikuu, wanakamatwa saa 8:00 za usiku katika madisko wanakwenda kufanya nini? Tena hao wanafunzi wa Chuo Kikuu, nini matokeo yake baadae. Kwa hivyo, hii ni hali ya kuizuia, kwa sababu wale waliokuwepo kule wote ni watoto wa kike na wengine ni wake za watu.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana na mimi naunga mkono hoja ya Mhe. Mgeni Hassan Juma. Nakushukuru, ahsante sana.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi kuweza kuchangia hoja hii ya Mhe. Mgeni Hassan Juma, hoja ambayo inazungumzia kuhusu udhalilishaji wa watoto.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuanzia naomba nimpongeze Mhe. Mgeni Hassan kwa kuona kuwa sasa *enough is enough* na sasa kama Baraza tuvunje ukimpya na kuleta hoja hii ili kuona kuwa Baraza linatoa maazimio juu ya kadhia hii ambayo imeshamiri katika jamii yetu.

Mhe. Mwenyekiti, hata ukiangalia *trend* ya kesi zenyewe ambazo Mhe. Mgeni Hassan Juma, ametoa hapa katika hoja yake, basi utaona kuwa hili tatizo ni kubwa na kwa kweli sasa imefika wakati serikali na jamii kwa ujumla ione kwamba tunafika mwisho wa tatizo hili.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa takwimu za Mhe. Mjumbe mtoa hoja, mwaka 2010 zimeripotiwa kesi 48, 2011 kesi 74, 2012 kesi 72 na 2013 naamini kwamba idadi itaongezeka kutokana na vitendo hivi sasa ni vimeshamiri. Mhe. Mwenyekiti, ukijumlisha kesi hizo zote ni kesi 194 kwa muda wa miaka 3 tu, na hizo ni ambazo zimeripotiwa, zipo zinazoishia juu kwa juu ambazo naamini ni nyingi sana kuliko hata hizi zinazoripotiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuanzia nataka nianze na jamii yenyewe, huku ndiko hasa vitendo vyenyewe vinakofanyika, kwani sisi wenyewe katika jamii tuna matatizo, kwa kuwa haya mambo mara nyingi hufanywa na watu wa karibu kama si baba mdogo, mjomba, baba mlezi, jirani au baba mzazi. Wewe kama hao tatizo linapotokea familia inachukua muda sana kuripoti kesi hizi, mpaka kwanza kikao cha familia kikae kijadili, tupelekeni kesi au tusipelekeni. Wakati yanapofikia maamuzi ya kuamua kwamba walete hizi kesi, tayari inakuwa *too late*.

Mhe. Mwenyekiti, pia wapo wanaowahi kuleta hizi kesi lakini inapita muda kesi imeshapelekwa ipo katika hatua ya kusikilizwa, unasikia upande mmoja wa familia umetoka unakwenda kwa Mkurugenzi wa Mashtaka au Polisi wanakwenda kusema sisi familia tumefikia suluhu kwamba hii kesi tunaomba ifutwe, tumeshakubaliana na aliyefanya hichi kitendo ameshamlipa mtoto. Sasa mtoto amelipwa lakini ule utu wake uko wapi?

Mhe, Mwenyekiti, kutokana na hayo naunga mkono sana azimio namba 3 la Mhe. Mgeni kutaka miongoni mwa majukumu ya msingi ya mikakati ya kupambana na kutokomeza udhalilishaji wa watoto, yazingatie utoaji wa taaluma kwa jamii, tena itolewe hasa. Jamii watambue kwamba kile kitendo ni kibaya na hakuna haja ya kumficha yule mfanyaji hata kama ni baba wa mtoto. Ni lazima afikishwe katika sehemu husika, ili ile haki ya mtoto ionekane kwamba inapatikana.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine naungana na Wajumbe walioanza kusema ipo haja sasa kwa serikali kuona kwamba hichi kifaa cha *DNA*, pamoja na kwamba tuna *One Stop Centre*, lakini kifaa cha *DNA* ni muhimu sana katika kuthibitisha hizi kesi. Msingi wa Mashtaka ya jinai ni ku-*prove* yule mshtakiwa kafanya kile kitu. Sote tunajua usiri wa mambo haya yanavyofanyika kwa kweli inakuwa ni yule mfanywaji na mfanyaji, hakuna mwengine yeyote anayehusika.

Sasa inakuwa vigumu ku-*prove* hizi kesi kwamba huyu ndiye aliyefanya kama Hamza au Hija ndiye aliyefanya, lakini hii mashine ikipatikana moja kwa moja itaonesha kwamba huyu mfanyaji ndiye huyu au siye ni huyu. Mimi naona kuna umuhimu sana, naungana na Wajumbe waliopita kwamba ipo haja ya bajeti inayokuja kama haitokuja na kipaumbele hichi ipo haja ya kuitoa kafara kama Mhe. Ismail Jusssa Ladhu alivyosema. Aidha bajeti ya Wizara ya Afya ama Wanawake na Watoto au mfuko Mkuu wenyewe Wizara ya Fedha, kuona kwamba hichi kifaa kinapatikana.

Mhe. Mwenyekiti, wapo wanaosema kwamba kipo ghali hichi kifaa, lakini mimi naamini meli ni ghali zaidi kuliko hichi kifaa na zilichangwa pesa hapa na zikapatikana na tukaambiwa meli ipo katika *process*. Tuone kwamba hichi kifaa kinapatikana ili wale wanaofanya haya matendo watiwe hatiani. Mhe. Hamza Hassan Juma, alisema hapa mtoto anapelekwa anakwenda kama kaa. Mimi namwambia hata aende kama gari bovu, lakini kama hakuna ushahidi Mhe. Mwenyekiti, yule mtu kumtia katika hatia ni ngumu. Njia pekee ambayo tunaweza kumtia huyu mtu katika hatia ni kuwa na kifaa cha *DNA*. Naomba serikali ione kwamba jinsi gani hichi kifaa ni muhimu.

Naunga mkono pia azimia Nam. 8 la Mhe. Mgeni Hassan Juma, katika kurahisisha huu upelelezi wa kesi za udhalilishaji wa watoto serikali ihakikishe ndani ya kipindi kifupi kijacho, mashine ya uchunguzi wa vinasaba inapatikana hapa Zanzibar, ili kuona watoto nao wanapata haki zao ambazo wanastahiki.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo tunalo hapa katika matatizo ambayo tunayapata katika upelelezi ni maumbile ya ushahidi. Hii inatokana na sheria yenyewe ya ushahidi ambapo inasema *competent* ya kutoa ushahidi ni mtu awe mtu mzima na mwenye akili timamu. Sasa hapa tuna *deal* na watoto na masikini ya Mungu watoto wengine wanakuwa *very bright*, yule aliyefanya kile kitu anamjua kama ni Hamza anasema ni Hamza hasemi hata siku moja Mshimba. Kwa maana hiyo Mhe. Mwenyekiti, tunaona jinsi gani sheria zinabana hawa watoto. Kwa hiyo, pia naunga mkono lile azimio Nam 7 la Mhe. Mgeni Hassan Juma, alilosema kwamba sasa ipo haja ya sheria hizi kufanyiwa marekebisho pamoja na sheria ya mtoto na sheria nyengine ambazo zinahusu haki ya mtoto kupatikana.

Mhe. Mwenyekiti, kitu chengine, siku hizi udhalilishaji uko wa aina nyingi, sio lazima mtoto abakwe tu. Tumeshuhudia sisi sote hapa watoto wadogo wanatandazwa kwenye *internet* pengine kama Mheshimiwa mmoja

alivyosema kadanganywa kwa pesa mbili tatu au chipsi kuku, anakubali anapigwa picha anaanza kusambazwa katika mitandao. Hii Mhe. Mwenyekiti, *Evidence Act* tunayotumia ni ya mwaka 1917. Kwa hiyo, hai- *cove* mambo kama haya ya *cyber crime* na mambo mengine.Kwa hiyo, inakuwa shida saa nyengine. Nalo hili pia linasababisha kwamba watoto wanakosa haki zao.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine tunajua kwamba sheria zipo lakini haya mambo bado yanaendelea kushamiri. Mimi nafikiri adhabu hazitoshelezi ni kidogo kwa hawa watu pengine sheria zitakapofanyiwa marakebisho, iangaliwe kwamba labda mtu aondolewe dhamana ajue kwamba miye nikifanya hichi nakwenda kule sina dhamana nakwenda moja kwa moja jela. Kwa maana hiyo nayo sheria watu wa *ages chamber*, waangalie kwamba hizi sheria wanazotunga zinazohusiana na mambo haya kuwe kuna adhabu kali ambazo zinawekwa juu ya hawa watu.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ni rushwa. Rushwa imetawala sana, polisi, Mahkama kwa kweli rushwa inakosesha haki watoto. Mimi naomba hasa kwa pande zote mbili polisi na Mahkama tunasikia kuna kesi, polisi anachomoa *PF3*. Kuna mama mmoja mtoto wake kabakwa, kenda polisi, daktari kaangalia kwamba kweli mtoto kaharibiwa, jalada limepelekwa polisi la uthibitisho kwamba mtoto kapata *penetration*, lakini polisi wamechomoa *PF3* ile wameweka nyengine ya daktari ambayo inasema mtoto yule hajabakwa.

Mhe. Mwenyekiti, Mungu kubariki yule mama wa mtoto ilimjia akili wakati anatoka hospitali na ile fomu aliitoa *copy* njiani. Akawa nayo ile *copy* kwamba yule mtoto ameharibiwa. Jalada limekwenda kwa *DPP*, *DPP* kapelekewa na ile fomu ya *PF3* ambayo polisi wamei-*fix*. *DPP* kafunga jalada kwa sababu dokta anasema mtoto hakuna *penetration* iliyofanywa, kafunga jalada kesi imekwisha. Mama mtu kaenda kwa *DPP* na fomu mkononi analia kwamba fomu ya dokta hii hapa mtoto ni kweli kathibitishwa. Sasa nafikiri kesi inaendelea. Kwa hiyo, tuone jinsi gani polisi walivyokuwa wapo *corrupt*. Kwa hiyo, mimi sishangai hata upanga wao kuibiwa, kwa sababu mwisho wataibiwa hata na wao wenyewe.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka kuzungumzia kuhusu *capacity building* ya hawa wanaoendesha hizi kesi za watoto; kwa wapelelezi, waendesha mashtaka, mahakimu na majaji pia. Ni muhimu wakapatiwa mafunzo yanayoendana na kesi ambazo wanaziendesha. Leo hii waendesha mashtaka wanatupiwa mzigo wa kila kitu, bangi wao, madawa, wizi, watoto, hivi kweli watakuwa na muda wa kuwashughulikia watoto, huku ana kesi kibao za wizi na mabangi na madawa hayo yaliyoenea. Mimi naona ipo haja ya kuwajenga hawa wanaoshughulikia haya mambo waka-*specialize* kabisa katika hizi *issue* za kuwapatia haki watoto.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo mimi naunga mkono hoja ya Mhe. Mgeni Hassan Juma, na naomba Wajumbe wengine wajadili hasa wanawake kwa sababu sisi ndio wazazi, sisi ndio tunaumia, sisi ndio tunaoingia *labour* kule tukaumia. Kwa hiyo, mimi sioni haja Mjumbe mwanamke hapa kukaa

kitako akaacha tu hii hoja inapita hivi hivi bila ya kuchangia. Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi na naunga mkono hoja.

Mhe. Marina Joel Thomas: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi hii kuchangia hoja ya Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, kuliomba Baraza la Wawakilishi la Zanzibar kutoa maazimio dhidi ya vitendo vya udhalilishaji wa watoto na wanawake Zanzibar. Pia, nampongeza Mhe. Mgeni Hassan Juma, kwa kutoa hoja hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, tafiti mbali mbali zimefanyika na asasi za kiraia *NGOs*, polisi na sehemu nyengine mbali mbali. Na kuna kesi nyengine zinamalizwa katika ngazi za familia bila ya kupelekwa katika vyombo husika kwa kuona aibu na fedheha. Lakini taarifa ya mtoa hoja Mhe. Mgeni Hassan Juma, imetueleza takwimu kuanzia mwaka 2010 hadi 2012 kwamba alitueleza:

Mwaka	**Kesi**
2010	48
2011	74
2012	72
Jumla	**194**

Mhe. Mwenyekiti, hatujui mwaka 2013 pengine zipo zaidi ya hizo. Hii hali inatisha ni hatari. Kubwa ni kuiomba serikali ichukue hatua zaidi kuhusu vitendo hivi vya udhalilishaji wa watoto.

Mhe. Mwenyekiti, wanaofanya vitendo hivi ni miongoni mwa jamii yetu wakiwemo baba zetu, wajomba, kaka na majirani. Mara nyingi wazazi wanashindwa kuripoti kutokana na aibu na fedheha ambazo zinawapata. Lakini tumuangalie mtoto ambaye ameathirika tusiangalie aibu na fedheha na hili hasa nasisitiza kwa upande wa wazazi. Mtoto yule anakuwa keshamuharibu kisaikolojia, *future* yake ya maisha imeshaharibika. Kubwa kwetu sisi kwa upande wa wazazi kuyafichua maovu, tusiyafiche.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitatoa mfano mdogo tu. Nilikuwa nina mwanangu wa miaka 8, siku moja nikamtuma mafuta ya taa, nikampa chupa akaenda, sasa nikaona kakawia, nikatoka nje pale nikasimama. Nikamuona kuna jamaa na baiskeli yake anazunguka zunguka mbele ya geti la mlango pale. Dakika namuona yule jamaa kaondoka, sasa namuona yule mwanangu anakuja mbio kajaza mawe mifukoni. Nikamuuliza mbona umechelewa. Akanambia mama umemuona yule babu ana baiskeli kanita ananambia njoo wee mtoto nikupakie twende, akanambia lakini mimi nimekusudia nimpige haya mawe, ningempiga kweli kweli!

Sasa na mimi nilikuwa namwambia kwamba ukienda nje au pahali popote ukiitwa na mtu ambaye humjui akikwambia njoo unipeleke mahali fulani au njoo nikuulize usiende. Sasa tunapaswa na sisi wazazi tuwaelimishe watoto elimu kama hiyo, japo wadogo ili wawe na ujasiri, angalau akiitwa na mtu asiyemjua *at least* aweze kusema sitaki. Kwa sababu watu wengine humu kazi

yao kutafuta watoto na kuwaharibu, ambao wenye akili hafifu wanaotembea njiani, haipendezi kwa kweli. Serikali ichukue hatua madhubuti kwa watu kama hawa. Serikali ikichukua hatua madhubuti ina maana hata wale wengine watashindwa kufanya vitendo viovu kama hivi.

Pia, nawasisitiza Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu na wazazi wote kwa ujumla. Jamani sisi ndio wazazi uchungu tunaujua sisi, baba yeye akishaweka vitu vyake, huyo anakwenda zake. Lakini sisi ndio tunaoujua uchungu, tunaoumia vitandani, tunaolea. Kwa hivyo, mambo kama haya ni lazima tuyakemee. Naomba Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu kila mmoja hapa mwanamke asimame aichangie kwa nguvu zote ili hoja hii ipite na kuweza kupunguza vitendo viovu kama hivi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nayapongeza yote maazimio tisa yote aliyoyasema Mhe. Mgeni Hassan Juma, lakini nayasisitiza hasa la kwanza kuhusu elimu katika ngazi ya msingi. Elimu inaweza kuwajenga watoto wawe wanajiamini, wawe wanatembea kifua mbele, kwa sababu anakuwa ameshajengeka.Kwa hivyo, anakuwa hawezi kudanganyika kwa kitu chochote.

Jengine ni suala zima la kifaa cha mashine ya *DNA*. Serikali ijitahidi kwa nguvu zake zote itafute kifaa hichi, kwa sababu mtu akifanyiwa udhalilishaji wowote ushahidi utakuwa haupo, kitachukuliwa kipimo kile kitapelekwa Muhimbili kikifika huko pengine kitakuwa kimeshaharibika. Kwa kweli inakuwa haipendezi, matokeo yatakayotoka Muhimbili yatakuwa tofauti kwa sababu kipindi kile cha kuhamisha mpaka ikifika Muhimbili ushahidi wote unakuwa umeshapotea.

Naiomba sana serikali ijitahidi kama ilivyokuwa na mikakati ya kununua meli hapa kila bajeti ya Wizara imekatwa ili kuhakikisha meli inanunuliwa. Na katika hili Mhe. Mwenyekiti, pia, serikali ijitahidi. Bajeti ya mwaka ujao kila wizara ikatwe pesa ili kuhakikisha kinanunuliwa kifaa hicho.

Mhe. Mwenyekiti, jengine kuhusu Mahakama za watoto. Kama Mhe. Mgeni Hassan Juma, katika azimio lake amesema Mahakama za watoto wawekwe mahakimu wa kutosha, majengo, dhamana ili zile kesi zikienda ziwe na mazingira mazuri ya kusikilizwa. Pia, *coordination* baina ya taasisi za kiraia na serikali kwa kufanya mashirikiano. Vyombo hivi vikishirikiana pamoja. Kwa hivyo, hata ule utekelezaji wake unakuwa rahisi na hata maamuzi yakitolewa yanatolewa kwa pamoja. Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kuweza kunipatia nafasi niweze kusema machache juu ya hoja hii aliyoileta mwenzetu Mhe. Mgeni Hassan Juma. Kabla sijaendelea naomba na mimi nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa ambaye ameileta hoja hii. Kwanza niseme amekuwa jasiri kwa kuweza kuileta hoja hii mbele yetu. Pia, kuonesha kwa kiasi gani alivyokasirishwa na wimbi kubwa la matukio haya ambayo baada ya kuileta hoja hii amekuwa hata sisi Wajumbe ametutonesha kabisa matumbo yetu. Sisi wanawake ndio tunaowazaa hao wahalifu.

Mhe. Mwenyekiti, ni jinsi gani mwanamke anaathirika kutokana na kadhia hii. Tulikuwa tuna Mswada ule ambao tumeupitisha juzi hapa ambao ulikuwa unasema neno muathirika unafafanua maana ya muathirika. Lakini na hili la kubakiwa watoto wetu sisi kama wazazi linatuathiri sana. Labda tunaweza tukajiuliza maswali mengi kwamba sasa hivi labda watu wanapata ugonjwa ma-*pressure* mengi, sukari nyingi, tujiulize ni kwa sababu gani. Hili pia linachangia kwa sababu mtu yeyote au mzazi yeyote ambaye atakutwa na kadhia hii kwa mwanawe basi hatokuwa muathirika yule mtoto tu na mzazi wake ataathirika, hili ni jambo ambalo linaumiza sana Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kadhia hii ambayo mwenzetu ameona asinyamaze kimya kwa kuona vitendo hivi vinazidi siku hadi siku, na hapa kesi ambazo zinaonekana udhaifu wake jinsi gani kesi zimepelekwa na jinsi gani kesi ambazo zimechukuliwa hukumu. Jambo hili linaonesha kwamba bado hatujawa *serious* nalo kulifanyiwa hukumu zinazokubaliana ili wale wengine iwe ni funzo kwao.

Mhe. Mwenyekiti, vitendo hivi vya udhalilishaji niseme labda si kwa watoto wetu tu lakini pia kuna wazee wetu pia wanafanyiwa vitendo hivi. Mtu anamuona mtu mzima hajiwezi basi anaingia anamfanyia vitendo hivi. Kwa hivyo, tuelewe katika udhalilishaji huu pamoja na watoto wetu lakini na wazee wetu wengine wanafanyiwa vitendo hivi. Kwa hivyo, udhalilishaji huu unatukumba au unatugusa katika sehemu kubwa, tunadhalilishiwa watoto wetu, lakini pia tunadhalilishiwa na wazee wetu.

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa kuhusu kadhia hii kumekuwa na waratibu wengi ambao wanajihusisha katika ufuatiliaji wa mambo haya. Watafuatilia kuanzia hatua ya kwanza mpaka mwisho. Ushahidi umeshakamilika, lakini baadaye inapofika kesi Mahakamani inakuwa hakuna kinachoendelea, kwa hiyo inakuwa tunawavunja moyo wale ambao wanatusaidia juu ya kadhia hizi ambazo zinatupata.

Mhe. Mwenyekiti, kadhia nyengine kubwa ambayo inatupata, mimi naiomba sana serikali kwa sababu ukosefu wa chombo hichi cha *DNA*, mimi nasema watu wanapata kichaka cha kujificha, mtu anajua umeshamkamata hivi, lakini ukienda Mahakamani unaambiwa bado ushahidi hautoshi. Lakini kikiwepo hiki chombo baada ya kukamatwa na chombo hiki kipo kikathibitisha, tutaweza kupiga hatua katika kesi hizi.

Mhe. Marina Joel Thomas, amenifilisi hapa kidogo amesema kwamba serikali ilipotaka jambo lake la kununua meli hapa Wizara zilikatwa bajeti, lakini wakahakikisha suala la meli linafanikiwa. Lakini kuhusu jambo hili inaonekana bado hatua zozote hazijachukuliwa, hii *DNA* inauzwa bilioni ngapi. Jamani tunaumia! Wazazi tunaumia kuona watoto wetu wanafanyiwa vitendo visivyokuwa na maana tunawavunjia maisha yao, halafu bado sisi hatujaona hatua za kuchukua, Hichi chombo ni muhimu kinunuliwe ili uweze kupatikana huo uthibitisho unaotakiwa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme nayaunga mkono maazimio haya yote ambayo Mhe. Mgeni ameyaleta hapa. Lakini pia nilitaka niseme karafuu zimeundiwa *task force* ili zisiibiwe wala zisiuzwe magendo. Na hili jamani kwa sasa liundiwe *task force* ili ziweze kushughulikiwa kila ilipo kesi hii tuweze kuijua na imefikia hatua gani.

Mhe. Mwenyekiti, sisi wanawake lazima tukereke sana juu ya kadhia hii, na kwa nini tukereke. Kwa sababu sisi ndio wazazi tuliobeba ujauzito tena kwa tabu sana, mpaka tukafika kujifungua, tukapinda kigongo kumlea mtoto. Leo mtoto keshakuwa wa kutia tamaa anatokea jambazi anakuja kumbaka, ni kitu cha kusikitisha. Lazima sisi wanawake tukereke. Na katika shehia zetu mwenzetu ikimfika kadhia kama hii basi tuungane naye kwa kwenda kumpa ushauri, kumsaidia njia au hatua za kuchukua ili tuone kesi yake ile inafika mbele ya sheria na inachukuliwa hatua.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kadhia ambayo inawapata watoto wetu wa kike, lakini kadhia kubwa zaidi ipo kwa watoto wa kiume kulawitiwa. Tatizo hili mimi naomba bado tufanye utafiti wa kina. Tatizo hili bado linaonekana lipo kwa asilimia kubwa sana. Tatizo hili la kulawitiwa watoto wetu wa kiume maana yake tusitegemee kizazi ambacho kitapatikana hapo baadae. Watu wote wameshakuwa goi goi atazaa nani? Lazima hili tulifanyie utafiti wa kina na liweze kuchukuliwa hatua za kisheria.

Mhe. Mwenyekiti, wito wangu kwa jamii, wenzangu wengi wamesema hapa, lakini na mimi naongeza kusema kwamba jamii hivi sasa tubadilike, tuache mtindo ule wa kuzihukumu kesi hizi kinyumbani, jamani tuache! Kwa sababu wewe unachukua unaona huyu ni mjomba yangu au ni kaka yangu au ni ndugu yangu, lakini yeye kitendo alichokufanyia ni cha kinyama. Kwa nini wewe umjengee utu wakati yeye kakufanyia kitendo cha kinyama. Mimi naomba sana jamii ibadilike kwa hivi sasa. Kama hatukubadilika basi vitendo hivi vitakuwa havina dawa na vitaendelea siku hadi siku kwa kuoneana huruma wakati huyo unayemuonea huruma yeye hakuonei huruma.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niungane na wenzangu katika haya maazimio aliyoyaleta Mhe. Mgeni Hassan Juma, kifungu cha 4, 5, 6, na cha 7 pia nakikubali sana, niseme vifungu vyote, kwa kweli vyote vina uzito mzuri na vina maneno mazuri. Mimi naungana na yeye kwa asilimia mia moja ili hoja hii ijadiliwe na Wajumbe waendelee kutoa michango yao ambayo itaweza kuisaidia hoja hii na baadaye tuweze kuipitisha na yaweze kuwa maazimio haya yametokana na Baraza hili Tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nasisitiza tena *DNA* inunuliwe kwa hali na mali.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii nami nikapata nafasi ya kutoa mchango wangu juu ya hoja ya Mhe. Mjumbe inayohusiana na maazimio dhidi ya vitendo vya udhalilishaji wa watoto Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nimelazimika na ni wajibu wangu kama Mwakilishi wa wananchi wa Zanzibar wa jimbo la Magomeni, na kwa sababu kama sijachangia hoja hii ya Mheshimiwa Mjumbe naona nitakuwa sijawatendea haki wananchi wa jimbo langu la Magomeni. Wananchi wa Jimbo la Magomeni ni miongoni mwa waathirika wa jambo hili, na mara nyingi nimekuwa nikipata malalamiko juu ya vitendo hivi vya udhalilishaji ama vya watoto wa kiume ama vya watoto wadogo wa kike.
Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti nimeona na mimi niungane na Wajumbe wenzangu, niungane na mtoa hoja Mhe. Mgeni Hassan Juma, kuzungumzia kadhia hii ya udhalilishaji au ya vitendo vya udhalilishaji kwa watoto Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, wenzetu hapa kinamama Wajumbe wanawake mara nyingi wanaona wao ndio wanaguswa zaidi kuliko kinababa. Lakini na sisi wanaume tunaguswa zaidi kuliko hata wao. Na hata Baraza lako hili Mwenyekiti ukiliangalia kinamama wengi hawapo. Mimi Mhe. Mwenyekiti ningetegemea kwamba hoja hii ambayo imewasilishwa tokea asubuhi basi sisi wanaume tungekuwa hatupati nafasi, lakini kumbe ni kinyume chake wanawake hawapo kabisa.

Sasa mimi nashangaa kuwa tunaonekana kama sisi ndio wakorofi, maana sisi ndio kinababa tunaofanya mambo hayo ya udhalilishaji, tukategemea leo kinamama hapa watafunga vibwebwe kuiambia serikali, kutaka serikali ichukue hatua lakini kinyume chake wameingia mitini.

Lakini sisi kinababa tutasema na kwa kweli hili jambo linagusa jinsia zote. Na kwa kweli Mhe. Mwenyekiti mimi napata uchungu mkubwa sana ninaposikia katika vyombo vya habari kwamba mtoto mdogo wa miaka 3, 4, 5, 6, 9 ameingiliwa amedhalilishwa. Wengine watoto wa kiume wamedhalilishwa kinyume cha maumbile, kwa kweli Mhe. Mwenyekiti huwa napata uchungu mkubwa sana. Na uchungu niliokuwa nao kama ningekuwa mwanamama labda mjamzito nadhani ningepata kujifungua kwa uchungu ninaouona na kukaribia kulia. Na kwa sababu sioni sababu ya jitu zima mwanamme shababi unakwenda kumuingilia mtoto wa mwenzio kinyume cha maumbile kwa hamu gani uliyokuwa nayo, kwa kivutio gani alichonacho mtoto wa miaka 3 na 4, huu ni ufisadi wa hali ya juu na ni udhalilishaji wa hali ya juu. Na jambo hili kwa kweli Mhe. Mwenyekiti linahitaji kuchukuliwa hatua zilizo imara zaidi, hatua madhubuti. Na bado pamoja na juhudi ya serikali na hatua zinazochukuliwa na serikali lakini inaonekana bado hakujawa na hatua zile hasa zinazostahiki juu ya vitendo hivi. Kwa kweli watoto wetu hatuwafanyii mambo yanayostahiki kabisa.

Sheria zetu kama alivyosema mtoa hoja bado zinaonekana ni dhaifu, juzi tulikuwa tunasikia rufaa ya yule babu Seya na mwanawe juu ya udhalilishaji ya watoto wa kike wamefungwa vifungo vya maisha kule Tanzania Bara, wamekatiwa rufaa, wamekwenda kwenye rufaa, Mahkama Kuu imesema warejeshwe waendelee kutumikia vifungo vyao vya maisha. Pale sasa utaona jinsi gani wenzetu walivyo *serious* juu ya jambo hili.

Lakini mbali na vifungo vya maisha utasikia hukumu zinazotolewa kwa wenzetu Tanzania Bara mtu akimdhalilisha mtu anafungwa miaka 30 jela. Lakini hebu tuziangalie sheria zetu, kweli sheria zetu adhabu zinazotolewa zinalingana na kosa lenyewe, hazilingani kabisa.

Lakini mbali ya kwamba hazilingani na makosa yenyewe lakini hata hao katika vyombo ambavyo tumevipa majukumu ya kisheria kushughulikia makosa ya jinai wanaonekana na wao pia hawako *serious* katika jambo hili. Juzi nilikuwa nasikiliza redio kuna kijana wa miaka 20 amemuingilia kinyume cha maumbile mtoto wa miaka 9 eti kenda kafungwa miezi kumi jela. Hivi hakimu yule ingekuwa mtoto yule ni mtoto wake angekubali keshaharibiwa mtoto tena kinyume cha maumbile mtoto wa miaka 9 anakwenda kufungwa miezi kumi. Hivi kweli tuko *serious* katika kuondosha jambo hili.

Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti mambo haya yanatia uchungu, na kwa kweli wenzetu hawa waliopewa dhamana ama vyombo vya Polisi au ni mahkama wasifanye mchezo katika jambo hili, huu ni udhalilishaji mkubwa ni mambo ambayo yanastahiki kuchukuliwa hatua kali za kisheria.

Mhe. Mwenyekiti nilikuwa naangalia takwimu za mtoa hoja ambazo amezieleza juu ya matukio yaliyotokea kwa kesi mbali mbali kuanzia mwaka 2010, 2011 na 2012 juu ya kesi zilizopelekwa mahkamani zilizokwisha kuhukumiwa, na bado
nyengine zinaendelea kusikilizwa mahkamani na kesi ambazo watuhumiwa wametiwa hatiani na wale walioachiwa huru wameachiwa huru, kwa kweli takwimu hizi zinatisha.

Kwa mfano mwaka 2010 kesi zipatazo 48 zilifunguliwa, ambapo kesi 35 zilitolewa maamuzi, kesi 13 zinaendelea kusikilizwa na kesi zilizotolewa maamuzi ni kesi 2 tu ambazo washtakiwa wake walipatikana na hatia na kuhukumiwa adhabu ya kifungo na 7 *fine* na kesi 28 washtakiwa wao wameachiwa huru. Hivi katika hali ya kawaida na juu ya tukio ya jambo hili na mambo haya yalivyo ni kweli watu 28 waliokamatwa miongoni mwa watu 35 ambapo 2 tu ndio wametiwa hatiani katika mazingira ya kawaida kweli *seriousness* ipo.

Hivi kweli hawa watuhumiwa hawa waliokamatwa wameonewa kwa kiwango kikubwa kiasi hiki au tuseme ushahidi haupo, kwa kweli jambo hili linahitaji kuangaliwa kwa umakini sana, lazima serikali iwe *serious* katika jambo hili.

Taarifa tulizonazo kwamba sheria zimewapa Polisi uwezo wa kuhifadhi vinasaba, hebu tutizame Polisi wana uwezo huo, wanazo zana hizo, wanavyo vyombo hivyo. Mwenzangu anasema hapa upanga wao umeibiwa leo tunawapa jukumu la kuweza kuhifadi vinasaba. Polisi kweli kama sheria inaelekeza hivyo nadhani sheria hii Mhe. Mwanasheria Mkuu inahitaji kufanyiwa marekebisho ili kuondokana na jambo hili.

Hapa nimetoa takwimu tu za mwaka 2010 lakini ukiangalia takwimu za mwaka 2011 halikadhalika ziko hivyo hivyo, washtakiwa 2 tu ndio wametiwa kifungoni na vifungo vyenyewe ndio hivyo vya miezi 10, miezi 2 miezi 3. Lakini halikadhalika hata mwaka 2012 zinaonesha hivyo hivyo, mimi Mhe. Mwenyekiti nathubutu kusema kwamba tatizo hili sasa serikali itangaze kwamba ni janga la taifa, ikubali kutangaza kwamba suala la udhalilishaji wa watoto liwe ni janga la taifa kabisa.

Na nadhani tutakapofika pahala tukikubaliana kwamba hili ni janga la taifa maana yake sasa hatua zitachukuliwa juu ya mambo yote yanayosababisha kwamba hatua zisichukuliwe dhidi ya watu hawa na ndio maana vitendo hivi vinaongezeka. Kwa kuwa hakuna hatua madhubuti zinazochukuliwa za kupambana na jambo hili maana yake vitendo hivi vinaongezeka. Watoto wetu wataendelea kudhalilishwa, watoto wetu wa kiume wadogo wataendelea kunajisiwa, na mijitu mizima hii inatia uchungu na kwa sababu hakuna hatua madhubuti zinazochukuliwa kupambana na jambo hili.

Mhe. Mwenyekiti Polisi hawa lazima wafike pahala wajue kitu gani wanachokifanya na wajue dhamana zao juu ya taifa hili, wasifanye majukumu yao kwamba ni vitega uchumi vyao, wasiyachukulie matatizo ya wananchi kwamba ni sehemu ya uchumi wao hilo ni jambo la hatari. Lazima wafike pahali waelewe kwamba rushwa ni adui wa nchi, wanapofika kuona rushwa ni jambo la kawaida basi taifa hili wataliangamiza.

Mhe. Mwenyekiti juzi au siku za hivi karibuni kuna mzee mmoja amemuingilia mwanawe wa kumzaa wa miaka 9, kwa bahati baba yule kashikwa na watu kwa kufanya vitendo vile. Kwa bahati kwa uchungu kabisa watu wale walimchukua na kumpeleka Polisi kwa kosa lile. Lakini katika mazingira ya kutatanisha baba yule na mkewe na yule mtoto wakachukuana wakaenda Polisi walipofika Polisi wakaenda wakasema kwamba mpaka sasa

yule mzee amekwenda kuomba radhi, amemuomba radhi mwanawe, amemuomba radhi mkewe kwa kitendo kilichotokea na wameshakubali kumsamehe na atampa yule mtoto faini ya shilingi laki tano ili jambo hili liishe. Wamekwenda Polisi kwamba mama mtu na mtoto wa miaka 9 wamemsamehe baba yao na yule kamsamehe mumewe kwa kitendo alichokifanya na atampa fidia yule mtoto shilingi laki tano.

Na Polisi wamekubali kufuta kesi ile isiendelee kwa sababu ndio tayari wameshakubaliana. Hebu tuangalie mazingira kama hayo, mtu mwanawe wa kumzaa ana kivutio gani, kwa kweli hili jambo linasikitisha sana na linahitaji kuchukuliwa hatua zinazostahiki, wenzetu Polisi lazima watusaidie, hawana mamlaka ya kufuta kesi, inapotokea kesi ya jinai waipeleke mahkamani.

Polisi wamekuwa wakizungusha wananchi, hivi karibuni mimi kuna mama mmoja alinijia mwanawe wa kiume amefanyiwa vitendo vya udhalilishaji amekwenda Polisi Kituo cha Mwanakwerekwe, siku tatu, nne anazungushwa, anaambiwa mara nenda mara rudi mara hivi na mwanzo walifanya vizuri walipofika pale wamemchukua wamekwenda naye hospitali ameangaliwa maelezo ya daktari lakini wameshindwa kumpeleka mahkamani.

Kwa hivyo, wenzetu hawa Kamishna mpya wa Polisi aliyeteuliwa juzi lazima atusaidie katika hili kuona kwamba watu ambao wamekamatwa juu ya vitendo hivi wanafikishwa katika vyombo vya sheria na mahkama nazo zisaidie nchi, janga hili ni kubwa na kama halitodhibitiwa basi tutakuwa hatuna taifa hapo baadae. Watoto wa kiume wadogo wanaingiliwa ovyo, hivi katika zama za leo mtu anaweza kufanya kitendo kama hicho, watu wamejaa tele kwenda kuchukua vitoto vidogo, ukizunguka tu, wanakwenda kutafuta vitoto vidogo unavidhalilisha unaviingilia, hawa wanatakiwa wahukumiwe kunyongwa hawa! Mtu kama huyu anayekamatwa kuwaingilia watoto wadogo ahukumiwe kunyongwa huyu! Mwenzangu hapa Mhe. Hija alisema wahasiwe, mimi nasema hawa wanyongwe hadharani! Tutakapowanyonga hawa hadharani maana yake hili jambo litakoma, kila mmoja atamtafuta yule anayestahiki, kwa kweli wanafanya vitendo vibaya si vya kibinaadamu. Sisi sio wanyama sisi ni binaadamu, Mwenyezi Mungu katupa akili leo tumegeuka wanyama mtu anamuingilia mwanawe, anamuingilia mtoto mdogo kinyume na maumbile, mtu mzima ana akili timamu asinyongwe kwa sababu gani, lazima anyongwe kwa sababu ataendeleza tu vitendo hivi. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti mimi nakubaliana.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti mimi nakubaliana na hoja za mtoa hoja, maazimio ya mtoa hoja, maazimio kama tisa juu ya kuitaka serikali ichukue hatua juu ya mambo haya, na vyombo hivi lazima vifike pahala visaidie taifa hili, Polisi, Makundi ya Wanasheria, Asasi za Kiraia, Ofisi ya Mkurugenzi wa

Mashtaka, Wakuu wa Wilaya, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na wengine wote wanaohusika na masuala haya.

Lakini na wazee nao lazima walisaidie taifa hili, siku hizi kuna tabia ya watu kuzungumza wenyewe kwa wenyewe. Kitendo kinafanyika eti wanafanya mazungumzo wanakubaliana, mnakubaliana na mtu hasidi huwezi kuwa na mazungumzo kwenye mambo kama haya. Wengine wanakataa kwenda kutoa ushahidi, kwa hivyo vyombo hivi lazima vifike pahala vikae pamoja vijadili juu ya janga hili la taifa kuwanusuru watoto wetu wadogo hawajafikia umri wa kufanya vitendo hivyo tunawalazimisha kwa vijisenti, raha gani mtu anayoipata mimi sioni.

Kwa hivyo, mimi niiombe sana serikali iangalie sana maeneno haya ambayo mtoa hoja ameyaeleza, suala la *DNA* ambalo limezungumzwa ni muhimu tumekuwa tukizungumza tu hapa suala la *DNA* chombo hiki ni muhimu hasa kwa wakati huu na lazima serikali itenge fedha maalum kama wenzangu walivyosema kwa mwaka huu kwa ajili ya kununua kifaa hiki, hakina ughali wa kiasi hicho kuliko maisha ya watu.

Nadhani Mhe. Waziri wa Fedha anatusikia jambo hili tutaliangalia kwa macho mia, kuanzia kwenye Kamati ya Wenyeviti utakapoleta bajeti yako kwanza tutaangalia chombo hicho, Wizara ya Afya ambao ndio wahusika wa jambo hili si jambo la kudharau hata kidogo, na kwa sababu tatizo la kukosekana kwa chombo hiki lina athari kubwa, na kwa sababu linapotokea tokeo kama hili mwananchi mwenyewe anatakiwa eti akatoe fedha kwa ajili ya kipimo hiki, kipimo hiki hakipungui shilingi laki tatu. Polisi wanakwambia sisi pesa hatuna, ukienda Wizara ya Afya wanakwambia pesa hatuna, itabidi wewe mwenye mtoto ndiye unayetakiwa utoe fedha kwa ajili ya kipimo hiki cha *DNA* kule Dar es Salaam.

Matokeo yake kesi ile inakwenda uchunguzi ule haujulikani mwisho mtu hana uwezo wa kutoa shilingi laki tatu na hata yule aliyekuwa na uwezo wa kutoa laki tatu foleni iliyopo kule kwa wenzetu Bara jambo lile linachukua muda mkubwa mwaka mzima vipimo havijaletwa. Jambo hili Mhe. Mwenyekiti lazima katika bajeti hii lionekane na chombo hiki kinunuliwe na kinunuliwe kwa mujibu wa taratibu za manunuzi. Tenda iitishwe, kwa sababu Mhe. Mwenyekiti kumekuwa na kawaida tukiwa na shida ya kitu serikali ikatoa fedha, lakini utakuja kukuta katika mazingira ya kutatanisha waliohusika wananunua vitu ambavyo havihusiki vitu vibovu, fedha zikishatolewa na serikali tayari watu wenye tamaa wanakuja wanaona sasa na sisi ndio hapa pa kupata pesa.

Badala ya kupata kitu sahihi ambacho kitawasaidia watu, watu wanaweka tamaa matokeo yake kifaa kinakuja, chombo kinakuja kinafika hapa hakifai, unaambiwa sijui kitu hiki hakuna, kitu hiki hakuna. Kwa hivyo, lazima fedha zitakapopatikana za serikali zitumike kwa mujibu wa sheria, kwa mujibu wa tenda ili tuone chombo kile kinasaidia watu.

Mhe. Mwenyekiti baada ya maelezo hayo mimi nakubaliana na hoja zote na ni jambo la kweli, na nimpongeze Mhe. mtoa hoja na akatafakari na akaleta hoja iliyo sahihi tena imechelewa na inahitaji kufanyiwa kazi madhubuti. Sisi sote Mhe. Mwenyekiti ni wazazi hapa tuna watoto. Na kama leo unasikia linamkuta mwenzio basi ujue iko siku litakuja kukuta wewe au ndugu yako.

Kwa hivyo, sisi ndio dhamana kwa serikali, sisi ndio dhamana ya wananchi, sisi ndio waangalizi wa wananchi, jambo hili lazima tulichukulie *serious*. Si jambo la mchezo, hili si jambo la mas-hara na si jambo la mchezo, lazima tufanye jambo ambalo watu wanaona sheria hizi ziletwe hapa kama Polisi wamepewa dhamana ya kudhibiti vinasaba basi sheria hii lazima ibadilishwe ipelekwe katika taasisi ambayo ina uwezo. Hospitali ndio yenye uwezo wa kuhifadhi vinasaba hivi sio Jeshi la Polisi, tuwaachie Polisi wahifadhi pingu na mambo mengine lakini mambo haya ya kitaalamu yawe yanadhibitiwa na Wizara ya Afya, na kama kuna sheria zinazowapa mamlaka sheria hizo lazima zibadilishwe hazifai kwa sababu tunaona kuna mambo ya kiujanjaujanja.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti mimi baada ya maelezo hayo naungana mkono na hoja ya Mhe. Mjumbe na niiombe serikali mapendekezo yote haya 9 ambayo yameelezwa nayaunga mkono, lakini na moja ambalo naliongeza hili la kukubali kuwa tutangaze suala hili la udhalilishaji wa watoto ni janga la taifa lazima tukubaliane, hivyo hili ni janga la taifa si kitu cha mas-hara. Na kwa sababu kila kukicha jambo hili linaongezeka na hakuna hatua hasa madhubuti. Tunajua hatua zipo zinachukuliwa lakini zile madhubuti za kukomesha jambo hili inaonekana hazipo.

Kwa hivyo, baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti naunga mkono hoja na niwaombe wenzangu waunge mkono juu ya jambo hili, lakini kama wachangiaji wapo Mhe. Mwenyekiti naomba kuwasilisha hoja kwa mujibu wa kanuni ya 156 tuweke kanuni kando, kanuni ya 27(1)(3) ili Waheshimiwa Wajumbe waendelee kujadili hoja hii, na kwa sababu ni hoja muhimu na inagusa wananchi, kila mmoja anayo haki ya kujadili na kutoa maoni yake.

Kwa maana hiyo naomba kutoa hoja ya kuweka kanuni kando kwa mujibu wa kanuni ya 156 Kifungu cha 27 (3) ili Waheshimiwa Wajumbe waendelee kujadili hoja hii. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe haja ya kufanya hivyo ipo, na hapa nina orodha karibu 11 bado wanataka kuchangia.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali: Mhe. Mwenyekiti napenda kuchukua nafasi kukushukuru kwa dhati kabisa kwa nafasi hii adhimu uliyonipa katika mada ambayo iliyoletwa na Mhe. Mgeni dada yangu, na nichukue nafasi hii vile vile kuwaunga mkono wenzangu wote kwa michango yao ambayo iliyotumika sana hekma na busara. Mhe. Mwenyekiti nafikiri hoja za wenzangu pamoja na mimi na wenzangu wataokuja niungane na Mhe. Salmin Awadh kwa kweli ame-*wind up* katika mazingira ya kuondosha hili tatizo.

Mhe. Mwenyekiti hii hoja ina uzito wake na inatwambia kwamba maadili yetu kwa Zanzibar yameanza kupotea, lakini vile vile tujiulize tumefikwa na nini sisi Wazanzibari katika hayo. Mhe. Mwenyekiti hivi vitu vitaendelea na havitokwisha, tatizo litaendelea kuwepo na kwa sababu nina ushahidi tokea nimeingia kwenye Baraza ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Uzini nimekuwa kila ninapokuwa nina hoja lakini nina ushahidi, ndio maana
nikasema hili tatizo halitoweza kutoka kama hatutokuwa wakweli, lakini vile vile kama maadili yetu mapenzi tuliyokuwa nayo hatujaweza kuyaweka mbele ya Mwenyezi Mungu.

Mhe. Mwenyekiti, hivi karibuni kama miezi mitatu iliyopita kuna kesi nzito iliyotokea katika Mkoa wa Kusini Unguja, kilifanyika kitendo kinyume na maadili na maumbile ya binadamu. Kwa bahati wahusika hawakupewa mashirikiano na Jeshi la Polisi, huo ushahidi upo. Kwa mfano Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Ikulu na Utawala Bora, nachukua mfano wake, ile familia ilikwenda kwake baada ya kuona mashirikiano hakuna, kwa bahati Mhe. Waziri kama ni kiongozi wa wananchi na Waziri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, akamuandikia Kamanda wa Polisi barua kumwambia bwana uje tuonane kuna vitu nataka tuzungumze, miezi mitatu iliyopita. Kamishna wa Polisi anamuandikia Waziri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, anamwambia bwana huna haki wala uwezo wa kumwita.

Mhe. Mwenyekiti, familia imekwenda kwa Waziri baada ya kuona kwamba haki ile haipati kwa sababu familia hahe hohe ya kimasikini, si akina Raza, Jecha, Pandu, ni hahe hote wamekwenda kwa Mhe. Waziri ushahidi upo, *three Months ago*. Waziri kwa sababu ya nafasi yake ya Ikulu au Waziri

anayehusika yeyote ikiwa Waziri wa Afya, anamuandikia barua ili kupata maelezo zaidi kutokana na malalamiko ya familia ile ya hahe hohe. Kamishna anamuandikia barua Waziri miezi mitatu iliyopita anamwambia *hey, stop it* huna uwezo wala mamlaka, hii ni serikali matokeo yake hakuna kilichotokea.

Sasa ndipo ninaposema kwamba Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Salmin Awadh Salmin, kaka yangu na wengine waliotangulia *issue* hapa ninachoona Mwenyekiti, tuna tatizo, *there is a problem.So, we have to find a solution and what is next*.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu mimi napongeza, lakini kama hatukuwa *serious* na hivi vitu, kesi za miezi mitatu, sita zifufuliwe na hizo barua watu wawajibike. Hatuwezi kukaa tu, familia inakwenda kwa Waziri, halafu Waziri anaandika barua kwa ushahidi kwa sababu ya mkubwa tu, unajua tatizo letu wakati mwengine tunaharibikiwa sisi viongozi.

Kwa sababu mtu akishakuwa kiongozi, tena hata ule mwendo wa kwenda anauanza mwenigne, ule wa kawaida unakuwa haupo tena. Sasa Mhe. Mwenyekiti, hili ni tatizo, ninachoomba Mwenyekiti, Mhe. Salmin Awadh Salmin,hapa mimi katika kusaidia kupitia Baraza la Wawakilishi, sioni sababu ya serikali, najua
serikali yetu hahe hohe, tuna uchumi na bajeti, lakini sioni kwa sababu ya maslahi ya wananchi wa Zanzibari kama nchi, mashine hii kwa nini isipatikane kwa muda wa miezi mitatu.

Nina sababu zangu Mhe. Mwenyekiti, ninaomba mimi na Mhe. Salmin Awadh Salmin, tupewe fursa Baraza la Wawakilishi tuna wahisani, tuna ndugu zetu dunia nzima Marekani, Uingereza, Sweden, Abudhabi na Kuwait, kote niko tayari kwa Mhe. Salmin Awadh Salmin ama kupata mkopo usiokuwa na riba ama tutapata bure, tunaomba kazi hiyo tupewe kupitia taratibu za sheria na Katiba ya nchi yetu kama alivyosema Mhe. Salmin Awadh Salmin, mimi niko tayari.

Mhe. Mwenyekiti, nitakwenda safari hii kwa gharama zangu na nitamchukua Mhe. Salmin Awadh Salmin kwa gharama zangu kama Mzanzibari, hatutoitia serikali hasara. Mhe. Mwenyekiti, kufika kwangu hapa ni wananchi wa Zanzibar, wananchi ndio walionifikisha hapa nikavaa koti langu hili na tai humu ndani. Kwa hivyo, namshukuru Mwenyezi Mungu nitatumia rasilimali yangu walionisaidia wananchi kupeleka kwa wananchi wenzangu kwa Visiwa vya Unguja na Pemba na Tanzania kwa jumla bila ya kujali rangi, kabila, dini wala jinsia.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiri hayo yanatosheleza kutoa mchango wangu na imani yangu serikali katika hili tufikie pahala sasa *what is next, otherwise* Mhe. Mwenyekiti, watakaoumia zaidi ni masikini. Hilo lipo na litaendelea kuwepo, tutafanya mjadala na napongeza mjada huu uendelee, lakini tufikie *conclusion* kwamba hii mashine imepatikana.

Mhe. Mwenyekiti, ametwambia Mhe. Salmin Awadh Salmin, mtu anaambiwa aende Dar es Salaam shilingi laki tatu, masikini mshahara wake shilingi laki moja haufiki, hatuwezi ku-*solve problem* kama hatukuwa wakweli. Kwa hivyo, Baraza lako tukufu kupitia mwenyekiti wetu wa Baraza, Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na maazimisho ya Mapinduzi yetu matukufu ya miaka 50, basi tukitoka tuseme hii mashine miezi mitatu ishafika kwa uwezo wa *Allah*. Wananchi na serikali watatufahamu ama tutapata msaada au mkopo usiokuwa na riba kwa kuweza kulipa taratibu ili tuwaokoe watoto wetu wa leo na wa kesho kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa nafasi hii kuchangia hoja ya Mhe. Mgeni Hassan Juma, kwa umakini wake mkubwa na kuona umuhimu wa hoja hii kuleta Barazani. Kwanza nimpongeze
sana dada yangu Mhe. Mgeni Hassan Juma, juu ya hoja hii ya Baraza la Wawakilishi kuliomba kutoa azimio dhidi ya vitendo vya udhalilisha wa watoto wetu.

Kama tunavyojua Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa na dhamira ya dhati kwa kulinda watoto wa Zanzibar kwa kuchukua hatua mbali mbali ikiwemo ya kuwa na sheria Nam.6 ya 2011 na kuhakikisha kupatikana kwa haki zao ikiwa ni pamoja na kuwapatia elimu bora, makaazi bora, malazi, chakula na kuwalinda dhidi ya aina zote za ubakaji na udhalilishaji.

Mhe. Mwenyekiti, azma hii imekubalika dunia nzima na sio hapa Zanzibar tu, kwa kuwalinda watoto wetu kwa vitendo vyote vibaya vya udhalilishali na mambo mengine. Mimi nitoe mfano mmoja wangu mwenyewe binafsi mwaka 2000 nilibahatika kufika Marekani New York. Nilifika kwa rafiki yangu mmoja pale nikakaa kwa bahati usiku mwanawe akawa anaangalia televisheni, basi yule mtoto wazee wake wakamwambia kesho unakwenda skuli hiyo televisheni basi izime ukapumzike ili uweze kuamka asubuhi.

Kama unavyowajua watoto wetu wanakuwa na vipindi vyao kwenye televisheni, basi yule mtoto akasema nataka kuangalia hiki kipindi, akaambiwa aa kalale zima televisheni, baba mtu akazima televisheni ile mtoto akenda kulala.

Alipokwenda skuli mtoto yule akawa hayuko katika hali nzuri ya masomo yake na akawa hana furaha. Kwa bahati walimu wakamuuliza wewe una nini. Akasema jana baba yangu kanizimia televiseni usiku sijaangalia kipindi changu. Kwa hivyo, walimu wakapiga simu katika kitengo husika cha haki za binadamu hasa kwa watoto, wakaja kumfuatilia mtoto yule nyumbani na akaulizwa mbele ya wazee wake jana ulifanywa nini, Kwa bahati akasema alinizimia televisheni baba yangu na mambo mengine. Kwa bahati yule mtoto na mama wakazungumza kwa Kiswahili hawawezi kufahamu wale watu wa kitengo cha haki za binadamu.

Sasa wale watu wakamwambia tutakuchukua tutakuweka sehemu husika achana na kukaa na wazee wako, lakini bahati nzuri akazungumza lugha ya Kiswahili na baba yake pamoja na mama yake, wakamwambia wambie wasikuchukue hawa sio wenzetu ubaki kwetu, kataa kuondoka. Sasa mtoto yule akakataa akasema mimi nitakaa na wazazi wangu sitokuwa na nyinyi kwa sababu nawapenda na mtoto akabaki pale.

Lakini walipoondoka pale watu wa kitengo kile baada ya muda wakarudi na televisheni nyengine kubwa kuliko ile aliyokuwa anatizama mtoto yule, wakasema televisheni hii itawekwa chumbani kwake huyu asizimiwe mpaka atapochoka mwenyewe. Kwa kweli mimi mwenyewe nilishangaa kuona hali ile jinsi watoto wanavyopewa kipaumbele na wenzetu hawa Wazungu. Kwa hivyo, na sisi tulinde haki hii ya watoto kwa hali na mali kwa kuona hali hii, kwa sababu watoto ni muhimu sana katika taifa letu.

Tunategemea leo tupo sisi hapa katika Baraza la Wawakilishi, lakini kesho watakuja wao, sisi tutakuwa hatupo sote. Wenzetu wamejipanga sana kuwalea watoto wao kwa mazingira mazuri sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwalinda na kupata zile fursa za uhakika. Kama wanavyosema wenzetu mimi niliambiwa kule, kwanza anapewa haki mtoto, pili mwanamke, watatu anapewa mbwa na nne ni mwanamme. Kwa nini wanafanya hivyo, kwa sababu wanajua kwamba wakiwapa haki sana wanaume, basi udhalilishaji utakuwa mkubwa kwa upande wa wanaume.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli ongezeko hili la udhalilishaji halitokwisha hapa Zanzibar kama hatukuwa makini. Lakini mimi nizungumzie sekta tatu; ubakaji, ulawiti na udhalilishaji wa wanafunzi.

Mhe. Mwenyekiti, suala la ubakaji limekuwa ni mchezo wa kawaida sana hapa Zanzibar, Wajumbe wamezungumza kuhusu kesi nyingi na mifano mbali mbali, sitaki nizungume yote hayo. Lakini niseme tu kwamba kuna tatizo kubwa sana katika Mahakama zetu. Sasa tukiangalia ripoti hii nzuri

aliyoileta Mhe. Mgeni Hassan Juma, imeeleza wazi haikuficha kitu na kwa kweli inasikitisha sana, Mahakama zetu zinavyoendesha kesi hizi za udhalilishaji wa watoto.

Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia takwimu za Mahakama Kuu ya Zanzibar zinasikitisha na mimi nasema haitendi haki, sijui kuna nini, lakini kuna mambo yanafanyika hapa. Takwimu zinaonesha katika mwaka 2010 zilipatikana kesi 48 za udhalilishaji huu, lakini cha kusikitisha ni kwamba unakuta watu 28 wameachiwa huru karibu nusu bin nusu na hawa waliobakia 20 kesi yao inaendelea haijakuwa na ufafanuzi. Hatujasikia hata siku moja kama mtu kalawiti, basi kapata adhabu gani.

Tukija kwenye mwaka 2011 takwimu zinaonesha wazi kesi zote zilikuwa 74 zilizofunguliwa katika Mahakama Kuu, lakini kwa bahati mbaya au kwa kusikitisha sana walioachiwa huru ni watu 32, maana kama hawana kosa wakati pengine ushahidi upo, lakini hakuna kilichofanyika chochote. Naamini wazi watu hawa hiki kitendo wamekifanya cha kulawiti watoto wadogo, lakini kwa kuwa kuna mchezo unafanyika Mahakamani watu hawa wanakuwa wanaachiwa huru.

Mwaka 2012 kesi zilizofunguliwa 72, lakini kwa mwaka huu walioachiwa huru ni watu wanane. Sasa mimi sijui hapa kunakuwa kuna nini na kesi nyengine hatupati taarifa kama nani kafungwa na miaka mingapi. Tatizo kubwa Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia hapa ni ushahidi na huu ushahidi sio kama haupatikani, lakini ukishaweka mambo ya watu juu ya meza, basi ule ushahidi unauliwa kabisa, unaambiwa huyu mtu hajashiriki wala hajafanya kitendo kama hicho. Kwa hivyo, hakuna kinachoendelea kwa sababu ushahidi unakuwa mdogo kabisa.

Tatizo hili Mhe. Mwenyekiti, kama hatujawa makini hatuwezi kulimaliza suala hili Zanzibar, litaendelea siku baada ya siku na tutakuwa tunawadhalilisha watoto. Na kama nilivyosema mwanzo watoto ni taifa letu la kesho, tukishakufanya matendo kama haya kwa watoto wadogo hakuna kitakachokuwa, hii inapelekea ongezeko kubwa sana la ubakaji na kitendo hiki ni cha kinyama na cha ajabu kabisa kumfanyia mtoto.

Sheria hii Mhe. Mwenyekiti, bado adhabu yake haijawa mkini, mimi nashauri wale wanaoshughulikia suala hili la Mahakama au sheria, basi angalau mtu akifanya kosa hili afungwe miaka 30 na bila ya kuonewa huruma ukiwa ushahidi haujakamilika au umekamilika huyu mtu afungwe iwe onyo kwa wale wengine ambao watalikabili tendo kama hili.

Pia, nimuombe Kamishna wetu mpya aliyechaguliwa sasa hivi awe makini, kesi kama hizi zikipelekwa kituoni, basi kwanza adhabu inaanza pale kwa yule mtuhumiwa, kama kafanya basi adhabu ianze pale kabla ya kufikishwa Mahakamani. Naomba Kamishna awe makini na suala hili asije akalizembea zembea. Mtu atapofungwa kwa kesi kama hii, vyombo vya habari vitangaze. Mhe. Mwenyekiti, kila siku vitoe habari hii kama mtu kafungwa miaka 30 kwa tuhuma hii ili wale wengine waogope kufanya mambo kama haya ya ajabu.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme tu kwamba, suala hili la watoto limefanyiwa utafiti mkubwa sana, utafiti wa kisayansi unaoonesha kuwa mtoto wa miaka minane ya mwanzo ndio muhimu sana katika maisha yake yote atakayoishi katika dunia. Kwa hivyo, huu utafiti uliofanywa na wanasayansi hawa, mtoto ukimchanganya kwenye akili zile za miaka minane, hasomi tena na hawi mtoto mzuri katika jamii. Kwa hivyo, naomba katika miaka hii ni muhimu sana tuwalinde watoto wetu na tuwaangalie sana maisha yao.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, katika kuishi duniani kipindi chote achilia mtoto katika miaka minane, hiyo ndio inakuza kiakili katika kujifunza lugha haraka, mila na utamaduni wa eneo husika. Kwa hivyo, naomba miaka hii minane kwa wanasayansi wetu walivyosema tuzingatie sana kwa watoto wetu ili waweze kuwa watoto wazuri na maadili mema kabisa. Sasa mtu huyo akifanyiwa mambo kama haya sidhani kama atakuwa na akili ya kusoma au kuwa na maisha yake mema baadae.

Mhe. Mwenyekiti, huu udhalilishaji sasa hivi umekuwa ni kitu cha kawaida, mimi naomba wazee, viongozi wenzangu, serikali kwa ujumla, wadau mbali mbali na wafanyabiashara, tushirikiane kwa pamoja kuliondosha suala hili, utaposikia au kama kuna ushahidi basi tukae pamoja sote kulisimamia suala hili ili mtuhumiwa apate adhabu yake inayostahiki. Tusimuonee mtu huruma wala aibu kwa sababu sote tunajuana humu. Hivyo, tushirikiane kwa pamoja kuliondosha tatizo hili hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitoe mfano wangu binafsi, nilipokuwa mdogo kwenye miaka kumi au kumi na mbili nilikuwa naishi Malindi pale, baba yetu alikuwa anatwambia Mzee Ibrahim Makungu, hapa angalieni sana mtaa huu wa Malindi, eneo la Funguni kule msisogee. Sasa mimi nikawa sijafahamu kipindi kile, nikawa naogopa kwenda, lakini sijajua kuna tatizo gani kule Funguni, akasema sitaki kusikia kabisa mnakwenda katika eneo lile la Funguni muishie huku huku kucheza.

Sasa hivi nakumbuka na najua umuhimu wake Mzee wangu kunambia vile, alikuwa ana maana yake ili tusije tukafanya mambo mabaya kama haya

tunayoyazungumza sasa hivi. Kwa hivyo, naomba wazee wote wawe makini kwa watoto wao, wakishakuona eneo hili sio zuri, basi wawazuie watoto wao wasisogee kule, wawe walinzi kwa watoto wao na sio wazee tu kila mtu awajibike na suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niingie kidogo suala la wanafunzi ambao wanasoma mpaka sasa wapo skuli. Kuna siku moja nilikuwa Darajani nimekaa na kipindi hicho hata bado sijagombea kuwa Mwakilishi au haijatokea nafasi ya kuingia kwenye kinyang'anyiro cha kugombania Jimbo la Bububu, watoto watatu waliingia kwenye daladala na kuingia yule utingo akawasukuma, akawaambia msiingie humu kwa sababu mimi nishapakia watoto watatu na nikiwapakia na nyinyi watatu mtakuwa sita na nauli yenu ni ndogo. Sasa yule mmoja aliposukumwa aliumia mdomoni mimi nikenda pale nikamwambia kwa nini unawasukuma watoto, akasema mimi siwezi kupakia tajiri wangu hawezi kuniruhusu kupakia watoto, pesa zitakuwa kidogo.

Mimi niliwalipia watoto wale nauli halali kabisa ya mtu mzima nikamwambia basi waachie waingie kwenye gari. Kwa bahati nzuri watoto wale wanakwenda Bububu wanarudi nyumbani kwao, lakini nashukuru Mwenyezi Mungu nilisema pale pale, endapo kama mimi nitakuwa Mwakilishi siku yoyote au Mbunge basi nitahakikisha wanafunzi nawawekea basi litakuwa bure bila ya malipo wasidhalilishwe na mtu yeyote.

Kwa hivyo, namshukuru Mwenyezi Mungu azma yangu ile kaniona na kanisikia na mimi kufanikiwa kuingia kwenye kinyang'anyiro hiki na kushinda, basi nikatafuta mabasi ya wanafunzi na mpaka leo hii sitaki wanafunzi wa Jimbo la Bububu kuulizwa nauli hata shilingi kwa sababu sitaki kuona hali ile ya zamani inarudia kwao.

Mhe Mwenyekiti, nitoe mfano mwengine, mara mbili nishawafukuza madereva wangu wakipakia wanafunzi wanakuwa na tabia mbaya ya kuwataka, mimi nimeweka walinzi ndani ya basi mle. Sasa ukianza kufanya mambo yale nikipata taarifa mwenyewe nakwenda namfukuza kazi mtu pale pale. Kwa hivyo, naomba viongozi wenzangu tushirikiane pamoja hili suala ni letu sote tuwasaidie watoto na wanafunzi wetu hawa ili waweze kufanya safari zao kwa urahisi na bila ya kudhalilishwa.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana mimi naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na nakushukuru sana.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nakushukuru sana kunipatia nafasi hii kutoa mchango wangu katika hoja iliyo mbele yetu. Kwanza kabisa nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Mgeni Hassan Juma,

kuleta hoja hii katika chombo kikubwa na kupata fursa ya kuijadili. Mhe. Mgeni Hassan Juma ni Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii. Nadhani katika kufanya kazi za kamati katika kupata hoja au maoni ya wananchi, amevutiwa sana na kuweza kupata fikra na busara kuweza kupanga na kuleta hoja hii. Hii ni kwa mujibu wa utekelezaji wake wa kamati ameona udhalilishaji katika shughuli zake za kufanya kazi na ndio akaleta hoja hii. Mimi niseme nampongeza sana na awe na moyo huo.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, vitendo vya udhalilishaji vinazidi kushamiri siku hadi siku. Mhe. Mwenyekiti, nikiwa nazungumza hapa ni juzi tu kijana wa miaka 20 kambaka mtoto wa miaka minne na kumharibu vibaya, shughuli hii kila siku inaendelea na kama hatukujipanga vizuri, basi siku hadi siku wimbi hili litaendelea. Nilimsikia Mhe. Hamza Hassan Juma, hapa akichangia mchana alisema mtoto anaharibiwa mpaka kufika kutembea kama kaa, sijui nyinyi wenzangu kaa mnamjua kwa wale wavuvi au hamumjui mnasikia tu. Kaa anapotembea hutanua magando yake, sasa sijui kwa ulinzi, lakini kwa mtoto anayeharibiwa atakuwa na maumivu makubwa sana, nadhani ndivyo alivyokusudia Mhe. Hamza Hassan Juma.

Sasa kama hatukuwa wakali katika sheria hii Nam. 6 ya mwaka 2011, sheria ipo ila inataka usimamizi mzuri wa kuwalinda watoto wetu, bila ya hivyo, tutakuwa tunatwanga maji katika kinu yatakuwa hayakai.

Mhe. Mwenyekiti, tukizungumzia katika mambo ya udhalilishaji mara nyingi watoto wetu wanapodhalilishwa, basi ushahidi unakuwa haupatikani kwa woga wa watu, jambo hili si la kulifumbia macho ni jambo hatarishi kabisa. Kwa sababu kesi hizi zinapopelekwa Mahakamani au hazifiki Mahakamani watu wanazisuluhisha kienyeji tu, mimi nadhani tungekuwa na utaratibu kesi hizi zisikubalike kusuluhishwa kienyeji, mtu akipatikana na hatia hii moja kwa moja apelekwe Mahakamani na aweze kusikiliza jalada lake litakavyosomwa na akipatikana na hatia, basi apewe hukumu kali iwe fundisho kwa watu wengine.

Mhe. Mwenyekiti, nikiwa naendelea na mchango wangu huu kama kesi hizi tutazisimamia vizuri, kazungumza Mhe. Makame Mshimba Mbarouk jioni hii, kasema jinsi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inavyojipanga inapofika misimu ya zao la karafuu kwa kule Pemba, tunaona kila sehemu tuna *road block* la kuzuwia magendo ya karafuu yasifanyike. Basi kama tuna dhamira nzuri kama hoja hii inavyoeleza, ni vyema na sisi tukawa na ulinzi wa kutosha na mtu akipatikana na hatia hii akawa kama alivyozungumza Mhe. Hussein Ibrahim Makungu, basi asifichwe.

Mhe. Hija Hassan Hija, kazungumza hapa kama mtu aliyekuwa akifanya kosa hili anaitwa kitangi na kutajwa hadharani si jambo la aibu, kwa sababu kesi hii ni sawa sawa na ya uuaji, mtoto mdogo wa miaka minne unambaka unakusudia nini, ndio uuaji. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, jambo hili si la mzaha isiwe tunazungumza tu hapa likawa halina mkazo wowote, lazima tulitilie mkazo wa nguvu zote za kisheria tulizojipangia.

Mwenzangu alipozungumza Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, kasema jinsi serikali inavyoshughulika wakati wa msimu wa zao la karafuu wanavyojipanga kudhibiti yasifanyike magendo na karafuu zikauzwe kwa mujibu wa taratibu za kisheria. Mimi hapa nataka leo chama cha kisiasa kitangaze maandamano ya nchi nzima tena chama kiwe cha upinzani, uangalie serikali jinsi inavyojipanga na haijipangi kwa sababu ya nini, inajipanga kwa ajili ya usalama tu. Basi na sisi kama tunavyo dhamiria kuwalinda watoto wetu lazima serikali ijipange na ijue kwamba tendo alilofanyiwa mtoto wa mwenzako, ukifanyiwa wewe kama huridhiki basi ulichukie kwa nguvu zako zote. Si jambo zuri.

Mhe. Mwenyekiti, hapa katika maelezo ya mtoa hoja sehemu yake ya pili, naomba ninukuu kazungumzia kwamba, Na kwa kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeridhia mikataba inayohusiana na haki za watoto duniani ambapo Zanzibar inahusika katika utekelezaji wa mikataba hiyo ili kuona azma ya kuwalinda watoto inafikiwa. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeridhia, lakini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar nayo inahusika ili kuwalinda watoto. Kwa hivyo, sisi tunasema sote tushirikiane kwa vizuri ili watoto wetu wapate ulinzi na tendo hili la udhalilishaji likome kabisa.

Lakini vile vile, niseme tu kwamba kama wazazi na sisi tuna wajibu wa watoto wetu kuwalea katika mazingira yaliyo mazuri au katika utamaduni tuliyouzowea wa Kizanzibari. Leo mtoto anaweza kutoka nyumbani hujui muda gani wa kurejea, mtoto mdogo anarudi saa tano za usiku, mama au baba mzazi unakusudia nini ikiwa humkemei au mtoto anachukua mapambo kushinda mama yake, wewe mama mzazi unakusudia nini, huyu hawezi kufanya matendo mabaya japokuwa mdogo, anakulia vibaya. Sasa jambo hili tujidhatiti kweli kweli kwa walezi wa watoto wetu.

Zamani kulikuwa na vipindi vya televisheni basi mtoto ilikuwa ikifika saa moja na nusu kipindi cha watoto kimekwisha na hapo mtoto haruhusiwi tena kuangalia televisheni, angalieni watoto wetu wa siku hizi mpaka muda wa saa ngapi. Vile vile, watoto leo wako katika majumba ya starehe na katika majumba hayo kuna adhabu kali zinazotendeka, lakini mtoto unamuachia huru unategemea kupata mtoto wa aina gani.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani hoja hii imechangiwa sana na itaendelea kuchangiwa na kila mtu kutoa wazo lake. Mhe. Mjumbe, hapa Mhe. Salmin Awadh Salmin, kasimama na kasoma kifungu cha kanuni ili kuweza kuweka kanuni kando na kuongezewa muda ili kila Mjumbe apate kuchangia hoja hii iliyo muhimu. Sasa tunaomba kila mtu achukie matendo ya kudhalilishwa kwa watoto wetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nisiende mbali nitoe fursa kwa wenzangu, lakini jambo hili kama serikali italisimamia vizuri, basi sisemi kama litaondoka lakini walau litapungua. Mhe. Mwenyekiti, angalia mtu kambaka mwanawe na kafungwa na alipotoka jela karudia tena kitendo kile kile. Hii ni kuonesha adhabu haitoshi. Mheshimiwa, kapendekeza mpaka miaka 30, lakini mimi ninasema ipo haja ya mtu kufungwa hata maisha, kama alivyosema Mhe. Salmin Awadhi Salmin, Babu Seya na watoto wake ilivyokuwa pale.

Ni jambo baya sana. Kwa hivyo, hili si jambo la kulifumbia macho, sote tuwe walinzi wa watoto wetu, tukifanya utamaduni uliokuwa mzuri wa Kizanzibari huko tulikotokea, basi mambo haya hayawezi kutokea. Mimi ninataka mtu avae katika utamaduni wetu wa Kizanzibari; avae nguo zake halafu avae bui bui anakwenda na heshima zote hapati udhalilishaji wowote. Lakini mtu tukimuacha atembee na ki-*min,* basi hafiki, kila sehemu anayopita atapata adhabu tu ya mambo machafu, lakini kama unavaa vizuri, basi hata yule mtu anayefikiria dhana mbaya hakufiki.

Mhe. Mwenyekiti, kwa haya machache naunga mkono hoja na yale maazimio yote aliyoyatoa Mhe. Mgeni Hassan Juma, tisa ninayaunga mkono.

Kwa haya machache ninasema ahsante sana ninakushukuru kwa kutoa mchango wangu. Ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa hii jioni hii kuchangia hoja ambayo ni nzito kwa kusema kweli na ya aina yake.

Nichukue fursa hii kumpongeza kwa dhati kabisa Mwenyekiti wa Kamati ya Wanawake na Watoto na Ustawi wa Jamii Mhe. Mgeni Hassan Juma, kwa kitendo chake cha ujasiri, uungwana, cha huruma na kuwajali wananchi wa visiwa hivi vya Unguja na Pemba, *inshaallah* Mwenyezi Mungu akujaalia kila la heri, akulinde na madui. Ni mfano mzuri uliotoa na kuigwa. Nikupongeze kwa dhati kabisa ndani ya nafasi yangu.

Baada ya hapo ninataka nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Uzini Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali, kwa jitihada zake na kuwajali wananchi na yupo tayari kuchangia mchango huu kwa suala la *DNA.*

Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, nianze na mchango wangu kwa vyombo vya habari ambavyo vinakwenda kinyume na maadili yetu. Leo kama gari njiani inafanya makosa, Baraza la Mji wanaifunga wanaitia mnyororo. Kwa nini televisheni hizi zinazozagaa leseni zao zisifungwe. Hapa ipo haja leseni

zizuiwe. Matelevisheni yanaongezeka na watoto wetu wanaathirika.Ikawa sheria nyengine zinatungwa na magari, matelevisheni yanafunguliwa ovyo ovyo, televisheni zidhibitiwe, hizi ndizo chanzo cha kuharibu watoto wetu.

Ikiwa gazeti nalo linafungiwa linalofanya makosa, kwa nini televisheni isifungiwe. Magazeti mangapi yameshafungiwa hapa. Hii kesi nzito Mhe. Mwenyekiti, juzi gazeti la Mwananchi lilifungiwa likafunguliwa baadae. Tuangalie suala la televisheni na Mhe. Ismail Jussa Ladhu, alilizungumza suala hili na mimi ninasisitiza zaidi kuwa vyombo vya habari sasa hivi vifanye kazi kwa kuangaliwa. Chombo muhimu sana cha televisheni kwa kuharibu watoto, sio *TVZ* murekebishe kauli yangu ni vyombo vya televisheni, lazima leseni zao ziangaliwe, kikenda kinyume na taratibu kizuiliwe.

Nije katika sehemu ya pili uadilifu katika utendaji wa sheria hasa katika maeneo ya Mahakama, Jeshi la Polisi, Serikali za Mitaa, yaani Masheha katika kusimamia uadilifu Mhe. Abubakary Khamis Bakar, Mahakimu wao naomba azungumze nao, watoto wananyanyasika vibaya, tena kupita kiasi. Kesi zinarundikana tu. Mtoto baada ya siku mbili anapewa dhamana anaambiwa ushahidi haujakamilika.

Mhe. Hamza Hassan Juma, alizungumza kuwa sijui ushahidi gani unaohitajika tena, mtoto anatambaa kama kamba, mtu anapewa dhamana hatuwezi kufanya kazi namna hiyo Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Abubakary Khamis Bakar, mimi ninafikiri ipo haja ya kufanya semina na Mahakimu na Majaji wako kwa suala hili.

Sehemu ya tatu Mhe. Mwenyekiti, hapa kidogo itabidi uniruhusu ninukuu, "Serikali kwa kusimamia na kuzuia maporomoko ya maadili kwa mfano suala hili lina wajibu Kikatiba kulinda Kifungu cha 10 (f) cha Katiba ya 1984, utamaduni wa Zanzibar utalindwa, utaimarishwa na kuendelezwa kwa malengo makuu ya siasa Zanzibar".

Mfano suala la viroba jana au leo nililizungumza suala hili. Ulevi katika mitaa hivi sasa umezagaa na mabaa yamekuwa mengi mitaani. Zimbabwe kama sikosei ninafikiri wanaulizwa watu watano katika kijiji, akikataa moja leseni ya baa haipo. Wenzetu Uislamu haupo kuliko hapa Zanzibar, basi wanaheshimu.

Mimi ninafikiri Zimbabwe mbuzi akichinjwa akilia, basi unakuja kushtakiwa wewe. Leseni kama hizi ziangaliwe. Leo kila kichochoro kuna baa, unafikiri tutapata maadili kweli. Hatuwezi kwenda namna hii. Vitengo vya udhalilishaji wa watoto vinaendelea kuzidi na kuzidi.

Nije kwenye suala la *DNA. DNA* ipo Zanzibar, lakini iliyokuwepo ni *skeleton* tu, si *DNA*. Ipo Maruhubi Bohari Kuu, mimi nilikuwa ni mjumbe wa Kamati ya Wanawake na Watoto. *DNA* ipo lakini iliyokuwepo ni *frame* tu. Sasa sijui Mhe. Juma Duni Haji, alisema hapa katika kikao kilichopita kuwa *DNA* ipo, meli ipo njiani wakati wowoto itafika na maneno si yangu hayo kama tutafuata *hansard* tutapata hicho kitu.

Lakini kilicholetwa, sijui kama tumeuziwa kuku kwa mlio, yumo ndani ya gunia. Faida yake nini. *DNA* ipo Maruhubi, lakini sijui imeletwa kama kichwa, mguu haina. Hatuwezi kufanya kazi namana hii, ina maana gani na msaada kama ule. Umekaa mzigo tu pale na chombo chenyewe hakitoshi.
Ninarudia tena kusema kuwa *DNA run cost* yake ni kubwa, sio tunapiga kelele tu, si kitu kidogo, gharama zake ni kubwa. Ninafikiri kwa mwaka *almost* dola laki mbili *cost* yake.

Kwenye kifungu cha 5 eneo la biashara holela za *CD* zimezagaa mitaani za ngono kwa watoto wadogo. Unafikiri Mhe. Mwenyekiti, unachokipanda ndio unachokivuna, huwezi kupanda mpunga ukaja ukavuna shelisheli. Hatujawa tayari, tutapiga kelele siku zote humu. Serikali ni lazima itoe kauli kwa suala hili. Mimi nimeshawahi kupiga kelele si mara moja wala mbili katika kipindi cha maswali na majibu.

Katika kifungu cha 6 Ofisi za Masheha. Ipo haja wizara sasa hivi kuwajengea Masheha ofisi zao, sio kuwa majumbani. Leo imetokea jambo Sheha hayupo, lakini ofisi ipo. Utakwenda utaambiwa Sheha hayupo limeshatokea jambo, lakini wakishajengewa ofisi Masheha watakuwepo watendaji.

Kuhusu suala la mawakili. Watoto mpaka hawajaekewa mawakili wa kuwatetea. Nilipiga kelele Pemba sijui kama kaajiriwa ama hakuajiriwa mpaka leo muda umepita. Atawatetea nani watoto. Kuna wakati tulikwenda sisi kamati kabla haijamaliza muda wake, tulikwenda Kiinua miguu Magereza tukamkuta mtoto wa miaka 10 au 12 kaiba nazi sita tu, yupo ndani mwezi mzima. Kweli hakuna adhabu nyengine ya kufanywa mtoto kama yule, ya kufungwa kifungo cha nje ya kupewa pahali ya kwenda kufyeka. Hakuna wakili wa kwenda kumtetea. Mhe. Hija Hassan Hija, tulikuwa kamati hiyo pamoja na Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa, naye pia hayupo. Sasa watoto wetu watapata haki zao wapi, wawepo mawakili wa kuwatetea watoto.

Jengine Polisi imekuwa Masheikh sasa wanaowazowesha vituoni. Inapotokea janga wanaitwa wazee wanasawazishwa. Ninafikiri hivi sasa imefika wakati wale wanaopatanishwa, washtakiwa na wazee sasa hivi.

Suala jengine ni kuangalia Mabaradhuli na Wasagaji Zanzibar. Hili ninafikiri lipigwe marufuku. Itafutwe orodha yao waandikwe na wafahamishwe, ninafikiri ipo haja ya kuangalia hilo.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili nimuombe sana mwenyekiti wa kamati kuhusu mavazi. Mhe. *Haji* alihimiza hili suala naomba mwenyekiti ulipokee kwa mikono miwili. Mavazi ya watoto wetu hivi sasa hayaridhishi hata kidogo Mhe. Mwenyekiti. Hili suala uliangalie na ulipokee kwa mikono miwili. Kuna

zile nguo za majanga sasa hivi jana au juzi nimezungumzia au *skin tight*, ni vitu ambavyo vinavyoleta matamanio.

Jengine kwa kumalizia umasikini nao Mhe. Mwenyekiti, ni chanzo cha matatizo haya kuchangia. Nchi yetu hii imekuwa maskini kwa kiasi kikubwa sana. Leo mtu usiku pale anakwenda kuuza mikate yake ya boflo, susu lake moja ambapo hakeri mtu, ana watoto karibu kumi au kumi na tano anategemea mikate ile auze, leo Baraza la Mji wanakwenda kumnyanyasa mtu, wanaichukua mikate ile au pesa zake, atawalisha nini watoto wale.
Hebu tujiulizeni kweli usiku pale susu moja ana watoto kumi au sita, mkate wenyewe ni shilingi ishirini au tano faida, anakera nini pale, hata Baraza la Mji kwenda kumnyanyasa bure mtu yule usiku ule. Umaskini ni chanzo cha kuchangia migogoro hii. Atamkuta mtoto anakwenda kuomba peremende, apate nini. Umasikini ndio chanzo, lakini kila tukipiga kelele humu sisi hatusikilikani. (Makofi).

Lakini dini yetu inatwambia tumia mambo matatu; utakapoliona ovu, lisemee kwa mdomo wako, tumia mkono wako na mwisho uchukie. Hivyo, umasikini ni chanzo. Wale wanalipa halafu mikate yao ivurugwe. Leo ukitaka mkate uingie *super market* kwa Shamsu kule, ukanunue mkate utakiri magendo. Sasa utendaji gani huu. Tokea lini mkate wa boflo kuuzwa usiku, ni unyonge tu, nchi hii haina ajira. Ni kitu cha kusikitisha sana hichi. (*Makofi*).

Na hii kuhusu semina kuendeshwa vijijini nacho ni chanzo cha maporomoko. Sasa hivi visemina kibao vinaoneshwa vinapelekwa vijijini. Na hili nalo serikali iliangalie na kupiga marufuku kupeleka semina vijijini.

Ninafikiri baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, na mimi niungane sana na Mhe. Mgeni Hassan Juma, hoja yake madhubuti kabisa na maridadi kabisa.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kwa kumalizia mchango wako vizuri na sasa bado tuna orodha hapa ambapo kesho tukijaaliwa uhai, uzima na salama, baada ya taratibu za asubuhi tutaendelea na Mhe. Asaa Ohman Hamad, Mhe. Salma Mussa Bilali, Mhe. Salmin Abdalla Hamad, Mhe. Amina Iddi Mabrouk, Mhe. Rufai Said Rufai na Mhe. Kazija Khamis Kona na baadae watafuata Waheshimiwa Mawaziri Mhe. Zainab Omar Mohammed na Mhe. Abukakary Khamis Bakar na Mhe. Othman Masound.

Waheshimiwa Wajumbe kabla hatujaakhirisha Baraza hili, kuna tatizo hapa. Kuna taarifa ambayo imeletwa na Waziri wa Habari, Utamadun, Utalii na Michezo, inayosema kwamba asubuhi ya leo kulikuwa na uzinduzi wa

uwekaji wa nyasi bandia katika Uwanja wa Amani na kwa kuwa Wajumbe wa Baraza hili ndio walioishauri serikali kutekeleza mradi huo. Hivyo, inaonekana ni heshima kwa Wajumbe wa Baraza hili kupitia timu yao ya mpira wa miguu wawe wa mwanzo kucheza mechi rasmi kwenye Uwanja wa Amaan kwenye nyasi bandia. (Makofi).

Mechi hiyo imepangwa kufanyika siku ya tarehe 23/12/2013 saa kumi barabara za jioni baina ya timu ya mpira wa miguu ya Baraza la Wawakilishi na timu ya mpira wa miguu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.
Katika mechi hiyo, kauli mchezaji atakayefunga goli la kwanza katika uwanja wa Amaan kwenye nyasi bandia, atazawadiwa king'amuzi na *dish* la Azam *TV* pamoja na kulipiwa *air time* kwa muda wa mwaka mzima. (*Makofi*).

Kiingilio cha mechi hiyo kitakuwa ni bure na wananchi wote wanaalikwa kuhudhuria. Mgeni rasmi katika mechi hiyo atakuwa ni Mhe. Spika wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar. (*Makofi*).

Baada ya maelekezo hayo, sasa ninapenda kuchukua fursa hii kuliakhirisha Baraza hili hadi kesho siku ya Ijumaa tarehe 20/12/2013, saa 3.00 za asubuhi. Naomba kuakhirisha.

(*Saa 1.45 usiku Baraza liliakhirisha hadi tarehe 20/12/2013 saa 3. 00 asubuhi)*